ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI

SPIKA – MHE. PANDU AMEIR KIFICHO

1.Mhe. Kamal Basha Pandu	Naibu Spika/Jimbo la Rahaleo.
2.Mhe. Ali Mzee Ali	Mwenyekiti wa Baraza/Uteuzi wa Rais.
3. Thuwaibah Edington Kissasi	Mwenyekiti wa Baraza/Nafasi za Wanawake.
4.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	MBM/Waziri Kiongozi/ Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Jimbo la Mwanakwerekwe.
5.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Naibu Waziri Kiongozi/Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo/ Jimbo la Donge.
6.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	Kiongozi wa Upinzani/"Waziri Kivuli"–Afisi ya Waziri Kiongozi/Jimbo la Mgogoni.
7.Mhe. Haji Omar Kheri	Mnadhimu wa Upande wa Serikali/Jimbo la Tumbatu.
8.Mhe. Haji Faki Shaali	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Katiba na Utawala Bora/Mnadhimu wa Upande wa Upinzani/Jimbo la Mkanyageni.
9.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi/ Jimbo la Dimani.
19.Mhe. Ramadhan Abdulla Shaaban	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora/Uteuzi wa Rais.

11.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi Vya S.M.Z./Jimbo la Jang'ombe.
12.Mhe. Hamza Hassan Juma	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/ Jimbo la Kwamtipura.
13. Mhe. Machano Othman Said	Waziri wa Nchi, (AR) Mawasiliano na Uchukuzi./Jimbo la Chumbuni.
14. Mhe. Br.Gen. Adam C. Mwakanjuki	MBM/Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Uteuzi wa Rais.
15.Mhe. Samia Suluhu Hassan	MBM/Waziri wa Utalii/Biashara na Uwekezaji/Nafasi za Wanawake.
16.Mhe. Burhan Saadat Haji	MBM/Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/ Jimbo la Kikwajuni.
17.Mhe. Asha Abdalla Juma	MBM/Waziri wa Kazi Maendeleo ya Vijana,Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais.
18.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Makunduchi.
19.Mhe. Sultan Moh'd Mugheiry	MBM/Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/ Uteuzi wa Rais.
20.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Kiembesamaki.
21.Mhe. Zainab Omar Moh'd	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Kazi Maalum/ Nafasi za Wanawake.
22.Mhe. Idi Pandu Hassan	Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

23. Mhe. Mahmoud Thabit Kombo	Naibu Waziri wa Habari Utamaduni na Michezo/Jimbo la Mpendae.
24. Mhe. Mzee Ali Ussi	Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chaani.
25. Mhe. Khatib Suleiman Bakari	Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Bububu.
26.Mhe. Khamis Jabir Makame	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mtoni.
27.Mhe. Shawana Bukheti Hassan	Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Dole.
28.Mhe. Tafana Kassim Mzee	Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Uzini.
29.Mhe. Zahra Ali Hamad	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/Nafasi za Wanawake.
30.Mhe. Zakiya Omar Juma	"Waziri Kivuli"-Wizara ya Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Nafasi za Wanawake.
31.Mhe. Said Ali Mbarouk	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) na MBLM Fedha na Uchumi/Jimbo la Gando.
32.Mhe. Abdulla Juma Abdulla	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Tawala za Mikoa na Vikosi Vya SMZ/Jimbo la Chonga.
33.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) Kazi Maalum/Nafasi za Wanawake.

34.Mhe. Hamad Masoud Hamad	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Maji,Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Ole.
35.Mhe. Omar Ali Shehe	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chake-Chake.
36.Mhe. Rashid Seif Suleiman	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Ziwani.
37.Mhe. Mohamed Ali Salim	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mkoani.
38.Mhe. Asaa Othman Hamad	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Wete.
39.Mhe. Aziza Nabahan Suleiman	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Nafasi za Wanawake.
40.Mhe. Najma Khalfan Juma	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo/Nafasi za Wanawake.
41.Mhe. Muhyddin Moh’d Muhyddin	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji/Jimbo la Mtambile.
42.Mhe. Abdulla Mwinyi Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Unguja.
43. Mhe. Abass Juma Muhunzi	Jimbo la Chambani.
44.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini.
45.Mhe. Ali Denge Makame	Jimbo la Amani.
46.Mhe. Ali Haji Ali	Jimbo la Mkwajuni.

47.Mhe. Ali Moh'd Bakari	Jimbo la Tumbe.
48.Mhe. Ali Suleiman Ali	Jimbo la Kwahani.
49.Mhe. Ame Mati Wadi	Jimbo la Matemwe.
50.Mhe. Ame Ussi Juma	Jimbo la Nungwi.
51.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake.
52.Mhe. Anaclet Thobias Makungila	Jimbo la Fuoni.
53. Mhe. Asha Moh'd Hilal	Jimbo la Magogoni.
54.Mhe. Ashura Abeid Faraji	Nafasi za Wanawake.
55.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Nafasi za Wanawake.
56.Mhe. Dadi Faki Dadi	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Pemba.
57.Mhe. Fatma Abdalla Tamim	Nafasi za Wanawake.
58.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	Jimbo la Mji Mkongwe.
59.Mhe. Haji Mkema Haji	Jimbo la Koani.
60.Mhe. Hasnuu Moh'd Haji	Uteuzi wa Rais.
61.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani.
62.Mhe. Major Juma Kassim Tindwa	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Pemba.
63. Mhe. Juma Duni Haji	Uteuzi wa Rais
64.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope.
65.Mhe. Mkongwe Nassor Juma	Nafasi za Wanawake.
66.Mhe. Moh'd Kombo Mkanga	Jimbo la Chwaka.

67.Mhe. Mustafa Moh'd Ibrahim	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Unguja.
68.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake.
69. Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	Uteuzi wa Rais
70.Mhe. Omar Ali Jadi	Jimbo la Kojani.
71.Mhe. Pembe Juma Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Unguja.
72.Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu	Jimbo la Muyuni.
73.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake.
74.Mhe. Said Khelef Ali	Jimbo la Bumbwini.
75.Mhe. Salim Abdulla Hamad	Jimbo la Mtambwe.
76.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni.
77.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni.
78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde.

Ndg. Ibrahim Mzee Ibrahim	**Katibu wa Baraza la Wawakilishi.**

Kikao cha Tisa - Tarehe 22 Juni, 2010

(Kikao kilianza Saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Mwenyekiti (Thuwaibah Edington Kissasi) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ: Mhe. Mwenyekiti, naomba Kuwasilisha Mezani hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nchi, Afisi ya Rais Tawala za Mikoa na vikosi vya SMZ kwa Mwaka 2010/2011. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala: Mhe. Mwenyekiti, napenda Kuwasilisha Mezani Hotuba ya maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawa kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nchi Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Waziri Kivuli wa Wizara ya Nchi, Afisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ: Mhe. Mwenyekiti kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha Mezani hotuba ya Maoni ya Upande wa Upinza Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nchi, Afisi ya Rais Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ. Naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 1

Udhalilishaji wa Watoto

Mjumbe aliyeuliza swali hili ameliondoa.

Nam. 62

Darasa Maalum la Kusomesha Madaktari Zanzibar

Mhe. Hija Hassan Hija – Aliuliza:-

Serikali imefanya jambo zuri sana kuwashawishi wenzetu wa Cuba kufungua darasa maalum la kufundisha madaktari hapa Zanzibar *(Zanzibar Medical*

School) na kutoa walimu na vifaa kwa ajili ya darasa hilo ambalo linaendelea vyema.

(a) Ni wanafunzi wangapi wanaosoma katika darasa hilo; na

(b) Wanafunzi hawa wanahitaji kupata vifaa maalum kwa ajili ya kufanyia mazoezi ya vitendo (*Practical*) likiwemo Gadava (maiti). Je vifaa hivyo vinapatikana ipasavyo wakiwemo hao gadava.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake Nam. 62 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Mwenyekiti, wanafunzi wanaosoma katika darasa la mafunzo ya Udaktari linaloendeshwa kwa mashirikiano na Serikali ya Cuba ni 38 kwa Unguja na 12 kwa Pemba; na

(b) Vifaa maalum kwa ajili ya kufanyia mazoezi ya vitendo katika darasa hilo (*practical*) vinapatikana kulingana na mahitaji ya uendeshaji wa mafunzo hayo. Aidha napenda kumfahamisha Mhe. Mwakilishi kuwa mafunzo hayo yanaendeshwa kwa kufuata mitaala yake maalum (*curriculum*) ambapo vifaa hunununliwa hatua kwa hatua kulingana na mwenendo wa mafunzo yenyewe. Kwa hivi sasa wanafunzi katika darasa hilo wanajifunza elimu ya mwili na viungo vyake (*Anatomy*) kwenye kimpyuta pamoja na mafunzo ya vitendo vijijini ambapo vifaa vyake kwa sasa vinapatikana na wizara pia inaendelea na juhudi zake za kuimarisha kliniki na maabara za Hospitali ya Mnazi Mmojana Chuo cha Afya Mbweni ambazo zinatumika kwa mafunzo hayo.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu vifaa, wanafunzi hawa wamepatiwa vifaa vya kusomeshea vikiwemo Computa, *video power point*, nakadhalika. Hivi ndivyo vifaa wanavyosomeshewa. Kuhusu Gadava, naomba kutoa maelekezo kuhusu neno "*Ganavar*" ni maiti na kuweko kwenye '*formalin'* ambayo inazuwiya kuoza maiti hiyo na imekuwa na kumekuwa na uzoefu kwamba wanafunzi wa kidaktari wapasue maiti hizo.

Lakini katika program hii mpya ambayo tumejifunza kutoka ndugu zetu wa Cuba wanafunzi hao wanaangalia binaadamu aliye hai *x-ray*, *ct scan,* na pia wanajifunza *anatomy* kwenye

compyuta/CD compyuta za DVD. Mfumo huu wa kusomesheya umekubalika hata katika baadhi ya nchi ikiwemo Cuba.

Napenda kulihakikishia Baraza lako Tukufu kwamba '*quality'* ya madaktari watakao hitimu skuli yetu hiyo ni ya Kimataifa kama ziliopo katika skuli za namna hizi zilizopo Cuba na nchi nyengine.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, baada ya majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri naomba niulize suala la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwa kuwa amesema kwamba hakuna haja ya kutumia Gadava kama maiti maalum wa kufanyia vitendo na mazoezi ya wanafunzi wetu. Je, anakusudia kunambia kwamba wale wanafunzi ambao mara nyengine hupelekwa Tanzania Bara pia sasa hawatahitaji tena kupelekwa kwa sababu vifaa vilivyokuwepo Zanzibar vya *compyute, Video power point* vinatosha .

Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Mwenyekiti, hakutokuwa na haja sasa hivi wanafunzi hao kupelekwa Bara. Watasoma hapa hapa masomo yao kwa kupitia kwa huo mfumo ulioandaliwa na baadaye kama wakishakumaliza baada ya miaka sita tumeweka kama mtu anataka ku-*specialise* atakwenda Cuba ku- *specialise* kwa miaka miwili kwa kozi ambayo anaihitaji.

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Mwenyekiti, baada ya majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kidogo niongeze.

Sasa hivi Zanzibar tunawapeleka vijana wetu kusomea udaktari nchi mbali mbali, Uturuki, Tanzania Bara, Wingereza, Amerika kila sehemu ya ulimwengu. Ninachokisema mimi ni kwamba nimezungumza na Dokta Gilbato huyu ni Mkuu wa Madaktari wa Cuba aliyekuwepo hapa Zanzibar akanambia umuhimu wa Gadava sasa ulimwenguni haupo kwa sababu sasa hivi dunia haipo katika kiza. Sasa hivi ni ulimwengu wa sayansi na teknolojia.

Mhe. Mwenyekiti, nakipongeza Chama cha Mapinduzi nampongeza Mhe. Makamo wa Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi Dokta Amani Abeid Karume, nampongeza Jemedari, Kamanda Mhe. Mansour Yussuf Himid kwa kuondosha kiza Pemba. Hivi sasa hivi tumeweka computer, tumeweka ma-internent kwa wanafunzi wetu wanaosomea Udaktari pale Chakechake. Kwa hivyo hakuna rai ya kusomesha kwa Gadava, ma CD, maDVD, ma-internent inaona mwenyewe hivi hivi vitu wazi wazi ma- *Xray*, tena Gadava ya nini.

Mhe. Mwenyekiti, lakini bado tutaendelea kupeleka wanafunzi wetu nchi za nje kusomea udaktari.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii pamoja na Naibu wake naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti, na mimi niungane kwa dhati kabisa kumshukuru Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi lakini pia kumpongeza sana Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi kwa ilani ya asilimia 100 iliyopatikana au zaidi katika kuleta umeme Pemba. Hiyo ni hongera.

Mhe. Mwenyekiti, umeme ni changamoto ya kuhakikisha ufanisi wa kazi unapatikana katika nyanja mbali mbali na nyanja moja iliyokuwa ikilalamikiwa ni ya afya, lakini sasa hivi naamini manung'uniko hayo yatakuwa hayapo.

Kwa kuwa Wizara imejiandaa vyema kuhakikisha kwamba wanafunzi hao wanasomeshwa ili kuondoa kero la kukosekana madaktari katika sehemu zetu za Unguja na Pemba. Je, kwa upande wa Pemba Wizara imejiandaa vipi kuwadhibiti hawa watakaokwisha kumaliza masomo yao wasihame kurudi Unguja na kuepusha kuwepo kwa upungufu wa madaktari ambao hatuutaki utokee.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nimpongeze Mhe. Ali kwa kumshukuru Mhe. Rais kwa kazi yake nzuri aliyoifanya pia na kumpongeza Waziri wa Maji na Umeme kwa hatua aliyofikia hata kuweza kutuleta umeme Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu suala lake vipi tutawadhibiti watakaomaliza masomo. Tutajitahidi kwa kuwapatia maslahi mazuri ili waweze kufanya kazi zao vizuri na pia tutajitahidi kwamba tunahakikisha kuwa wanabaki hapa nchini kwetu wasiweze kuondoka kwenda nchi nyengine.

Jengine mtu kubaki nchini kwake kufanya kazi hili ni suala la uzalendo linalotoka ndani ya moyo wake. Kwa hivyo sisi tutajitahidi kuwanasihi madaktari wetu baada ya kwisha kumaliza kusoma kwa vile elimu wameipata hapa, serikali ndio iliyowasomesha kwa hivyo tutawaelekeza na tutajitahidi kadri ya uwezo wetu kuwaomba kuwa wabakie hapa nchini na sisi tutajitahidi kuwaweka katika mambo yao yawe mazuri ili wafanye kazi hapa nchini.

Mhe. Zakia Omar Juma: Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, mimi nikuwa nina swali moja la dogo tu nilipenda kujua katika kulizwa maswali ya msingi kifungu cha (b) kimeelezea kuhusu vifaa ikiwemo hawa Gadava. Utaratibu katika mafunzo na fani hii ya *pathology* hawa maiti inakuwa hamufanyii wale watu wenu, inakuwa mnabadilishana baina ya nchi na nchi. Nilikuwa napenda

kujua Tanzania tunapokea kutoka wapi tunaobadilishana nao au wale wanaotupa ni nchi gani.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Mwenyekiti, kuhusu suala la magadava sasa hivi tumeachana nayo. Sasa hivi tunatumia watu wazima ambao wanakuwepo kwenye *computer/CD, DVD, Ct-scan* na *X-ray*. Kwa hivyo suala la Gadava tumeliacha.

Nam. 56

Vifaa vya Upakuzi wa Mizigo Bandari za Pemba

Mhe. Ali Denge Makame – Aliuliza:-

Je, Mhe. Waziri, wizara yako ina mpango gani wa kuongeza vifaa vya upakuzi wa mizigo kwa ajili ya Bandari za Pemba.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi – Alijibu**:-**

Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetujaali kuwa wazima na kuhudhuria Kikao cha Baraza . Baada ya hapo kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake namba 56 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti katika kuimarisha huduma za upakizi na upakuzi Bandarini wizara yangu kupitia Shirika la Bandari ina mpango wa kununua vifaa vipya vya kuhudumia mizigo katika Bandari zake Unguja na Pemba. Vifaa hivyo vitanunuliwa ndani ya mwaka huu wa fedha baada ya kukamilika taratibu za kupata mkopo kutoka Benki ya Watu wa Zanzibar.

Kati ya vifaa vitakavyonunuliwa tunakusudia kupeleka kreni mbili (2) za tani 20 na tani 10 huko Pemba kwa ajili ya Bandari ya Mkoani.

Mhe. Said Ali Mbarouk: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali la nyongeza kama hivi ifuatavyo. Kwa vile hali ya Bandari ya Mkoani ilivyo kwamba kuna ziwa kubwa la maji hivi inayumkini pale kule kreni ya tani 20 ya kupakua mizigo au wanakusudia kuna aina ya kreni zinazoelea kwenye maji za kupakuliwa mizigo.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Mwenyekiti, anaelewa kwamba pamoja na mambo mengine lakini suala zima la kutoama maji bandarini tunalielewa Mkoani kwa hivyo pamoja na hilo suala

la kununua Kreni lakini vile vile suala la kuondoka kwa maji pale tutalifanyia kazi kabla ya kreni hizo kufika Pemba. Ahsante.

Mhe. Moh'd Ali Salum: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu sikumfahamu

Mhe. Naibu Waziri naomba nimuulize swali lifuatalo.

Alipotuambia katika mwaka huu fedha kakusidia hizi siku nane zilizobaki.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Mwenyekiti ninapozungumzia mwaka wa fedha kwa upande wa Bandari unaanzia January wala sio kama ilivyo hapa. Lakini vile vile suala hili la upatikanaji wa hizo kreni zitategemea na jinsi gani tutaweza kupata mkopo katika Banki ya Zanzibar kama nilivyozungumza katika suala langu la msingi kabisa.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kupata kuuliza swali la nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti, gati ya Mkoani tunaijua na tumepiga makelele siku nyingi sana na tuliambiwa tunasubiri mpaka ikisha *settle* katika kuzama kwake ndio itengenezwe. Leo ikiwa gati ile tunasema kuwa ni mlango wa kimataifa na hali ndio ile na Mheshimiwa badala ya kuleta mpango wa kuitengeneza ile gati kwanza ikafanana na hiyo sifa yake anasema ataleta krena maji ataondoa. Ina maana kubakia shimo vile na kila siku kujaa maji itakuwa ndio tumeifanya lolote hai kwa sababu ya bandari inayotumika sana.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka niwaombe Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwamba suala la kuondoa maji pale linahitaji kwanza apatikane mkandarasi ambaye ataweza kufanya usanifu mzuri na sio suala tu la kwenda pale ukaripua tu. Tunaweza tukenda pale tukaripua baada ya siku mbili tatu kazi ile ikaonekana haikufanikiwa vizuri.

Tunachofanya ni kuona kwamba ni nani anao uwezo mzuri wa kuweza kuhakikisha kwamba pale mahala patafanywa kazi inayokusudiwa na kuondosha tatizo. Kwa hivyo mara baada ya kukamilika utaratibu huo basi na masuala mengine yote yatafuatilia kama kawaida kama nilivyosema katika jibu langu la mwanzo.

Nam. 76

Utoaji wa Ardhi bila ya Ridhaa ya Watumiaji

Mhe. Hija Hassan Hija – Aliuliza:-

Hivi karibuni wimbi la migogoro ya ardhi imekuwa ikiongezeka hapa Zanzibar. Tumewahi kusikia malalamiko ya wananchi hususan maeneo ya Nungwi na Pwani Mchangani wakidai kuwa Idara ya Ardhi na Upimaji imekuwa ikitoa maeneo ya wananchi kwa watu maarufu au wenye fedha bila ya kufuata taratibu.

(a) Je, Mhe. Waziri nini msimamo wa Wizara yako juu ya madai hayo?

(b) Je, utakubaliana nami kuwa baadhi ya watendaji hutumia vibaya ile dhana ya "Ardhi ni mali ya Serikali na kuwadhulumu wananchi kwa maeneo wanayoyataka?

(c) Kwanini wananchi wanapodai kwamba eneo fulani ni lao kwa ushahidi, Wizara yako haichukui hatua ya kukaa nao kwanza na kupata ufumbuzi?

Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake Nam.76 lenye vifungu (a,(b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, kufuatia Mapinduzi Matukufu yaliyofanyika hapa Zanzibar mwaka 1964, Ardhi yote Visiwani Zanzibar ilitangazwa rasmi kuwa mali ya serikali na kwa hivyo serikali ndio mmiliki wa ardhi yote iliopo nchini Zanzibar. Serikali huwapa wananchi wake haki za matumizi ya ardhi kwa madhumuni mbali mbali kama ujenzi wa nyumba na kilimo.

Aidha zipo Ardhi khalia ambazo hakuna mtu aliyepewa haki za matumizi yake. Wizara yangu ina jukumu la kupanga matumizi mbali mbali ya ardhi. Kwa mujibu wa mipango ya matumizi ya ardhi ambayo hupitishwa na serikali. Kwenye utekelezaji wa mipango huo wakati mwengine hata zile ardhi ambazo serikali imetoa haki ya matumizi ya ardhi kwa wananchi mbali mbali zinaathirika. Kwa mujibu wa Sheria ya Umilikaji Ardhi, kama inavyoeleza Katiba ya Zanzibar.

Serikali ina haki ya kuingiza ardhi yoyote kwenye mpango wa matumizi ya ardhi hata kama kuna wananchi wenye haki ya matumizi ya ardhi hiyo. La

msingi ni kwamba katika uchukuaji wa ardhi ambazo zina haki ya matumizi ya ardhi aliopewa mwananchi, mwananchi anaehusika anatakiwa kulipwa fidia ya ardhi, na hatakiwi kukataa na kuzuia mpango wa matumizi ya ardhi kwa serikali, kufanyika kwenye ardhi aliopewa haki ya kutumia. Kwa pande wa Nungwi za Pwani Mchangani ambapo Mheshimiwa Mwakilishi ametaja ni kwamba maeneo yote hayo yako kwenye mipango ya Matumizi na Uendeshaji Ardhi. Eneo la Nungwi analozungumzia limepangwa kwa Uendeshaji wa ujenzi wa Hoteli za Kitalii na ardhi imegaiwa baada ya utaratibu nilioelezea wa kupanga matumizi ya ardhi na kulipa fidia kufanyika. Eneo la Pwani Mchangani limepangwa kwa kuendeleza makaazi hasa kwanza kwa kuzingatia ukuaji wa mahitaji ya makaazi kwa wananchi wa Pwani Mchangana na Matemwe. Upangaji umezingatia huduma nyengine muhimu na kwa hivyo viwanja vimetengwa kwa madhumuni hayo na kupewa kwa taasisi zinazohusika.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake.

(a) Mhe. Mwenyekiti, kwa vile wizara yangu imetekeleza majukumu yake kwa mujibu wa mpango uliopitishwa na serikali, msimamo ni kuendelea na utekelezaji wa majukumu hayo. Hata hivyo, Wizara yangu itahakikisha kwamba muda wote wa utekelezaji unaheshimu Sheria na Katiba. Kwa hivyo kwa wale ambao watathibitishwa kuwa wanastahiki kulipwa fidia wanalipwa ipasavyo, aidha Wizara itahakikisha kwamba ardhi imepangwa na kutolewa kwa mujibu wa mpango wa kitaifa wa matumizi ya Ardhi ambapo umepitishwa na serikali;

(b) Dhana ya kua ardhi ni mali ya serikali inatakiwa itumike kwa utaratibu kama niliioueleza kwenye utangulizi wangu. Kama baadhi ya watendaji wanaitafsiri na kuifanyia kazi kinyume na hivyo ni kosa. Wizara yangu ingependa kupata mifano hai ya madai ya namna hii ili ifanye uchunguzi na ikithibiti kuwachukulia hatua watendaji wanaojihusisha na dhulma hizo; na

(c) Mhe. Mwenyekiti, wizara yangu inaheshimu sana haki za wananchi juu ya ardhi mbali mbali, kwani pale inapothibitishwa haki ya mtu kwenye ardhi, wizara yangu hutoa Hati rasmi ya haki ya matumizi ya Ardhi kwa muhusika, au kwa maeneo ya uwekezaji, Wizara yangu huhakikisha kwamba mwenye haki ya ardhi hiyo anakubaliana na muwekezaji kwanza. Mhe. Mwakilishi

atakubaliana mimi kwamba wapo baadhi ya watu wanashindwa kuthibitisha haki zao juu ya ardhi kwa vile wanazozidai mara nyingi huwa ni ardhi khalia.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na nampongeza Mhe. Waziri nimezoea kujibiwa maswali yangu na Mhe. Naibu Waziri nilipomuona yeye leo nilishtuka sana.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri nina masuala madogo sana ya nyongeza. Tatizo lililokuwepo hapa kwa mujibu wa taaluma iliyotolewa Barazani ni ukosefu wa elimu ya kujua matumizi na haki ya ardhi kwa wananchi.

(a) Je, jukumu hili la matumizi ya ardhi na jukumu hili la kuwaelewesha watu kwamba ardhi ni mali ya serikali kama ilivyotangazwa na Mapinduzi ya 1964 ni la nani, la wizara yako au wizara gani inapaswa kutoa elimu hii?

(b) Maeneo ya Pwani Mchangani na Nungwi ambayo wananchi wanayalalamikia inaonekana serikali imekubali kutoa fidia au imetoa fidia je, wale wahusika wizara yako inawajua?

Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi: Mhe. Mwenyekiti, kwanza kashtuka kuona mimi najibu swali lake lakini mimi nasema kwamba mimi na Tafana ndio huyo huyo.

(a) Ardhi ni mali ya serikali nafikiri tangu September 8 mwaka 64 ndipo lilipotoka tangazo rasmi la kutaifisha ardhi yote na kuwa mali ya serikali. Elimu tangu 64 hadi hivi sasa inaendelea kutolewa. Kilichotokea hivi sasa ni kuongezeka kwa bei ya ardhi. Mfano mwaka 2000 eka moja ya ardhi kwenye fukwe hasa Unguja ilikuwa wananchi wanapata fidia kama dola elfu 20. Hivi sasa eka hiyo hiyo inakaribia dola laki moja hamsini na kuendelea. Kutokana na mazingira ya kuongezeka mahitaji ya ardhi, kuongezeka bei ya ardhi watu kwa makusudi wanafanya haya mambo hawayaoni.

(b) Eneo la Pwani Mchangani na Matemwe tunalolizungumzia na kama nimemfahamu Mheshimiwa sahihi hakuna suala la ulipaji wa fidia hata kidogo. Kwa sababu nyote mtakumbuka na wizara yangu ilileta mbele yenu gazeti rasmin la serikali la mwaka 1997 maeneo yote yale tuliyozungumza Kiwengwa hadi Pwani Mchangani yalipimwa rasmin tangu mwaka huo kwani ilikuwa ni

ardhi halia na ushahidi tumeleta kwenu hapa. Hili suala la ulipaji wa fidia kwa maeneo yale naliyopimwa viwanja hivi sasa kwa shughuli za serikali na jamii yenyewe kwa shughli zao na viwanja kuwapatia wananchi wengineo kwani ni haki yao kwa mujibu wa katiba ya nchi hii hakuna suala la ulipaji wa fidia. Mhe. Mwenyekiti, kwa bahati mbaya sana lililokuja kutokezea pale sipendi kutumia maneno haya Mhe. Mwenyekiti, lakini zaidi ni choyo na fitina na kuwakoroga wananchi na kuwatia sumu dhidi ya serikali yao, kwa sababu hata viongozi wa Serikali za Mitaa, Wilaya, Mkoa na vyama vya siasa tuliwapelekea ushahidi ule. Mhe. Mwenyekiti, wizara yangu imefanya jitihada kubwa ya kutoa elimu kwa wananchi wale. Hilo ndilo liliopo.

Mhe. Haji Faki Shaali: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na namshukuru Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri lakini hata hivyo na mimi napenda kuuliza swali moja la nyongeza lenye (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, tunafahamu sote kwamba ardhi ni mali ya serikali lakini kuna ardhi nyengine au tunaweza kuita mashamba yamemilikiwa na watu wa nyaraka, lakini inatokezea shamba lile lile ambalo mtu ana hati au warka baadaye akanyang'anywa akapewa mtu mwengine na yule mtu mwengine na yeye akapewa hati, kwa hivyo ikawa shamba moja lile lina watu wawili wenye hati. Mmoja pengine tokea wakati wa ukoloni na mmoja hivi sasa.

a) Je, kuwamilikisha wananchi wawili shamba moja na kila mmoja ana hati hapa hatusababishi migogoro?

b) Kuna baadhi ya viongozi wengine baada ya mapinduzi walijichukulia ardhi bila ya kutaifishwa wakaifanya yao, na mpaka hii leo bado ardhi ile haijataifishwa rasmi. Je, nalo katika suala kama hili Mhe. Waziri anatuambia nini?

c) Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi kumejitokeza tatizo kwa wananchi wenye heka wakifariki Masheha huwarithisha watoto wao yale maheka. Je, hili nalo Mhe. Waziri atatuambia nini?

Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi: Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana Mhe. Mwakilishi kwa suala lake hili kwani litanisaidia kutoa ufafanuzi wa mambo mawili matatu ambayo ni ya msingi kabisa yanayohusiana na ardhi.

Mhe. Mwenyekiti, tunapozungumza mwananchi kupewa hati mbili, moja ya ukoloni na moja baada ya mapinduzi. Mhe. Mwenyekiti, serikali ilipotaifisha

ardhi mkoloni hayupo tena na hati zake hazipo tena, ikiwa Sultani, ikiwa Mwingereza, Baraza la Mapinduzi lilipotoa tamko la kutaifisha ardhi, hati zote zile hazikuwa na uhalali tena. Mhe. Mwenyekiti, japokuwa kuna baadhi ya misingi ya hati zile zilikubaliwa hasa ardhi zilizokuwa za wakfu, hizo hazikubadilika zimeendelea tangu wakati ule mpaka hivi sasa wakfu zinaendelea kuheshimiwa.

Mhe. Mwenyekiti, hii dhana ya viongozi ya kujichukulia ardhi baada ya mapinduzi na hili nalo hata kwa kipindi hiki linazungumzwa sana kwamba viongozi wanajichukulia tu. Mhe. Mwenyekiti, ardhi iliyotaifishwa kwenye gazeti rasmi na kuingizwa kwenye gazeti rasmi au ardhi iliyohodhiwa yote inahesabiwa kwamba ardhi imetaifishwa, pamoja na mali isiyohamishika.

Mhe. Mwenyekiti, ziko nyumba zilizotaifishwa na serikali lakini hazikutaifishwa rasmi kupitia gazeti rasmi la serikali. Lakini sheria ya nchi hii zinaeleza pia kwamba nyumba iliyoachwa na huyo aliyemiliki basi inahesabiwa kuwa imetaifishwa. Mhe. Mwenyekiti, masheha kurithisha heka ya watu hilo ni kosa, sheha hana mamlaka ya kumrithisha mtu yeyote ardhi. Kwa mfano, mimi leo nimefariki nina shamba langu Kiboje hivyo sheha hana haki ya kuwamilikisha hata watoto wangu hiyo sio kazi yake. Kazi yake yeye ataulizwa tu je, hili shamba kweli lilikuwa la marehemu Mansour Yussuf bin Maftaha, wakurithisha ni wengine yeye hana haki hiyo.

Kwa hivyo, kama sheha anafanya hivyo ni dhambi na kinyume na sheria. Lakini sheha ana umuhimu sana katika masuala yote ya matumizi na umilikishaji wa ardhi kwa sababu lazima aulizwe kwa sababu yeye ndiye anayewatambua watu wake. Baada ya hapo tena ndio inakuja Wilaya, Mkoa na hatimae wizara yangu hufuata taratibu ambazo zinapaswa kufanya kwa mujibu wa sheria. Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, kwa kuzingatia hali halisi ya ardhi ambayo ilikuwa na migogoro mingi sana hapa nchini, wizara kupitia serikali kuu ilianzisha Mahakama maalum ya ardhi na tegemeo letu kwamba mahakama hii inaamua haki na wananchi ni wajibu wao waitambue na waielewe pindi wanapokutwa na matatizo wajue wapi wanakimbilia.

Je, Mhe. Waziri kwa kuzingatia hilo ni taaluma gani ya wizara imechukua ili wananchi wetu wenye usumbufu au matatizo wanayoyapata kukimbilia katika mahakama hiyo ili wapate msaada.

Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi: Mhe. Mwenyekiti, sheria ya kuanzishwa kwa Mahakama ya Ardhi iko tangu miaka ya 94, lakini baada ya kuteuliwa kwangu mwaka 2005 na kujionea mimi mwenyewe kabla ya kuteuliwa kuwa waziri wa wizara hii juu ya muelekeo hasa ya migogoro ya ardhi tulijihimu na kuanzisha Mahakama ya Ardhi. Mahakama hiyo ilipaswa kuwepo kwenye kila Mkoa wa nchi yetu ili kukidhi mahitaji ya wananchi kwa pale ambapo wanahisi hawakutendewa haki kwa lile ambalo wanahisi ni haki yao, mwananchi anaweza kudhania kwamba ile ni haki yake lakini ikawa sio au inaweza kuwa ni haki yake lakini hakupewa haki yake hiyo.

Tumeanzisha kwa Mahakama moja hivi sasa tuna wenyeviti wawili ambao wanamsaidia mwenyekiti kwa hivyo tuna Mahakimu watatu hivi sasa ambao wanasikiliza kesi hizo. Kama mtakapokuja kusikia kwenye uwasilishaji wa hotuba ya bajeti ya wizara yangu ya malalamiko imepungua, kasi ya kusikiliza kesi kwa kiasi nayo imepungua lakini bado jitihada zinahitajika kuhakikisha kwamba Mahakama hizi zinaongezeka kwa haraka ili tupate kuwatendea haki yao wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, tumeshaanisha maeneo mawili ambayo yana matatizo kushinda maeneo mengine yoyote nchini mwetu ni Kaskazini Unguja na Kaskazini Pemba. Majengo tumeshayaanisha na tunategemea pengine kwenye mwaka ujao wa fedha kazi ya ujenzi wa Mahakama hizo na kupata mahakimu ili kuongeza kasi ya usikilizwaji wa kesi hizi utaongezeka. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe kabla hatujaendelea leo tumefikiwa na wageni kutoka Kigoma. Tuna Koplo Juma na Koplo Swahiba. Waheshimiwa Wajumbe askari hawa itakumbukwa kwamba mwaka jana moja ya Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ilifanya ziara ya kwenda Mkoani Kigoma kwa kazi za Baraza. Wakiwa katika ziara ile kwa bahati mbaya walivamiwa na majambazi. Lakini kwa bahati nzuri walikuwa na maaskari ambao walikuwa wakiongozana nao kwenye ziara ile na waliweza kuwaokoa katika matatizo hayo.

Itakumbukwa pia kwamba askari hao walialikwa kwa mashirikiano ya Baraza na Wizara hii ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi waliweza kuja hapa na wakaweza kusalimia tuliwaona na kupitia Baraza hili tutakumbuka pia kuwa tuliomba walinzi hao wapatiwe mafunzo. Kwa bahati nzuri miongoni mwao wawili walikuwepo hapa Zanzibar kwa mafunzo ndio hawa tulioletewa hapa leo. Kwa hivyo, kupitia Baraza hili tunawapongeza sana kwa kuhitimu mafunzo yao na wameona kabla hawajarudi Kigoma kuendelea na kazi basi wapite hapa kusalimia. Kwa hivyo, na sisi tunawakaribisha sana.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011
Wizara ya Nchi Afisi Rais Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ: Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwa Baraza lako tukufu kwamba sasa likae kama kamati ili ipate kupokea, kuzingatia na hatimae kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Tsh. 28,329,973,000/= kwa Wizara ya Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ kwa kazi za kawaida na kazi za maendeleo kwa mwaka wa fedha wa 2010/2011.

Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote shukurani zote zimuendee Mwenyezi Mungu Muumba wa Mbingu na Ardhi, mwenye sifa za kufisha na kuhuwisha na ambaye ametuwezesha kuwa wepesi wa kutekeleza majukumu yetu tulokuwa nayo kwa kipindi cha uongozi wangu. Aidha, kikao hiki kina umuhimu wa pekee katika historia ya nchi yetu kwani kinafanyika miezi mitatu (3) kabla ya uchaguzi mkuu wa mwaka huu wa (2010) na kumalizika kwa kipindi cha pili cha awamu ya sita ya SMZ.

Mhe. Mwenyekiti, naomba pia kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kuiongoza nchi yetu kwa amani na utulivu. Aidha, nawashukuru Viongozi wote wa Chama na Serikali ambao wameshirikiana pamoja katika kipindi chote cha awamu ya Sita. Miongoni mwao ni Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dr. Amani A. Karume, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dr. Jakaya M. Kikwete, Makamo wa Rais Mhe. Dr. Ali Moh'd Shein, Waziri Mkuu Mhe. Mizengo Pinda, Rais Mstaafu Mhe. Benjamin W. Mkapa, Mzee wetu Mstaafu Mhe. Ali Hassan Mwinyi, Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais Mstaafu wa awamu ya tano Dr. Salmin Amour Juma na Viongozi wengine mashuhuri wa Chama na Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, naomba pia nimshukuru na kumpongeza kwa dhati Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dr. Amani Abeid Karume kwa kuiwezesha nchi yetu kuwa na amani, utulivu na maendeleo endelevu pamoja na misukosuko ya Kiuchumi, Kijamii na Kisiasa na mengineyo.

Mhe. Mwenyekiti, niruhusu pia nimshukuru Waziri Kiongozi Mhe. Shamsi Vuai Nahodha kwa namna alivyokuwa karibu na kupokea miongozo ya viongozi wake kama vile Mhe. Rais wa Zanzibar, Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, Makamo wa Rais na kuiwasilisha kwa watendaji

wenzake. Aidha, tunampongeza sana jinsi alivyolivalia njuga suala la kuzipatia ufumbuzi Kero za Muungano.

Mhe. Mwenyekiti, nakuomba pia uniruhusu nitoe shukurani zangu za dhati kwa Kamati zako za Kudumu hususan za Katiba, Sheria na Utawala chini ya Mwenyekiti wake Mhe. Haji Omar Kheri – Mwakilishi wa Jimbo la Tumbatu na Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali (*PAC*) ikiongozwa na Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji Mwakilishi wa Jimbo la Mji Mkongwe.

Mhe. Mwenyekiti, kupitia kwako naomba pia nikushukuru wewe binafsi pamoja na watendaji wako wote wa afisi yako wakiwemo Naib Spika, Wenyeviti, Waheshimiwa Wawakilishi, Katibu wa Baraza, Makatibu wa Kamati, Maofisa na wafanyakazi wote kwa kuzitekelea dhamana za Baraza kwa ufanisi.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo, naomba sasa niwasilishe maelezo ya utekelezaji wa wizara yangu kwa mwaka 2009/2010 pamoja na mwelekeo wa wizara yangu kwa mwaka wa fedha wa 2010/2011 unaoanza mwezi wa Julai 2010.

UTEKELEZAJI

Mhe. Mwenyekiti, katika kutekeleza mipango na majukumu ya mwaka 2009/2010, bado wizara imezingatia mpango wa utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005/2010; Mpango wa Matumizi wa Muda wa Kati (*MTEF*); Mkakati wa Taifa wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini (MKUZA) na Malengo ya Dira ya Taifa ya mwaka 2020.

Mhe. Mwenyekiti, wizara yangu ina Idara Kuu nne (4), Idara ya Mipango na Sera; Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; Usajili na Utoaji wa Vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi na Afisi Kuu – Pemba. Aidha, wizara yangu inaratibu na kusimamia Idara Maalum tano (5) za Vyuo vya Mafunzo (MF); Zimamoto na Uokozi (KZU); Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM); Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU); na Kikosi cha Valantia (KVZ).

Mhe. Mwenyekiti, wizara yangu kwa jumla ina majukumu ya msingi ambayo yanaonekana hapo chini.

1. Kusimamia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005/2010 katika Wizara na Taasisi zake.
2. Kujenga Uwezo wa Wizara na Taasisi zake (*Capacity Building*) kwa :-
    - Kuwaendeleza watendaji wake Kielimu;

- Kuwapatia usafiri na vitendea kazi; na
- Kuwatengenezea mazingira mazuri ya kazi (*Conducive Working Environment*) kwa kukarabati majengo; kutafuta samani n.k.

3. Kuratibu na kusimamia marekebisho ya Sera na Sheria zilizo chini ya Wizara.
4. Kuimarisha Ulinzi na Usalama wa raia na malizao.
5. Kuratibu na kusimamia mipango ya maendeleo ya wananchi kupitia Mafunzo Shirikishi Jamii/ O & OD kwa mashirikiano na Miradi mbali mbali – kama vile *PADEP, ASSP/ASDP-L; MACEMP; JP5; UNICEF; UKIMWI; ZUSP; MKURABITA N.K.*
6. Kushirikiana na Taasisi nyengine katika kuandaa na kuadhimisha Sherehe za Kitaifa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuyatekeleza malengo na majukumu ya wizara na taasisi zake, kwa mwaka 2009/2010, Baraza la Wawakilishi lilituidhinishia matumizi ya Tsh. 25,943,270,000 zikiwa Tsh. 1,875,000,000 kwa shughuli za maendeleo na Tsh. 24.068,270,000 kwa kazi za kawaida. Hadi kufikia mwezi wa Juni 2010 wizara imepokea Tsh. 23,223,967,868 sawa na asilimia 90 zikiwa Tsh. 21,358,967,868 sawa na asilimia 89 kwa kazi za kawaida na Tsh. 1,865,000,000 sawa na asilimia 99.5 kwa shughuli za maendeleo kama kiambatanisho namba 1 kinavyoonyesha.

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako na Wajumbe wa Baraza lako tukufu, sasa naomba mpokee utekelezaji wa malengo kwa mwaka 2009/2010 na mapango wa mwaka 2010/2011 kwa wizara yangu na Taasisi zake kama ifuatavyo:-

IDARA YA MIPANGO NA SERA

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Mipango na Sera bado inashughulika na utekelezaji wa kuratibu shughuli za wizara pamoja na kuunganisha wizara na taasisi nyengine za ndani na nje ya wizara. Aidha, idara hii hutoa miongozo na maelekezo ya kitaalamu kwa watendaji wa wizara na taasisi zake kwa lengo la kuzidisha ufanisi wa kazi.

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Mipango katika kipindi cha 2009/10 iliidhinishiwa Tsh. 803,890,000 na hadi sasa, idara imepokea Tsh. 746,537,215 sawa na asilimia 93. Mgawanyo wa fedha upo kwenye kiambatanisho namba 1.

Mhe. Mwenyekiti, idara hii katika kipindi cha 2009/10 ilijipangia kutekeleza malengo yake makuu matatu (3) na hadi muda huu idara:-

i) Imewaendeleza watendaji katika fani mbali mbali kiambatisho namba 2 kinaonesha; na

ii) Idara kwa kusaidiana na idara nyengine za wizara imeweza kuratibu shughuli zote za uandaaji wa sera zinazotuhusu na kusaidiana na Taasisi nyengine katika maandalizi na marekebisho ya Sera zao – mfano Sera ya Mazingira n.k. Aidha Idara imetayarisha Mpango Mkakati wa Wizara na wa Programme ya *HIV/AIDs*. Sambamba na hayo, Idara imesimamia mipango ya wizara, pamoja na kuratibu shughuli zote za miradi ya maendeleo ya jamii ya Taasisi zake na kutayarisha taarifa kadhaa zikiwemo za utekelezaji wa miezi mitatu, miezi sita na za mwaka za Wizara pamoja na utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2005/2010 na kupelekwa kunakohusika kwa hatua zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2010/2011, idara inaazimia kutekeleza mambo 8 yaliopo hapo chini.

1. Kusimamia maadili mazuri ya wafanyakazi.
2. Kuweka mazingira mazuri ya kazi kwa:-
    - Kuwaendeleza wafanyakazi kielimu;
    - Kutafuta vifaa vya kisasa vya kazi; na
    - Kufanya matengenezo madogo madogo ya jengo na vyombo vya usafiri.
3. Kusimamia hatua za awali za upatikanaji wa jengo kwa ajili ya Ofisi mpya ya Wizara.
4. Kusimamia uandaaji wa taarifa za Wizara.
5. Kuratibu uandaaji na utekelezaji wa Sera ya Wizara, Mipango na Miradi.
6. Kuratibu na kusimamia Maadhimisho ya Sherehe za Kitaifa.
7. Kuratibu Uandaaji na utekeleza wa Sera za Wizara, Mipango na Miradi.
8. Kusimamia utekelezaji wa mchakato wa mageuzi ya Serikali za Mitaa.

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Mipango na Sera ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, kwa mwaka 2010/2011 naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe matumizi ya Tsh. 1,177,421,000/= kwa kazi za kawaida.

AFISI KUU PEMBA

Mhe. Mwenyekiti, Afisi kuu Pemba kwa mwaka wa fedha 2009/2010 ilifanikiwa vyema katika utekelezaji wa shughuli zake za kila siku kutokana

na ushirikiano madhubuti uliokuwepo kati yake na Afisi za Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa miwili (2) ya Pemba, Afisi za Wakuu wa Wilaya nne (4), Serikali saba za mitaa, Afisi ya Usajili na Utoaji Kadi za Vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi, pamoja na Vikosi vitano (5) vya SMZ.

Mhe. Mwenyekiti, Afisi Kuu Pemba kwa mwaka wa fedha 2009/2010 iliidhinishiwa Tsh. 145,456,000/= na hadi kufikia mwezi wa Mei afisi imepokea Tsh. 135,748,571/= Sawa na asilimia 93 kama inavyoonekana kwenye kiambatanisho namba 1.

Mhe. Mwenyekiti, Afisi Kuu Pemba, kwa mwaka wa fedha 2009/2010 ilifanikiwa kutekeleza malengo yake iliojipangia kama inavyoonekana kwenye kiambatanisho namba 3.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011, Afisi Kuu Pemba imedhamiria kutekeleza mambo yafuatayo yanayosomeka hapo chini, namba 1 hadi 5.

1 Kuratibu na kusimamia uandaaji wa taarifa za utekelezaji za robo, nusu na za mwaka mmoja za Ofisi.

2 Kujenga uwezo wa wafanyakazi kwa kuwapatia mafunzo ya kozi fupi na ndefu .

3 Kuijengea uwezo Wizara kwa ununuzi wa vitendea kazi na vyombo vya usafiri.

4 Kulifanyia matengenezo madogo madogo jengo la Ofisi Kuu.

5 Kukutana na Wakuu wa Vitengo na Taasisi mbali mbali kwa lengo la kuzungumzia ufanisi wa Wizara na Maendeleo ya wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, Afisi Kuu Pemba ili iweze kumudu utekelezaji wa majukumu yake iliojipangia kwa mwaka wa fedha 2010/2011, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe matumizi ya Tsh. 185,349,000/= kwa kazi za kawaida.

AFISI YA USAJILI NA KADI ZA UTAMBULISHO

Mhe. Mwenyekiti, Afisi ya Usajili na Kadi za Utambulisho imeanzishwa rasmi mwaka 2005 kwa Sheria namba 7 ya 2005. Afisi hii ina wajibu wa kuwasajili na kuwapatia Vitambulisho Wazanzibari wakaazi waliofikia umri wa miaka 18

na kuendelea na inao wajibu wa kutunza taarifa zote za wananchi zilizokusanywa kwa ajili hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka 2009/2010, Afisi ya Usajili na Kadi za Utambulisho iliidhinishiwa matumizi ya Tsh. Bilioni 1.2. Kati ya hizo Tsh. 371,580,000/= kwa kazi za kawaida na Tsh. 800,000,000/= kwa kazi za maendeleo. Hadi kufikia mwezi wa Mei, idara imepokea Tsh. 1,111,163,633 sawa na asilimia 95, ambazo Tsh. 311,163,633 sawa na asilimia 84 kwa kazi za kawaida na 800,000,000 (100%) kwa kazi za maendeleo. (Kiambatanisho namba 1 kinafafanua).

Mhe. Mwenyekiti, Afisi ya Usajili na Kadi za Utambulisho katika kipindi cha mwaka 2009/2010 ililenga kufanya mambo makuu 7 kama yanavyoonekana hapo chini.

1. Kuendelea kuwasajili wazanzibari wanaotimiza masharti ya usajili.
2. Kutengeneza vitambulisho vipya kwa ajili ya kubadilisha vitambulisho vilivyomaliza muda wake wa matumizi.
3. Kutekeleza agizo la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar juu ya uanzishwaji wa mtandao wa kompyuta wa SMZ (*Zanzibar E-government*).
4. Kutoa elimu kwa jamii juu ya matumizi bora na sahihi ya vitambulisho vya Mzanzibari kama ambavyo sera inavyoelekeza.
5. Kutoa vitambulisho maalum kwa wageni wanaoishi nchini kwa ruhusa maalum (*Residence Permit*) na kutunza taarifa zilizokusanywa kwa ajili hiyo katika database ya Serikali.
6. Kuendelea kutengeneza vitambulisho vya wafanyakazi wa SMZ na Taasisi zake.
7. Kuwajengea uwezo wa kielimu watendaji wa Afisi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu wa makisio hadi kufikia mwaka 2010 jumla ya watu laki tano sabini na tatu elfu mia mbili na ishirini na tano (573,225) walitarajiwa kusajiliwa kwa Zanzibar nzima. Hii ni kutokana na makisio ya idadi ya watu wa Zanzibar hadi kufikia mwaka 2010 itakuwa Milioni moja na laki mbili na sabini na tatu elfu mia nane na thelathini na nne (1,273,834). Hadi kufikia tarehe 30/04/2010 jumla ya wazanzibari wakaazi laki tano na sitini elfu, mia tano na themanini na tano (560,585) wamesajiliwa. Idadi hiyo ni sawa na asilimia tisini na nane (98%) ya watu waliotarajiwa kusajiliwa.

Mhe. Mwenyekiti, kazi inayoendelea hivi sasa katika Afisi Kuu ya Vitambulisho
ni kama inavyojieleza hapo chini:-

- Uingizaji wa taarifa za ziada za wananchi katika Database;
- Uchunguzi wa taarifa za waombaji zenye mashaka;
- Kufanya mabadiliko halali ya taarifa zao kwa wale wanaoomba;
- Utengenezaji wa vitambulisho vipya ili kubadili vitambulisho vilivyomaliza muda wake wa matumizi na kutengeneza vitambulisho vya watu wanaoendelea kusajiliwa na Afisi za Wilaya;
- Kuendelea na usajili wa wananchi wanaotimiza masharti ya usajili na ugawaji wa vitambulisho kwa wananchi; na
- Kutengeneza vitambulisho vya wafanyakazi wa SMZ na Taasisi zake.

Mhe. Mwenyekiti, utekelezaji wa lengo la kutengeneza vitambulisho vipya kwa ajili ya kubadilisha vitambulisho vilivyomaliza muda wake wa matumizi imeanza toka mwezi wa Machi mwaka huu 2010. Mpaka kufikia tarehe 30/04/2010 afisi imeshatengeza vitambulisho vyote vinavyoisha muda wake tarehe 31/05/2010. Afisi inaendelea na utaratibu wa kuvigawa kwa wananchi na kazi hii itakuwa inafanyika kila mwezi hadi mwezi wa 10 mwaka 2010 kutegemea na kadi zinavyomaliza muda wake.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa utekelezaji wa lengo la kuanzisha mtandao wa computer wa SMZ (*e-government*) utakaoziwezesha Wizara na Idara za SMZ kutumia chanzo kimoja cha taarifa kwa lengo la kuengeza usalama na ufanisi katika kutekeleza kazi za Serikali unaendelea. Afisi inashirikiana kwa karibu na Wizara ya Fedha na Uchumi katika kutekeleza lengo hili la muda mrefu, na hivi sasa taratibu zote za kitaalamu zimeshakamilika na agizo la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar limeshatolewa ili kazi ianze. Serikali imeomba mkopo wenye masharti nafuu kutoka Benki ya Exim ya China na kazi itaanza mara tu baada ya fedha hizo kupatikana.

Mhe. Mwenyekiti, katika kufanikisha utekelezaji wa lengo la kutoa elimu kwa jamii juu ya matumizi bora na sahihi ya vitambulisho vya Mzanzibari kama ambavyo sera inavyoelekeza, afisi inaendelea kutoa kipindi maalumu cha redio ambacho kinasikika hewani katika Sauti ya Tanzania Zanzibar mara moja kwa wiki, pia maafisa wa Afisi akiwemo Mkurugenzi wamekuwa wakishiriki mara kwa mara katika vipindi mbali mbali vya uelimishaji na mijadala inayohusu Vitambulisho.

Mhe. Mwenyekiti, katika suala la utoaji wa vitambulisho maalum kwa wageni *(Temporary Resident Cards)* wanaoishi nchini kwa ruhusa maalum *(Residence Permit)* afisi imeshakamilisha taratibu zote za urekebishaji wa sheria ya usajili nambari 7 ya mwaka 2005. Sasa rasimu hiyo inasubiri kupata Baraka za Makatibu Wakuu ili iwasilishwe Baraza la Mapinduzi (BLM) na hatimae iwasilishwe katika Baraza la Wawakilishi. Taratibu nyengine zote za kiteundaji

ikiwa ni pamoja na mfumo wa utengenezaji wa vitambulisho hivyo na matayarisho ya fomu za maombi ya usajili zimekamilika.

Mhe. Mwenyekiti, lengo la kuwajengea uwezo wa kielimu watendaji wa afisi, idara imeweza kuwasomesha wafanyakazi wake kama inavyoonesha kiambatisho namba 4.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na utekelezaji wa malengo hayo, afisi pia imefanikisha mambo yafuatayo:-

Afisi imefanyiwa ukaguzi na wakaguzi wa kimataifa kwa mara ya nne juu ya Muundo, mfumo na taratibu zake za utendaji na imethibitishwa kuwa imeweza kukubaliana na viwango vyote vya kimataifa. Hivyo afisi imetunukiwa vyeti vinne (4) vya kimataifa kwa mara ya nne na kuonesha kuwa imeweza kupiga hatua zaidi kimataifa. Vyeti viwili vya *ISO* 27001 kwa ajili ya viwango vya kiusalama (*information Security Management*) na viwili vya ISO 9001 kwa ajili ya viwango vya ubora (*Quality Management System*). Vyeti hivyo vimetolewa tena kwa pamoja na kampuni ya viwango vya kimataifa *IQnet* na Taasisi ya viwango ya Israel *The Standards Institute of Israel*.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011 afisi inalenga kutekeleza yafuatayo kama inavyojileza namba 1 hadi 7.

1. Kuendelea kuwasajili wazanzibari wanaotimiza masharti ya usajili na kuwapatia Vitambulisho.
2. Kuendelea kutengeneza na kuvigawa vitambulisho vipya kwa ajili ya kubadilisha vitambulisho vilivyomaliza muda wake wa matumizi mwaka huu.
3. Kuanza kutekeleza agizo la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar juu ya uanzishwaji wa mtandao wa computer wa SMZ (*Zanzibar E-government*).
4. Kuendelea kutoa elimu kwa jamii juu ya matumizi bora na sahihi ya vitambulisho vya Mzanzibari kama ambavyo sera inavyoelekeza.
5. Kuanza kutoa vitambulisho maalum kwa wageni wanaoishi nchini kwa ruhusa maalum (*Residence Permit*) na kutunza taarifa zilizokusanywa kwa ajili hiyo katika database ya Serikali.
6. Kuendelea kutengeneza vitambulisho vya wafanyakazi wa SMZ na Taasisi zake.
7. Kuendelea kuwajengea uwezo wa kielimu watendaji wa Afisi.

Mhe. Mwenyekiti, Afisi ya Usajili wa Kadi za Utambulisho ili iweze kufanya kazi zake kwa ufanisi na kufanikisha malengo iliyojipangia katika kipindi cha 2010/2011 naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe matumizi ya Tsh.

910,000,000/= kwa kazi za kawaida na Tsh. 800,000,000/= kwa kazi za maendeleo.

IDARA YA TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa inaendelea kutekeleza Majukumu ya kuongoza, kufuatilia, kuratibu uendeshaji bora wa Serikali za Mitaa pamoja na Mamlaka ya Utawala wa Mikoa kwa mujibu wa sheria namba 1 ya 1998 ya Mamlaka ya Utawala wa Mikoa na sheria namba 3 na 4 za 1995 ya usimamizi wa Serikali za Mitaa. Kwa maana hiyo idara hii inatekeleza shughuli zake katika nyanja kuu mbili:-

1. Tawala za mikoa ambayo inaunganisha nguvu za Mikoa, Wilaya hadi Shehia katika kutoa maelekezo na kusaidia kutatua matatizo yanayokabili jamii katika maeneo yao.

2. Usimamizi wa Serikali za Mitaa ambazo ni Baraza la Manispaa, Mabaraza ya Miji ya Mkoani, Chake Chake na Wete – Pemba, pamoja na Halmashauri tisa za Wilaya za Unguja na Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Tawala za Mikoa katika kipindi cha mwaka 2009/2010 iliidhinishiwa Tsh. 1,473,493,913. Kati ya hizo Tsh. 1,423,493,913 kwa shughuli za kawaida na 50,000,000/= kwa ajili ya kazi za maendeleo. Hadi mwezi huu, idara imepokea Tsh. 1,244,147,407 sawa na asilimia 84 zikiwa Tsh. 1,204,147,407 sawa na asilimia 85 kwa shughuli za kawaida na Tsh. 40,000,000/= sawa na asilimia 80 kwa kazi za maendeleo. Angalia kiambatanisho namba 1.

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha 2009/10, idara ilijipangia kutekeleza mambo tisa (9) na mpaka mwezi huu wa Juni, 2010, idara imefanikiwa kutekeleza mambo 9 yaliopo hapo chini.

1. Kuwajengea uwezo Makatibu wa Halmashauri kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi katika Chuo cha Utumishi wa Umma katika fani za uendeshaji wa Serikali za Mitaa na ujasiriamali na Kuendelea kutoa mafunzo ya muda mfupi yanayohusiana na Sheria na Utawala Bora kwa Waheshimiwa Madiwani na Masheha.

2. Kuhamasisha jamii kwa kutumia mbinu shirikishi katika kuibuwa miradi
   ya maendeleo katika maeneo yao.

3. Kusimamia Kamati ya Ukimwi (*Technical Aids Committee*) ndani ya wizara kwa kutoa elimu ya UKIMWI na kuendesha zoezi la upimaji wa hiari kwa kushirikiana na ANGOZA, ili kujua hali za afya za wafanyakazi.

4. Kushirikiana na ASASI za kiraia ili kutoa huduma kwa jamii na kwa kushirikiana na Mradi wa *MACEMP* Idara imeweza kumuajiri Mshauri Muelekezi kwa ajili ya kupata viwango vya elimu vinavyohitajika katika Mikoa na Serikali za Mitaa kwa wafanyakazi, kuelekea kwenye Mfumo wa Marekebisho ya Serikali za Mitaa.

5. Kufuatilia na kufanya tathmini kwa shughuli za maendeleo ya jamii kwa Serikali za Wilaya na Serikali za Mitaa.

6. Kujenga na kuimarisha uhusiano wa kitaasisi kwa ajili ya ustawi wa maendeleo ya wananchi kuanzia Wilaya hadi Shehia za Miji na Vijijini.

7. Vikao viwili vilifanyika baina ya TAMISEMI na Tawala za Mikoa Zanzibar kwa ajili ya kukuza uhusiano mwema wa watendaji wa Idara ya Tawala za Mikoa na watendaji wa TAMISEMI**.**

8. Kushirikiana na Wilaya kwa kuwatumia Maafisa wa Sekta katika ngazi za Wilaya kuweza kuwasaidia wananchi kuendelea kutekeleza miradi yao mbali mbali ya maendeleo katika Shehia zao, ikiwemo miradi ya *PADEP***,** *ASSP/ASDPL, TASAF, MACEMP,* nk.

9. Idara ilishirikiana na Taasisi ya *TRA* na kuwapatia mafunzo ya umuhimu wa ulipaji kodi watendaji wake wakiwemo Waheshimiwa Masheha na Madiwani wa Wilaya ya Mjini na Wilaya ya Kati. Vile vile walikumbushiwa juu ya Sheria No.3 ya Baraza la Manispaa na Sheria No.4 ya Mabaraza ya Miji na Halmashauri za Wilaya za mwaka 1995. Aidha wafanyakazi wawili (2) hadi hivi sasa wanaendelea na mafunzo ya muda mrefu ya Sheria katika ngazi ya Shahada ya pili mmoja ndani ya nchi na wapili nje ya Nchi. Pia Idara imeweza kununua Vespa moja kwa ajili ya ufuatiliaji wa kazi za Idara.

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha 2010/2011**,** idara inatarajia kutekeleza mambo yafuatayo yanayojieleza kuanzia namba 1 hadi 9.

1. Kuendelea kuwapatia mafunzo Maafisa wa Idara kuhusiana na uendeshwaji wa muundo wa Serikali za Mitaa ndani na nje ya nchi.
2. Kuendelea kuwajengea uwezo Masheha na Madiwani kwa kuwapatia taaluma ya Sheria na Utawala kwa njia ya semina na mikutano.
3. Kuwapatia taaluma watendaji kuhusiana na kuhamasisha jamii katika kubuni miradi (*Project Design*).
4. Kuendelea kuhamasisha wafanyakazi kujiepusha na maambukizo mapya ya Ukimwi na unyanyapaa.
5. Kuendelea kuwashajiisha na kuwapa taaluma ya maendeleo ya jamii na jinsia watendaji wa Wizara, Mikoa, Wilaya na Shehia za Unguja na Pemba.
6. Kuendelea kushirikiana na asasi za kiraia kwa ajili ya kutoa elimu na huduma nyenginezo katika jamii.
7. Kuendelea kufanya tathmini kwa shughuli za maendeleo ya jamii, na Serikali za Mitaa pamoja na Serikali za Wilaya.
8. Kuendelea kuimarisha uhusiano wa Taasisi mbali mbali za Serikali ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa ajili ya kukuza maendeleo ya jamii.
9. Kuendelea na utekelezaji wa maazimio ya Makatibu Wakuu kuhusiana na utayarishaji wa Sera ya Madaraka kwa wananchi na Mpango wa marekebisho ya Serikali za Mitaa.

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Tawala za Mikoa iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi katika mwaka 2010/2011, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe matumizi ya Tsh. 1,505,203,000/= kwa kazi za kawaida na Tsh. 250,000,000/= kwa kazi za maendeleo.

UTEKELEZAJI KATIKA MIKOA

Mhe. Mwenyekiti, sambamba na kusimamia na kuratibu majukumu yake, Idara ya Tawala za Mikoa, pia kiutekelezaji inasimamia na kuratibu utekelezaji wa malengo ya Ofisi za Mikoa pamoja na Serikali za Mitaa Unguja na Pemba. Kwa mwaka 2009/2010 Ofisi za Mikoa zilijipangia kuratibu, kusimamia na kutathmini shughuli mbali mbali za maendeleo pamoja na kuwashajiisha wananchi kulima mazao ya kilimo, misitu na biashara ili kujinasua na umasikini na kuimarisha uchumi. Aidha, Mikoa iliwajibika kuimarisha na kulinda amani, utulivu, umoja na mshikamano wa wananchi pamoja na Ulinzi na Usalama wa Raia na mali zao.

Mhe. Mwenyekiti, ili kutekeleza majukumu yao, Mikoa iliidhinishiwa Tsh. 3,576,850,000/= na hadi mwezi huu, Mikoa ilipatiwa Tsh. 2,833,642,998 sawa na asilimia 79 kama kiambatanisho namba 1 kinavyochambua.

Mhe. Mwenyekiti, mnasaba na mapato hayo, katika mwaka 2009/2010, Mikoa ilitekeleza majukumu yao ya kilimo kama inavyoonekana kwenye kiambatanisho namba 5 (a) kwa Mikoa ya Unguja na kiambatanisho namba 5 (b) kwa Mikoa ya Pemba. Aidha, kwa upande wa majukumu yasiyo ya kilimo, Mikoa ilifanikiwa kutekeleza kama ifuatavyo:-

MKOA WA MJINI MAGHARIBI – UNGUJA

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2009/2010 Mkoa umeratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli za usalama pamoja na utatuzi wa masuala/matatizo mbali mbali ya wananchi katika Mkoa huu. Mbali na hayo Mkoa wa Mjini Magharibi ulitekeleza malengo yake uliojipangia kama yanavyoonekana kwenye kiambatanisho namba 6 (a).

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2010/2011Mkoa wa Mjini Magharibi umejipangia kutekeleza malengo manne (4) kama unavyosomeka kwenye namba 1 hadi namba 4.

1. a) Kulima ekari :-
   - 1,500 za mpunga wa kutegemea mvua.
   - 4,000 za vipando mbali mbali vya mazao kama muhogo, migomba, viazi n.k

   b) Kulima na kuvuna tani 200 za mwani.
   c) Kutoa mafunzo kwa :-
      - Wavuvi 250 kuhusu utumiaji wa zana za kisasa.
      - Wafugaji 80 wa ng'ombe na mbuzi.
      - Wafugaji 200 wa kuku wa kienyeji na wa kisasa.

   d) Kuatika miche:-
      - 75,000 ya mikarafu
      - 100,000 ya misitu.
      - 75,000 ya mazao ya matunda na biashara.

2. Kutoa mafunzo kwa:-
   - Wafanyakazi 10 wa fani mbali mbali.
   - Kamati za Maendeleo za Shehia.
   - Kamati za Afya za Shehia.

3. Kuratibu shughuli za UKIMWI.

4. Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa miradi mbali mbali ya maendeleo kama kiambatanisho namba 6 (b) kinavyosomeka. Aidha, Mkoa utasimamia Ujenzi wa Afisi ya Mkuu wa Mkoa – Amani (**Tsh. 521,979,700/=**); Wilaya ya Mjini – Amani (Tsh. 161,000,000/=) na Wilaya ya Magharibi – Mwera (Tsh. 150,000,000/=).

Mhe. Mwenyekiti, Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja ili uweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi katika kipindi cha mwaka 2010/2011, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe matumizi ya Tsh. 661,000,000/= kwa matumizi ya kazi za kawaida.

MKOA WA KASKAZINI – UNGUJA

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2009/2010, Baraza lako tukufu liliidhinisha matumizi ya Tsh. 580,000,000/= kwa kazi za kawaida na Tsh. 115,000,000/= kwa kazi za maendeleo. Hadi mwezi huu, Mkoa umepatiwa Tsh. 480,987,720/= sawa na asilimia 83 kwa kazi za maendeleo na Tsh. 115,000,000 (100%) kwa kazi za maendeleo. Angalia kiambatanisho namba 1.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2009/2010 Mkoa ulijipangia na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

Kuhamasisha na kusimamia kilimo cha mpunga, kilimo cha juu, kilimo cha maweni na uwatikaji wa miche ya misitu na matunda kwa malengo tofauti, kama unavyoonekana kwenye kiambatanisho namba 5 (a).

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa miradi ya maendeleo ya wananchi, katika mwaka 2009/2010 Mkoa wa Kaskazini Unguja ulikusudia kuwashajihisha wananchi na kusimamia, miradi 17 mikongwe na miradi 6 mipya, na kufanya jumla ya miradi 23 inayotekelezwa na wananchi, kwa kushirikiana na viongozi wa Mkoa, Wilaya, Majimbo na Wahisani. Kati ya miradi hiyo 23, miradi (10 mikongwe) ndio iliyotekelezwa na kukamilika. Miradi (7) mikongwe na miradi (6) mipya haikukamilika kutokana na upungufu wa rasilimali fedha (*financial resources).*

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2009/2010, Mkoa ulipanga kutekeleza jumla ya miradi yake minne (4). Kati ya miradi hiyo Baraza lako tukufu liliidhinisha fedha Tsh. 115,000,000/= na kupatiwa Tsh. 90,000,000/= kwa mradi mmoja wa Ujenzi wa Afisi ya Mkuu wa Mkoa. Aidha, wahisani walichangia Tsh. 8,570,000/= na kukamilisha jengo kwa kuezekwa na kupigwa

plasta. Miradi mitatu (3) iliyobakia ya Ujenzi wa Afisi ya Mkuu wa Wilaya ya Kaskazini "A", Ujenzi wa Afisi ya Mkuu wa Wilaya ya Kaskazini "B" na matengenezo ya nyumba ya Mkuu wa Mkoa haikuidhinishiwa fedha.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2010/2011 Mkoa wa Kaskazini Unguja unakusudia kusimamia na kutekeleza shughuli zake kama inavyoonekana katika namba 1 na 2.

1) Kilimo cha mpunga, kilimo cha juu, kilimo cha maweni, na uatikaji wa miche ya matunda na misitu kwa kulima mpunga wa kutegemea mvua eneo liliopo ni eka 9,731 lengo ni kulima eka 6,893 sawa na asilimia 70.83; kulima kilimo cha maweni eneo liliopo ni eka 34,600 lengo ni kulima eka 12,654 sawa na asilimia 36.57; kulima kilimo cha juu mzao mbali mbali eneo liliopo ni eka 42,432 lengo kulima eka 18,221 sawa nja asilimia 43 na uatikaji wa miche ya matunda na misitu miche 50,279.

2) Kuwashajiisha wananchi kumaliza miradi yao 13 ya maendeleo kama inavyoonekana kwenye kiambatanisho namba 7 (a na b) pamoja na kutekeleza miradi yake ya maendeleo minne (4) ambayo mitatu (3) haikutekelezwa mwaka 2009/2010 na mradi mmoja umetekelezwa na unaendelezwa kama ilivyoelezwa katika ibara ya (51**).**

Mhe. Mwenyekiti, Mkoa wa Kaskazini Unguja ili uweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi katika kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011 naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe matumizi ya Tsh. 616,000,000/= kwa matumizi ya kawaida na Tsh. 150,000,000/= kwa matumizi ya kazi za maendeleo.

MKOA WA KUSINI – UNGUJA

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka 2009/2010, Mkoa uliidhinishiwa Tsh. 656,000,000/= kwa kazi za kawaida na Tsh. 60,000,000/= kwa kazi za maendeleo na hadi mwezi huu, Mkoa umeingiziwa Tsh. 517,833,100 sawa na asilimia 79 kwa kazi za kawaida na Tsh. 60,000,000 (100%) kwa kazi za maendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, mbali na shughuli za kila siku za utendaji Mkoa wa Kusini Unguja, katika kipindi cha 2009/2010 Mkoa ulijipangia kutekeleza shughuli za Kilimo kama inavyoonekana kwenye nambari 1 mpaka 7.

1. Kulima ekari 2,000 za mpunga wa kutegemea mvua
2. Kulima ekari 120 za mpunga wa kumwagilia maji
3. Kulima ekari 5,770 za mazao mchanganyiko
4. Kupanda miti ya matunda miche 16,260

5. Kupanda miti ya misitu
    - Mivinje 30,000
    - Mikeshia miche 30,000
    - Mitondoo miche 30,000
    - Misaji miche 5,500
6. Kupanda miche ya viungo
    - Pilipili Manga miche 600
    - Manjano, michaichai na midalasini miche 900.
7. Mikarafuu miche 4350

Aidha, Mkoa kwa kipindi hicho, umemudu kusimamia na kuratibu utekelezaji wa malengo hayo ya kilimo kama inavyoonekana kwenye kiambatanisho namba 5 (a).

Mhe. Mwenyekiti, sambamba na hayo, Mkoa wa Kusini Unguja katika kipindi cha fedha cha mwaka 2009/2010 ulilenga kuratibu, kusimamia na kusaidia kutekeleza jumla ya miradi kumi (10) ya maendeleo ya wananchi ambayo haikukamilika kutokana na kutopatiwa fedha kama inavyoonekana kwenye kiambatanisho namba 8.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwasaidia wananchi kuwapunguzia matatizo ya miundo mbinu ya usafiri kwa barabara za ndani, Mkoa kwa kushirikiana na Idara ya Barabara – Zanzibar na wananchi wenyewe, umezifanyia matengenezo barabara ndogo 3 kwa kiwango cha kutia fusi na kuziba mashimo kama inavyoonekana hapo chini.

1. Barabara ya Miwani, Ukongoroni na Charawe.
2. Cheju – Unguja Ukuu:- kazi ya kutia mawe na kuziba mashimo makubwa zimefanywa na Askari wa JKU kwa kushirikiana na wakulima wa bonde la Cheju na barabara ya Koani/Jumbi kazi ya kutiwa kifusi kutoka Koani hadi Pongwe (5km) zimefanywa na Kampuni ya ujenzi wa barabara *MECCO* kwa shughuli zao za uchukuaji wa kifusi kutoka Pongwe.
3. Ndijani Nyambiza / Ndijani Mseweni (barabara kuu mfuuni) na barabara ya Hanyegwa Mchana / Cheju Vijijini – kazi za kuwekwa sawa (Grading na kutiwa kifusi) hazikufanyika.

Mhe. Mwenyekiti, mbali na miradi hiyo ya wananchi, Mkoa wa Kusini Unguja kwa mwaka wa fedha 2009/2010 umemudu kutekeleza mradi wake wa Ujenzi wa Afisi mpya ya Mkuu wa Mkoa – Tunguu kwa kujenga ukuta wa kuzingiza jengo na kuchongesha madirisha, fremu za milango, utiaji wa plasta nje, utiaji wa chanja za dari, utiaji wa paipu za umeme na uchimbaji wa makaro.

Mhe. Mwenyekiti, Mkoa wa Kusini Unguja, kwa mwaka wa fedha 2010/2011 umelenga kuratibu kuhamasisha na kusimamia kutekeleza shughuli zifuatazo kama inavyojieleza namba 1 hadi 5 ya kilimo na miradi ya ujenzi namba 1 hadi 4:-

A. KILIMO:

1. Kulima mpunga wa kutegemea mvua ekari 2,000
2. Kulima mpunga wa kumwagilia maji ekari 613
3. Ukulima wa mazao mchanganyiko ekari 15,450
4. Ukulima wa mazao ya matunda miche 18,459
5. Upandaji wa zao la karafuu miche 4,650

B. MRADI WA UJENZI:

Kukamilisha mradi wa ujenzi wa Afisi ya Mkuu wa Mkoa Tunguu kwa:

1) Kutia palasta sakafu na tiles
2) Kukamilisha kutia madirisha na milango
3) Kutia umeme na mifereji
4) Kutia dari na rangi

Mhe. Mwenyekiti, Mkoa wa Kusini Ungua ili uweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi katika kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe matumizi ya Tsh. 657,000,000/= kwa kazi za kawaida na Tsh. 60,000,000/= kwa kazi za maendeleo.

MKOA WA KASKAZINI – PEMBA

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha fedha 2009/2010 Baraza lako tukufu liliuidhinishia Mkoa wa Kaskazini Pemba kutumia Tsh. 734,300,000 kazi za kawaida. Hadi mwezi wa Mei, Mkoa umeingiziwa Tsh. 585,991,168 sawa na asilimia 80 – kama inavyoonekana katika kiambatanisho namba 1.

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha fedha cha 2009/2010 Mkoa wa Kaskazini Pemba ulijipangia kutekeleza kama inavyoonekana kwenye namba 1 hadi 9.

1. Kulima na kuatika:-
   Kulima Vipando vya mazao ya juu Ekari 31047
   Kuatika Miche ya Misitu 39,789 na kuigawa kwa Wananchi
   Kuatika Miche ya Viungo 11,615
   Kuatika Miche ya Minazi 2518.
   Kuatika Miche ya Mikarafuu 39,789
   Kuatika Miche ya Matunda 12,696

1. Kusimamia Maendeleo ya Elimu na kuinua kiwango cha ubora.

2. Kusimamia na kuendelea kufatilia kuwaelimisha Wananchi athari za Madawa ya kulevya, Malaria, Maambukizo ya Virusi vya Ukimwi.

3. Kushirikiana na Wizara husika kusimamia upatikanaji wa huduma muhimu, Maji na Umeme kwa Vijiji vya Makongeni, Kivumoni, Machengwe, Mitambuuni, Kinazini na Mkanjuni kwa Wilaya ya Wete, Maziwang'ombe, Mjini Wingwi, Kiuyu Mbuyuni na Bule kwa Wilaya ya Micheweni.

4. Kushirikiana na Wizara husika kusimamia upatikanaji wa huduma muhimu, Maji na Umeme kwa Vijiji vya Makongeni, Kivumoni, Machengwe, Mitambuuni, Kinazini na Mkanjuni kwa Wilaya ya Wete, Maziwang'ombe, Mjini Wingwi, Kiuyu Mbuyuni na Bule kwa Wilaya ya Micheweni.

5. Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Miradi mbali mbali inayoendelea ikamilike.

6. Kuwashajiisha wakulima wa mwani na kusimamia utoaji wa fedha kwa Vikundi vya Ushirika wa SACCOS, Makampuni ya Ujasiri amali ili kupambana na umasikini na kujiimarisha Kiuchumi.

Aidha, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2009/2010 Mkoa kwa kushirikiana na wizara husika pamoja na nguvu za Wananchi, ulitekeleza malengo iliyojipangia kama viambatanisho namba 5 (b), 9 (a), 9 (b) na 9 (c) vinavyoonyesha.

Mhe. Mwenyekiti, mbali na malengo yaliyopangwa kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2009/2010, Mkoa pia umefanikiwa kutekeleza Miradi 3 inayoonekana kuanzia namba 1 hadi 3:-

1. Ujenzi wa banda la madarasa 4 Skuli ya Mkote Shehia ya Ukunjwi iliyojengwa kwa msaada wa Shirika la Action Aid, nguvu za wananchi na michango ya Mheshimiwa Mbunge na Mwakilishi wa Jimbo la Gando. Jengo hilo limegharimu jumla ya Tsh. 28,520,000/=.

2. Ujenzi wa Skuli mpya ya Mjini Kiuyu – Shehia ya Kiuyu Minungwini, ujenzi huu umekamilika kwa msaada mkubwa

wa Shirika la Action Aid, mchango wa Mheshimiwa Mbunge na Mwakilishi wa Jimbo la Ole, Halmashauri ya Wilaya ya wete, Alite Club, Kambuni ya Mwani ya Zan Que na Zanea, nguvu za Wananchi na hatimae Wizara ya Elimu ilimalizia. Hadi kumalizika kwake jumla ya Tsh. 37,600,000/= zimetumika.

3. Katika kuwakwamua wananchi kutokana na umasikini Wajasiriamali wamepatiwa mafunzo na kujengewa uwezo wa kibiashara kwa juhudi kubwa za Viongozi mbali mbali wa Chama na Serikali. Jumla ya Wajasiriamali 31 wa Mkoa huu baada ya kupatiwa mafunzo wamekabidhiwa jumla ya Tsh. 37,203 kutoka kwenye Kampuni ya FANIKIWA KIBIASHARA.

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2009/2010 jumla ya miradi 7 ya ufugaji wa kuku wa mayai iliyogharimu Tsh. 43,123, 235/= imesidiwa fedha kutoka Mfuko wa Jamii *TASAF*. Miradi hiyo ni kwa ajili ya watu wenye mahitaji maalum kama vile walemavu, wajane na mayatima. Vile vile ili kuwawezesha wananchi kiuchumi, kupitia Mfuko wa Mhe. JK na AK hadi kufikia mwezi Machi, 2010 jumla ya wananchi 61 wameshapata mikopo yenye thamani ya Tsh. 123,470,000/= kwa machanganuo ufuatao:-

1. Wilaya ya Wete	Wananchi 32	Tsh. 82,170,000/=
2. Wilaya ya Micheweni	Wananchi 29	Tsh. 41,300,000/=
	Wananchi 61	Tsh. 123,470,000/=

Mhe. Mwenyekiti, Mkoa kwa kushirikiana na Taasisi zote za Serikali uliweza kusimamia miradi yote ya maendeleo ya wananchi kisekta.

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011 Mkoa wa Kaskazini Pemba umekusudia kuratibu, kushajiisha, kusimamia na kutekeleza malengo kama inavyosomeka hapo
chini kuanzia namba 1 hadi 6.

1. Kusimamia Umoja na Mshikamano, Amani, Ulinzi na Usalama wa raia na Mali zao chini ya Chombo cha Kamati ya Ulinzi na Usalama cha Mkoa.

2. Kulima mpunga wa kutegemea Mvua Ekari 8500 katika Maeneo ya Bonde la Bandani, Dodeani, Mapungwi, Mzoite, Chwale, Kiungweni, Koowe, Ukele, Kanambe, Wapape, Chanjaani nk.

- Kulima Mpunga wa Umwagiliaji Maji Hecta 70;
- Katika Mabonde ya Mangwena, Weni, Tungamaa, Saninga, Kinyakuzi nk.;
- Kulima Vipando vyajuu Ekari 31047 katika Maeneo ya, Junguni, Gando, Ukunjwi;
Mtambwe, Kisiwani, Makangale, Konde, Kifundi, Mgogoni, Finya, nk.;
- Kuatika Miche ya Matunda 68,250 katika Vitalu vya Weni, Piki, Ole, Konde Kicha, Mapofu nk.;
- Kuatika Miche ya minazi 10,000 katika Vitalu vya Tumbe , Ole na Piki;
- Kuatika Miche ya Mikarafuu 90,000 katika Vitalu vya Weni, Kicha, Piki na Mapofu;
- Kuatika Miche ya Viungo 5,700 Katika vitalu vya Weni, Ole, Kicha na Mapofu; na
- Kuatika Miche ya Misitu 316,950 katika vitalu vya Konde, Ole nk.

3. Kushirikiana na Serikali kuu, Wizara husika na Kamati zinazosimamia Maendeleo ya Elimu, Afya, Kilimo, Maafa, nk. ili kuona kwamba huduma muhimu zinapatikana katika Mkoa.

4. Kusimamia Miradi ya Maendeleo kwa kushirikiana na Wizara zinazohusika ikiwemo miradi ya barabara inayofadhiliwa na *MCC* na *BADEA*.

5. Kuendelea kushirikiana na Taasisi zinazohusika ili kuwaelimisha Wananchi hasa Vijana wa rika na jinsia zote. Athari za maambukizi mapya ya Virusi vya Ukimwi, Madawa ya Kulevya na Malaria.

6. Kushirikiana na *NGOs* mbali mbali katika kutumia Rasilimali zilizomo ndani ya Mkoa kama vile Ardhi, Bahari, Misitu nk. ili kuwajengea uwezo Wajasiriamali wa Mkoa wetu kwa dhamira ya kupambana na umasikini.

Mhe. Mwenyekiti, Mkoa wetu wa Kaskazini Pemba ili uweze kumudu kutekeleza malengo yake yote uliyojiwekea katika mwaka wa fedha 2010/2011 naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha jumla ya Tshs. 834,000,000/= kwa kazi za kawaida na Tsh. 40,000,000/= kwa kazi za maendeleo.

MKOA WA KUSINI – PEMBA

Mhe. Mwenyekiti, Mkoa wa Kusini Pemba kwa mwaka wa fedha wa 2009/2010 uliidhinishiwa Tsh. 968,550,000/= kwa kazi za kawaida. Hadi sasa Mkoa umepokea Tsh. 726,903,949 sawa na asilimia (75) – kama kiambatanisho namba 1 kinavyoelekeza.

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha fedha cha mwaka 2009/2010 Mkoa wa Kusini Pemba ulijipangia kusimamia na kuona kuwa utekelezaji halisi kwa shughuli za kilimo unakuwa kama ulivyo katika kiambatanisho namba 5 (b).

Mhe. Mwenyekiti, Afisi ya Mkuu wa Mkoa Kusini Pemba kwa kushirikiana na viongozi wa Sekta ya Elimu katika kipindi cha 2009/2010 walijipangia kusimamia maendeleo ya elimu na kuinua kiwango cha ubora kama yanavyojieleza kuanzia namba 1 hadi 8.

1) Kuhakikisha kwamba wanafunzi waliofikia umri wa kwenda shule wanapata nafasi ya masomo.
2) Kuona kwamba wanafunzi hatembei zaidi ya km. 4 kufika Skuli.
3) Kuona kwamba kila Shehia inapatiwa Skuli ya msingi.
4) Kuhamasisha wazazi kuandikisha watoto Skuli.
5) Kuhamasisha wazazi kuchangia gharama za mitihani ya majaribio.
6) Bodi ya elimu Mkoa kufanya ziara na kuzungumza na Kamati za Skuli, wazee ili kuimarisha maendeleo ya elimu.
7) Kufanya ziara kwa kuhamasisha Skuli zilizofanya vibayaziongeze juhudi na kuzipongeza Skuli zilizofanya vizuri.
8) Katika kukuza kiwango cha elimu sekta hii pia iliendeleza kusimamia miradi ya ujenzi wa madarasa kama ilivyo kwenye kiambatanisho namba 10 (a).

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa Sekta ya Maji, Afisi ya Mkuu wa Mkoa Kusini Pemba ilishirikiana na uongozi wa Sekta hii kwa kufuatilia ukamilishaji wa miradi ya maji katika Mkoa na kuhakikisha kwamba idara inahudumia kwa kuvisafisha na kuvifanyia matengenezo madogo madogo ya pampu na visima vilivyopo. Kiambatanisho namba 10 (b) kinafafanua zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, Sekta ya Ujenzi na Matengenezo ya Barabara kwa kushirikiana na Afisi ya Mkuu wa Mkoa Kusini Pemba katika kipindi cha 2009/2010 pia ilishughulikia kazi za miradi ya ujenzi wa barabara kama inavyoonekana kuanzia namba 1 mpaka 7.

1. Mtambile – Muambe (9.3 km) kazi za usafisha, uwekaji wa kifusi cha mwanzo na ujenzi wa culverts zimeanza na zinaendelea.

2. Mtambile - Kangani (6.6 km) kazi za usafishaji zimeanza.
3. Mizingani – Wambaa (9.8 km) ilifanyiwa upimaji wa eneo la barabara (servey).
4. Kenya – Chambani (3.2 km) kazi haijaanza.
5. Tundauwa – Pujini (15.1 km) kazi haijaanza.
6. Sekta hii pia ilianza kazi ya usafishaji wa eneo katika barabara ya Mgagadu – Kiwani ambayo inagharamiwa na SMZ yenyewe.
7. Mbali na kazi za miradi sekta hii iliweza pia kuzifanyia matengenezo madogo madogo barabara ambazo zinahudumiwa ni pamoja na barabara ya Ndagoni, Birikau, Tironi na nyenginezo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa afya, Mkoa umesimamia huduma mbali mbali kwa kushirikiana na Sekta husika yakiwemo ya upigaji dawa majumbani, chanjo na kadhalika.

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2010/2011 Mkoa unajipangia kusimamia majukumu kama yanavyoonekana kuanzia namba 1 mpaka 9.

1. Kulima ekari:-
   a) 7,500 za mpunga;
   b) 13,000 kilimo cha juu.
   c) Miche 164,850 ya miti mbali mbali ya misitu na kuigawa kwa wananchi; na
   d) Miche 90,000 ya mikarafuu na kuigawa kwa wananchi.
2. Kusimamia maendeleo ya elimu na kuinua kiwango kwa wananchi.
3. Kusimamia uimarishaji wa miundo mbinu kama vile nishati na barabara.
4. Kusimamia uenezaji na uimarishaji wa huduma za maji.
5. Kuboresha huduma za afya katika Mikoa.
6. Kusimamia na kufuatilia mikakati ya kupambana na HIV/AIDS.
7. Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa miradi mbali mbali iliyoanzishwa na wananchi.
8. Kusimamia Utawala Bora na hali ya Ulinzi na Usalama wa Mkoa.
9. Kuboresha mazingira ya kazi katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Kusini Pemba, MKuu wa Wilaya ya Chake Chake na Mkoani.

Mhe. Mwenyekiti, Afisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kusini – Pemba ili iweze kutekeleza kazi zake kwa ufanisi zaidi katika mwaka 2010/2011 tunaliomba

Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya Tsh. 1,050,000,000/= kwa kazi za kawaida na Tsh. 60,000,000/= kwa kazi za maendeleo.

UTEKELEZAJI KATIKA SERIKALI ZA MITAA

Mhe. Mwenyekiti, bado Serikali za Mitaa kwa Zanzibar inamaanisha kuwepo kwa Baraza la Manispaa – (Unguja); Mabaraza ya Miji – Pemba na Halmashauri za Wilaya Unguja na Pemba vyombo vinavyowajibika kwa Sheria Namb. 3 na 4 za 1995.

Aidha, vyombo hivi vinasaidiana na Serikali Kuu katika mambo makuu matatu yaliyoorodheshwa hapo chini.

1. Kuweka taswira nzuri na za kupendeza za maeneo yao kwa bustani nzuri, kusafisha Miji; kusomba taka; kushughulikia mitaro ya maji machafu n.k.

2. Kutoa elimu ya afya kwa jamii kujilinda na maradhi ya kuambukiza na miripuko kwa kushirikiana na Taasisi mbali mbali.

3. Kupunguza kero za wananchi kwa kusaidia kugharamia vifaa au fedha katika miradi ya Kiuchumi na Kijamii katikia maeneo yao.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuyatekeleza hayo, Serikali za Mitaa kupitia ruzuku kutoka Serikalini na makusanyo yao kutoka vianzio vyao tofauti vya mapato kwa mwaka 2009/2010 ziliruzukiwa Tsh. 1,787,703,508 na kujipangia kukusanya Tsh. 1,582,035,900/= Hadi mwezi wa Juni Serikali za Mitaa zimepatiwa Ruzuku ya Tsh. 1,434,795,631 sawa na asilimia 85 na kumudu kukusanya Tsh. 1,547,569,834 sawa na asilimia 104. kama kiambatanisho namba 11 kinavyoonyesha.

BARAZA LA MANISPAA

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2009/2010, Manispaa imeendelea na juhudi zake katika kusimamia kazi mbali mbali za kawaida na za Maendeleo ya Mji wetu wa Unguja kwa kusimamia na kutoa huduma za taka, michirizi ya maji machafu na maji ya mvua. Tumeshuhudia harakati za kukarabati taa za njiani za maeneo ya Mji Mkongwe na baadhi ya maeneo ya N'gambo ambayo yalikuwa kiza kwa muda mrefu na sasa taa hizo baadhi zinawaka na hasa maeneo ya Michenzani, vile vile kwa mashirikiano na taasisi mbali mbali za Serikali na watu binafsi hatua ya kuendelea na matengenezo zinaendelea.

Mhe. Mwenyekiti, maeneo yaliokuwa wazi (*open spaces)* kama bustani ya Jamhuri, Bustani maarufu ya Forodhani hivi sasa yanaendelea kuwa sehemu muhimu sana na ya kivutio cha Mji wetu na maeneo makubwa ya kupumzikia.

Mhe. Mwenyekiti, Baraza la Manispaa katika mwaka 2009/2010 lilijipangia na kutekeleza malengo yake kama inavyoonekana kwenye namba 1 hadi 4.

1**.** Ukamilishaji wa maandalizi ya Mpango wa utekelezaji wa Mradi wa Michirizi awamu ya Tatu chini ya ufadhili wa Benki ya Dunia.

Rasimu ya Ripoti ya ubunifu, na bajeti *(Detailed design & Budget)* imekamilika kwa asilimia 100 % kwa ajili ya Ukarabati na ujenzi wa mitaro ya maji ya mvua maeneo yaliobakia ya ngambo imekamilika, na Rasimu ya vitabu vya Zabuni kwa ajili ya kutafuta wakandarasi wa ujenzi ambao unatarajiwa utekelezaji wake mapema mwakani 2011 zimekamilika. Kazi ambayo imetekelezwa kwa mashirikiano ya Manispaa, Kampuni ya H.P Gauff Ingenieure – JBG ya Ujerumani na sasa tunaendelea na utaratibu wa kuthibitishwa kwa ajili ya kupata baraka kutoka kwa wafadhili wa mradi huu yaani Benki ya Dunia na Kiasi cha fedha ni sawa na USD 10,000,000 zimetengwa kwa ukarabati na ujenzi wa mitaro katika maeneo ya Mpendae hadi Shule ya Jang'ombe; Ujenzi wa mtaro wa Migombani hadi Kilimani; mtaro wa Ziwa la Mtumwajeni hadi Sebleni, Sebleni hadi Lumumba, Shaurimoyo, Karakana, Magomeni, Ziwa la Binti Amrani Mpendae, Mnazi mmoja, Sogea n.k. sawa na urefu wa jumla kilomita 27.

2. Ripoti ya mwisho ya mpango wa taka wa maeneo ya ngambo imekamilika kwa asilimia 100% na vile vile vitabu vya Zabuni vimekamilika na tayari vimethibitishwa na Benki ya Dunia. Fedha zote zilizotengwa kwa ajili ya uimarishaji huduma za taka maeneo ya Ngambo yasiokuwa na majaa ni **Tsh** 4,200,000,000 sawa na USD 3,000,000 na utekelezaji wake utaanza mapema mwakani 2011.Kazi hii imetekelezwa kwa mashirikiano na Kampuni ya M.M.K Projects Services Ltd ya Tanzania.

3. Ripoti ya mwisho imekamilika kwa asilimia 100% ya tathmini ya kuinua uwezo wa Manispaa katika mapato, mafunzo ya wafanyakazi na taaluma ya utoaji huduma bora (ZMC Institutional Strengthening). Fedha zilizotengwa ni Tsh 4,200,000,000 sawa na USD 3,000,000. Kazi hii imetekelezwa kwa mashirikiano na Kampuni ya DEGE Consult kutoka Denmark.

4. Ripoti imethibitishwa na wafadhili yaani Benki ya Dunia na Vitabu vya Zabuni vimekamilika. Fedha za awali zilizotengwa na Benki ya dunia ni **Tsh 2,800,000,000** sawa na USD 2,000,000. Kazi hii imetekelezwa kwa

mashirikiano na kampuni ya Electric Plan ya Tanzania na utekelezaji wa Kazi za ukarabati na uwekaji wa taa mjini unatarajiwa mapema mwakani 2011.

Mhe. Mwenyekiti, Baraza la Manispaa limefanya matengenezo madogo madogo Soko la Darajani ili kwenda sambamba na mahitaji ya huduma inayotolewa hapo sokoni, pamoja na matengenezo ya sehemu ya Mamalishe na machinjio ya kuku. Aidha, kwa upande wa matengenezo ya Soko la Mwanakwerekwe ilifanya matengenezo kwa kuziba paa, kutengeneza kuta na kutia zege na tunakusudia kutia lami eneo linalopita gari kwa kuimarisha mazingira.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuendeleza ujenzi wa Afisi ya Mapato iliopo Baraza la Manispaa kwa ujenga ghorofa moja lakini kutokana na uwezo mdogo wa kifedha, kazi hii tunatarajia kuiendeleza katika bajeti ya mwaka 2010/2011 baada ya kukamilika taratibu za kuomba kibali cha ujenzi kutoka Mamlaka ya Hifadhi ya Mji Mkongwe (*STCDA*).

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2010/2011 Baraza la Manispaa limekadiria kukusanya kutoka vyanzo vyake vya mapato jumla ya Tsh. 1,276,700,000 na matarajio ya ruzuku kutoka Serikali Kuu jumla ya Tsh. 1,328,315,459 na kufanya jumla ya mapato yote kwa mwaka 2010/2011 kuwa Tsh. 2,605,015,459. Vilevile Baraza la Manispaa limekadiria matumizi ya jumla ya Tsh. 2,620,032,587/=, ikiwa ni jumla ya Tsh. 2,527,632,587 kwa kazi za kawaida na Tsh. 92,400,000 kwa kazi za maendeleo.

Aidha, kutokana na uzito na ukubwa wa malengo ya mwaka 2009/2010, Baraza linatazamia kuyaendeleza hayo hayo katika mwaka 2010/2011.

MABARAZA YA MIJI NA HALMASHAURI ZA WILAYA

Mhe. Mwenyekiti, Mabaraza ya Miji yanahusika na kusaidia kupunguza kero za wananchi maeneo ya Miji, wakati Halmashauri zinatekeleza hayo katika maeneo yao nje ya Miji. Kero hizi ni za kiuchumi na kijamii kama zilivyoelezwa kwenye Mikoa. Pia vyombo hivi katika mwaka 2009/2010 vimetekeleza majukumu yao kutokana na makusanyo kutoka vianzio vyao tofauti vya mapato walivyo navyo. Miongoni mwao ni – Ushuru wa Uzalishaji *(Product Tax);* Leseni za Biashara *(Trade Licence*) Huduma za Mazao; Ada, Faini na Adhabu; Miradi ya Taka n.k.

Mhe. Mwenyekiti, utekelezaji wa malengo ya vyombo hivyo kwa mwaka 2009/2010 ni kama ifuatavyo:-

BARAZA LA MJI WETE

Mhe. Mwenyekiti, mbali na shughuli za kiutawala, Baraza katika kipindi cha mwaka 2009/2010 lilimudu kusimamia mambo matatu yanayojionesha hapo chini.

1. Kusimamia ujenzi wa nyumba bora za kisasa (tofali) na kutoa vibali 41 vya ruhusa ya ujenzi.
2. Kulifanyia ukarabati chinjio lililoko Pwani Wete.
3. Kuwahamasisha wananchi kujua afya zao kwa kuwapatia elimu ya afya na pia utunzaji na udumishaji wa usafi wa mazingira na namna ya kujilinda na maradhi ya miripuko.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka 2009/2010, Baraza la Miji la Wete liliomba ruzuku ya Tsh. 200,000,000/= kutoka Serikali Kuu na hadi kufikia mwezi wa Juni, Baraza limepokea Tsh. 158,780,000/= sawa na asilimia 79. Aidha, Baraza lililenga kukusanya Tsh. 28,598,000/= na hadi sasa limemudu kukusanya Tsh. 28,598,000/= sawa na (100%).

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha 2009/2010, Baraza limesaidia Ujenzi wa Soko – Bandarini (Tsh. 5,000,000/=); Ujenzi wa Soko la Mtemani (Tsh. 5,000,000/=) na kutoa misaada kwa Miradi ya Jamii (Tsh. 1,000,000/=) kama ilivyojipangia.

Aidha, kwa mwaka wa fedha 2010/2011 Baraza hili linaomba kupatiwa Ruzuku jumla ya Tsh, 233,304,000/= kutoka Serikali Kuu. Pia Baraza limepanga kukusanya jumla ya Tsh. 40,000,000/= kutoka vianzio vyake vya mapato na kutumia Tsh. 20,000,000/= kwa kazi za kawaida na Tsh. 20,000,000/= kwa kazi za maendeleo kama inavyoonekana hapo chini.

1) Ujenzi wa Soko la Mtemani - Tsh. 5,000,000/=
2) Ukarabati wa Ukumbi wa Mikutano (Jamhuri Hall) - Tsh. 5,000,000/=
3) Ukarabati wa Soko la Samaki la Kitutia - Tsh. 5,000,000/=
4) Uwekaji wa kifusi stendi ya magari Kitutia - Tsh. 3,000,000/=
5) Misaada kwa miradi ya jamii – Wete Mjini - Tsh. 2,000,000/=

Tsh. 20,000,000/=

BARAZA LA MJI MKOANI

Mhe. Mwenyekiti, Baraza la Mji Mkoani kwa mwaka wa fedha 2009/2010 liliomba ruzuku kwa Serikali Kuu yenye jumla ya Tsh. 140,000,000/= na hadi kufikia mwezi wa Juni, Baraza lilikuwa tayari limeshapokea jumla ya Tsh. 112,360,000/= sawa na asilimia 80.3. Aidha, kwa mwaka huo Baraza la Mji

Mkoani lilipanga kukusanya jumla ya Tsh. 14,240,000/= kupitia vianzio vya mapato ilivyonavyo na lilipanga kutumia Tsh. 7,540,000/= kwa kazi za kawaida na Tsh. 6,700,000/= kwa kazi za maendeleo. Hadi kufikia sasa Baraza liliweza kukusanya jumla ya Tsh. 15,305,900/= sawa na asilimia 107 na kutumia Tsh. 9,037,100/= kwa kazi za kawaida na Tsh. 5,914,500/= kwa kazi za maendeleo kwa kutekeleza miradi inayoonekana kwenye jadweli.

No	JINA LA MRADI	ULIOPO	LENGO	UTEKELEZAJI	%
1	Ukarabati wa Ukumbi Umoja Nguvu	Ngombeni	4,000,000	5,356,900	134
2	Ukarabati wa Soko la Samaki na Matunda	Mbuyuni	1,000,000	625,000	63
3	Ukarabati wa Ofisi ya Baraza	Makadara	500,000	584,600	117
4	Kusaidia miradi ya jamii	Eneo la Baraza	1,200,000	1,348,000	112
JUMLA			**6,700,000**	**7,914,500**	**118**

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2010/2011 Baraza la Mji Mkoani limeomba kupatiwa ruzuku kutoka Serikali Kuu Tsh. 200,000,000/=. Aidha, Baraza la Mji Mkoani limepanga kukusanya jumla ya Tsh, 17,000,000/= kutoka vianzio vyake vya mapato na kutumia Tsh. 7,500,000/= (44.1%) kwa kazi za kawaida na Tsh. 9,500,000/= kwa kazi za maendeleo kama inavyosomeka namba 1 hadi 5.

1) Ukarabati Ukumbi wa Mikutano Umoja ni Nguvu – Ngombeni - Tsh. 3,000,000/=
2) Ukarabati wa Soko la Samaki na Matunda Mbuyuni – Tsh. 1,500,000/=
3) Ukarabati wa Ofisi ya Baraza la Mji Makadara - Tsh. 1,700,000/=
4) Ujenzi wa slabi sita (6) Sokoni Bandarini Mapinduzi 2 Uweleni na Mikarafuuni – Tsh. 1,800,000/=
5) Misaada kwa Jamii - Tsh. 1,500,000/=

JUMLA **Tsh. 9,500,000/=**

BARAZA LA MJI CHAKE - CHAKE

Mhe. Mwenyekiti, Baraza lilipanga kukusanya jumla ya Tsh, 40,000,000/= kutoka vianzio vyake vya mapato. Sambamba na makusanyo hayo, Baraza lilipanga kutumia Tsh. 24,000,000/= kwa kazi za maendeleo na Tsh. 16,000,000/= kwa kazi za kawaida. Hadi kufikia mwezi wa Juni, Baraza liliweza kukusanya jumla ya Tsh. 29,790,000/= sawa na asilimia 74.5 na kutumia Tsh.18,690,700/= (117%) kwa kazi za kawaida na Tsh. 11,100,000/= sawa na asilimia 46.3 ya lengo kwa kazi za maendeleo kama kinavyoonyesha kiambatanisho namba 12 (a) cha miradi ya wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa 2010/2011, Baraza la Mji – Chake Chake – Pemba limeahidiwa kupatiwa Tsh. 353,640,000/= kutoka Serikali Kuu. Aidha, limepanga kukusanya Tsh. 50,000,000/= na kutumia Tsh. 20,000,000/= kwa kazi za kawaida na Tsh. 30,000,000/= kwa kazi za maendeleo kwa kutekeleza shughuli zinazoonekana katika jadweli:-

1) Ujenzi wa Ofisi Chake Chake	-	Tsh.	12,000,000/=
2) Ujenzi wa Soko Machomanne	-	Tsh.	5,000,000/=
3) Ujenzi wa banda la Soko la Samaki Tibirinzi	-	Tsh.	5,000,000/=
4) Ujenzi wa njia 3 za vidaraja Tingatinga, Tenga na Mtoni /Batini	-	Tsh.	5,000,000/=
5) Ujenzi wa sleb tatu (3) Bandataka, Msingini na Tibirinzi	-	Tsh.	900,000/=
6) Misaada kwa jamii	-	Tsh.	1,500,000/=
7) Uwekaji wa fusi Michakaini /Kisiwani	-	Tsh.	600,000/=
Jumla		**Tsh.**	**30,000,000/=**

HALMASHAURI YA WILAYA YA MAGHARIBI – UNGUJA

Mhe. Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Magharibi Unguja ililenga kukusanya jumla ya Tsh. 300,000,000/= kutoka vianzio vyake vya mapato. Na kutumia Tsh. 196,500,000/= (65%) kusaidia miradi ya maendeleo. Hadi kufikia mwezi huu, Halmashauri imemudu kukusanya Tsh. 293,140,899/= (97.7%) na kutumia Tsh. 156,388,400/= (79.6%) kwa kusaidia miradi ya maendeleo kama kiambatanisho namba 12 (b) kinavyoonyesha. Pia Halmashauri haikuweza kutekeleza Ujenzi wa Nyumba ya Wageni Bweleo na kituo cha Afya Chuini kutokana na kutokamilika kwa baadhi ya taratibu za hati miliki.

Mhe. Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Magharibi katika kipindi cha fedha cha mwaka 2010/2011 imelenga kukusanya Tsh. 367,000,000/= kutokana

na vianzio vyake vya mapato na kutumia kiasi cha jumla ya Tsh. 237,000,000/= kwa miradi ya Maendeleo sawa na 67.7% kiambatanisho namba 12 (c) kinavyoonyesha. Aidha, Tsh. 130,000,000/= zinatumika kwa shughuli za kawaida, vianzio vyake hivyo vinaonekana hapo chini.

Kifungu	**Aina ya Ada**	**Mataraji ya Mapato**
1200	Ushuru wa Mauziano	27,710,000/=
1400	Ushuru wa Uzalishaji	63,740,000/=
1500	Leseni za Biashara	150,840,000/=
1800	Huduma za Mazao	4,680,000/=
2000	Ada, Faini na Adhabu	36,000,000/=
-	Mradi wa Taka	83,400,000/=
	JUMLA	**367,000,000/=**

HALMASHAURI YA WILAYA YA KASKAZINI "A" – UNGUJA

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2009/2010 Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini "A" Unguja ililenga kukusanya Tsh. 50,000,000/= kutokana na vianzio vyake vya mapato. Mpaka kufikia mwezi wa Juni, Halmashauri imeweza kukusanya Tsh. 32,945,740/= sawa na asilimia 65.89. Kutokana na hali hiyo imeweza kutekeleza malengo iliyojiwekea kama kiambatanisho namba 12 (d) kinavyoonekana.

Mhe. Mwenyekiti, Halmashauri imeshindwa kutekeleza Mradi wa utoaji wa Mipira ya Maji – Kinyasini (Tsh. 1,500,000/=) na ujenzi wa Skuli ya Kilindi (Tsh. 2,000,000/=) kutokana na upungufu wa fedha.

Mhe. Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini "A" Unguja, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011 umelenga kukusanya Tsh. 50,200,000/= sawa na asilimia 50 kwa kazi za kimaendeleo na Tsh. 25,000,000/= sawa na asilimia 50 kwa kazi za kawaida kama inavyoonekana hapo chini.

1. Ununuzi wa mipira ya maji	2,000,000/=
2. Ujenzi wa Skuli ya Kilindi	1,000,000/=
3. Ujenzi wa Soko Mkwajuni	2,000,000/=
4. Malipo ya Gari la Halmashauri	3,000,000/=
5. Ukarabati wa Soko la Mkokotoni	3,000,000/=
6. Matengenezo ya Afisi ya Halmashauri	10,000,000/=
7. Utayarishaji wa maeneo ya Soko ya Pwani Mchangani na Kendwa	4,000,000/=

	JUMLA	**25,000,000/=**

HALMASHAURI YA WILAYA YA KASKAZINI "B" – UNGUJA

Mhe. Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini "B" Unguja katika mwaka fedha wa 2009/2010 ililenga kukusanya Tsh. 49,418,000/= na hadi kufikia mwezi wa Juni, tayari imeshakusanya jumla ya Tsh. 55,662,243/= sawa na asilimia 112.63% ya lengo kutokana na vyanzo vya mapato viliomo katika Halmashauri.

Mhe. Mwenyekiti, kati ya makusanyo hayo ya Tsh. 55,662,000/=, Halmashauri imetumia jumla ya Tsh. 23,759,100/= sawa na asilimia 42.68 kwa kazi za kawaida na kwa kazi za maendeleo, zimetumika jumla ya Tsh. 30,372,400/= sawa na asilimia 86.77 ya lengo lake.

Sambamba na hayo, Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini "B" katika mwaka wa fedha 2009/2010 ililenga kutumia jumla ya Tsh. 35,000,000/= kwa kusaidiana miradi ya wananchi badala yake kutumia Tsh. 29,372,000/= kama kinavyoonyesha kwenye kiambatanisho namba 12 (e). Aidha, katika kipindi hicho hicho cha mwaka 2009/2010 Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini "B" pia imeweza kutumia Tsh. 6,210,000/= kwa kusaidia miradi ya ziada kama kiambatanisho namba 12 (f) kinavyoonyesha.

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011 Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini "B" -Unguja imekadiria kukusanya kiasi cha Tsh. 60,000,000/= kutokana na vyanzo vya mapato vinavyoonekana katika jadweli.

Kifungu	**Aina ya Ada**	**Mapato**
1400	Mali asili	30,000,000/=
1500	Leseni za biashara	20,000,000/=
1800	Huduma	10,000,000/=
	JUMLA	**60,000,000/=**

Kutokana na makusanyo hayo Halmashauri inategemea kutumia Tsh. 40,000,000/= kwa kushirikisha kusaidia nguvu katika miradi ya wananchi inavyoonekana kwenye jadweli:-

1) Ujenzi wa Soko la Mahonda	5,000,000/=
2) Kuendeleza ujenzi wa Kituo cha Afya Kiongwe	7,000,000/=
3) Kuendeleza ujenzi wa Soko la Donge Mtambile	3,000,000/=
4) Ujenzi wa josho la Wanyama Muwanda	2,000,000/=
5) Ujenzi wa Ukumbi wa Mikutano wa Halmashauri	6,000,000/=
6) Msaada wa ujenzi wa madarasa ya Skuli za Wilaya	

	ya Kaskazini “B”	9,000,000/=
7)	Msaada wa usambazaji maji Vijijini	6,000,000/=
8)	Msaada wa wanao soma elimu ya juu	2,000,000/=
	JUMLA	**40,000,000/=**

HALMASHAURI YA WILAYA YA KUSINI – UNGUJA

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2009/2010, Halmashauri ya Wilaya ya Kusini – Unguja ililenga kukusanya Tsh. 48,370,900/= na kutumia Tsh. 26,200,000/= sawa na asilimia 54.2 kwa kutekeleza miradi ya maendeleo ya wananchi. Hadi kufikia mwezi huu tayari Halmashauri imeshakusanya Tsh. 42,640,000/= sawa na asilimia 88 na kutumia Tsh. 13,560,000/= kwa kutekeleza miradi ya wananchi kama kiambatanisho namba 12 (g) kinavyoonekana.

Mhe. Mwenyekiti, miradi ya namba 1 (Tsh. 700,000/=); namba 4 (Tsh. 700,000/=); namba 7 (Tsh. 700,000/=); namba 10 (Tsh. 700,000/=); na namba 14 (Tsh. 3,500,000/=). Aidha, katika kipindi cha fedha cha mwaka 2010/2011 Halmashauri ya Wilaya ya Kusini Unguja ina azma ya kukusanya Tsh. 56,219,000/= na kutumia Tsh. 23,250,000/= kwa kutekeleza miradi inayoonekana katika kiambatanisho namba 12 (h).

HALMASHAURI YA WILAYA YA KATI – UNGUJA

Mhe. Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi wa Juni, Halmashauri ya Wilaya ya Kati ilikwisha kusanya jumla ya Tsh. 70,401,143/= sawa na asilimia 112.93 ya lengo iliyojipangia la Tsh. 62,336,000/= katika kipindi cha mwaka wa fedha 2009/2010, na kutumia jumla ya Tsh. 21,500,000/= kwa kutekeleza ahadi zilizoahidiwa kwa Wananchi kwa asilimia 68.98 ya ahadi zake.

Mhe. Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Kati kwa mwaka wa fedha 2009/2010, ililenga kutekeleza na kusaidia Miradi kumi na moja (11) ya Wananchi ambayo hubuniwa na wananchi wenyewe. Katika utekelezaji wa miradi hiyo Halmashauri ilisaidia ufanikishaji wa kazi hizo kwa kusaidia vifaa mbali mbali vyenye thamani zinazoonekana kwenye kiambatanisho namba 12 (i).

Mhe. Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Kati Unguja, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011 inatarajia kukusanya jumla ya Tsh. 109,885,000/= kwa mapato ya kawaida na maendeleo sawa na asilimia 43.27 ya ongezeko la Tsh. 47,549,000/= ya lengo la mwaka 2009/2010 la Tsh. 62,336,000/=.

Sambamba na utekelezaji wa ahadi hiyo, pia Halmashauri ina azma ya kutumia jumla ya Tsh. 55,000,000/= katika miradi mbali mbali ya kijamii na wananchi kama inavyoonekana katika kiambatanisho namba 12 (j).

HALAMSHAURI YA WILAYA YA WETE – PEMBA

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2009/2010 Halmashauri ya Wilaya ya Wete ililenga kukusanya jumla ya Tsh, 24,833,000/= kupitia vianzio vyake vya mapato na kutumia Tsh.13,003,000/= kwa kazi za maendeleo na Tsh. 11,830,000/= kwa kazi za kawaida. Hadi kufikia mwezi wa Juni, Halmashauri hii imekusanya jumla ya Tsh. 23,750,000/= sawa na asilimia 96. Halmashauri iliweza kutumia Tsh. 10,746,000/= kwa kazi za kawaida na Tsh. 13,004,000/= kwa kazi za maendeleo kama kiambatanisho namba 12 (k) kinavyoonyesha.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2010/2011 Halmashauri Wilaya ya Wete imepanga kukusanya kupitia vianzio vyake vya mapato jumla ya Tsh 24,000,000 na kutumia Tsh. 11,000,000/= (45.8%) kwa kazi za kawaida na Tsh. 13,000,000/= (54.2%) kwa kazi za maendeleo kwa kutekelea miradi inayoonekana kwenye jadweli.

1	Kusaidia ujenzi wa madarasa	Skuli ya Uondwe	500,000/=
2	Kusaidia ujenzi wa madarasa	Skuli ya Kisiwani	500,000/=
3	Kusaidia ujenzi wa madarasa	Skuli ya Daya	500,000/=
4.	Kusaidia ujenzi wa madarasa	Skuli ya Gando	500,000/=
5	Kusaidia ujenzi wa madarasa	Skuli ya Jojo	500,000/=
6	Kusaidia ujenzi wa madarasa	Skuli ya Kokota	500,000/=
7	Kusaidia ujenzi wa madarasa	Skuli ya Mkoto	500,000/=
8	Ununuzi wa pikipiki ya Halmashauri		4,500,000/=
9	Utiaji fusi barabara ya Makaani	Ole	5,000,000/=
		JUMLA	**sh. 13,000,000/=**

HALMASHAURI YA WILAYA YA MICHEWENI – PEMBA

Mhe. Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni kwa mwaka wa fedha 2009/2010 ilipanga kukusanya jumla ya Tsh. 19,000,000/= na kutumia Tsh. 10,000,000/= kwa kazi za maendeleo na Tsh. 9,000,000/= kazi za kawaida. Hadi kufikia mwezi wa Juni, Halmashauri imekusanya jumla ya Tsh. 15,298,987/= sawa asilimia 80.5 na kutumia Tsh. 6,873,000/= sawa na asilimia 68.7 kwa kazi za maendeleo na Tsh. 8,425,887 sawa na asilimia 93.6 kwa kazi za kawaida. Hali halisi ya utekelezaji wa miradi iliopangwa ni kama inavyoonekana kwenye kiambatanisho namba 12 (l).

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2010/2011, Halmashauri ya Wilaya Micheweni imelenga kukusanya Tsh. 20,000,000/= na kutumia Tsh. 9,000,000/= (45%) kwa kazi za kawaida na Tsh. 11,000,000/= (55%) kwa kazi za maendeleo kama zinavyoonekana kwenye namba 1 hadi 5.

1. Kuendeleza Ujenzi wa Afisi ya Halmashauri Tsh. 2,000,000/=
2. Kusaidia ujenzi wa kituo cha Afya Bule Tsh. 3,000,000/=
3. Ujenzi wa chinjio Mziwanda Tsh. 2,000,000/=
4. Kusaidia miradi ya Jamii Tsh. 2,000,000/=
5. Kusaidia gharama za wanafunzi na majanga Tsh. 2,000,000/=

Tsh. 11,000,000/=

HALMASHAURI YA WILAYA YA MKOANI – PEMBA

Mhe. Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Mkoani kwa mwaka wa fedha 2009/2010 iliazimia kukusanya jumla ya Tsh. 18,000,000/= kutoka vianzio vya mapato na kutumia Tsh. 8,000,000/= kwa kazi za maendeleo na Tsh. 10,000,000/= kwa kazi za kawaida. Hadi kufikia mwezi wa Juni, Halmashauri hii imekusanya jumla ya Tsh. 13,968,700/= sawa na asilimia 76.6 na kuzifanyia matumizi ya Tsh. 7,158,700/= sawa na asilimia 71.6 kwa kazi za kawaida na Tsh. 6,810,000/= sawa na asilimia 85 kwa kazi za maendeleo kama kiambatanisho namba 12 (m) kinavyoonyesha.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2010/2011 Halmashauri ya Wilaya ya Mkoani imekusudia kukusanya jumla ya Tsh. 19,400,000/= kutoka vianzio vya mapato viliopo na kupanga kutumia Tsh. 10,400,000/= (53.6%) kwa kazi za kawaida na Tsh. 9,000,000/= (46.4%) kwa kazi za maendeleo na kutekeleza miradi inayoonekana kwenye jadweli.

1) Kuendeleza ujenzi wa soko la samaki na matunda Kangani - Tsh. 2,000,000/=
2) Kuendeleza ujenzi wa soko la samaki na matunda Mkanyageni - Tsh. 2,000,000/=
3) Kusaidia miradi ya wananchi - Tsh. 2,500,000/=
4) Ununuzi wa kiwanja cha kujenga Afisi - Tsh. 2,500,000/=

JUMLA **Tsh. 9,000,000/=**

HALMASHAURI YA WILAYA YA CHAKE CHAKE – PEMBA

Mhe. Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Chake Chake kwa mwaka wa fedha 2009/2010 ililenga kukusanya jumla ya Tsh, 17,240,000/= kutoka vianzio vyake vya mapato na kupanga kutumia Tsh. 5,500,000/= kwa kazi za maendeleo na Tsh. 11,740,000/= kwa kazi za kawaida. Hadi kufikia mwezi wa

Juni 2010, Halmashauri hii ilikuwa imekusanya jumla ya Tsh. 15,459,520/= sawa na asilimia 89.7 na kutumia Tsh. 11,587,520/= sawa na asilimia 98.7 ya lengo kwa kazi za kawaida na Tsh. 3,872,000/= sawa na asilimia 70.4 ya lengo kwa kazi za maendeleo kwa kutekeleza miradi ya wananchi kama inayoonekana kwenye kiambatanisho namba 12 (n).

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2010/2011 Halmashauri ya Wilaya ya Chake Chake imeazimia kukusanya jumla ya Tsh. 24,570,000/= kutoka vianzio vya mapato walivyonavyo na kutumia Tsh. 15,340,000/= (62.43) kwa kazi za kawaida na Tsh. 9,230,000/= (37.57) kwa kazi za maendeleo kwa kuanzisha mradi wa ujenzi wa vibanda 10 vya biashara (vitega uchumi) na kusaidia nguvu za wananchi katika Wadi 10 kama jadweli inavyoonesha.

1.	Ujenzi wa vibanda 10 vya biashara	Machomane	Tsh.	5,230,000/=
2.	Kusaidia nguvu za wananchi wadi	ya Ziwani	“	400,000/=
3.	Kusaidia nguvu za wananchi wadi	ya Kwale	“	400,000/=
4.	Kusaidia nguvu za wananchi wadi	ya Ng’ambwa	“	400,000/=
5.	Kusaidia nguvu za wananchi wadi	ya Ndagoni	“	400,000/=
6.	Kusaidia nguvu za wananchi wadi	ya Wawi	“	400,000/=
7.	Kusaidia nguvu za wananchi wadi	ya Vitongoji	“	400,000/=
8.	Kusaidia nguvu za wananchi wadi	ya Pujini	“	400,000/=
9.	Kusaidia nguvu za wananchi wadi	ya Chonga	“	400,000/=
10.	Kusaidia nguvu za wananchi wadi	ya Kilindi	“	400,000/=
11.	Kusaidia nguvu za wananchi wadi	ya Shungi	“	400,000/=
	JUMLA			**Tsh. 9,230,000/=**

UTEKELEZAJI KATIKA VIKOSI

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2009/2010 Vikosi vya SMZ viliidhinishiwa matumizi ya Tsh. 17,747,000,000/= kwa shughuli za kawaida na **Tsh**. **850,000,000** kwa kazi za maendeleo. Hadi hivi sasa, vikosi vimeshapatiwa Tsh. 16,027,098,085 sawa na asilimia 90 kwa kazi za kawaida na Tsh. 850,000,000 (1000%) kwa kazi za maendeleo - kama inavyoonekana kwenye kiambatanisho namba 1.

Mhe. Mwenyekiti, Vikosi vya SMZ kwa mwaka 2009/2010 vilitekeleza majukumu viliyojipangia kama ifuatavyo:-

KIKOSI MAALUM CHA KUZUIA MAGENDO – KMKM

Mhe. Mwenyekiti, Kikosi cha KMKM ni Idara ambayo ipo chini ya Wizara ya Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum yenye majukumu ya Ulinzi wa Taifa na kupambana na biashara za magendo, uvuvi haramu, maadui wa amani na utulivu na usalama wa Zanzibar na pengine popote katika ardhi ya Tanzania

itakapoamriwa kufanya hivyo. Hivyo kwa kuzingatia hayo, Kikosi cha KMKM kwa mwaka 2009/2010 kilijipangia kutekeleza mambo makuu 6.

1. Kuendelea kuimarisha nguvu za ulinzi wa doria baharini.
2. Kuendelea kuwapatia elimu ya kazi wapiganaji ndani na nje ya Kikosi.
3. Kuendelea kuwapatia sare na vifaa vya kulalia wapiganaji.
4. Kuendelea ujenzi wa Hospitali ya KMKM Kibweni.
5. Kuendelea kufanya ukarabati majengo ya Kikosi Unguja na Pemba.
6. Kuvipandisha vyombo vikubwa Chelezoni.

Aidha, utekelezaji wa malengo hayo ya Kikosi kwa mwaka 2009/2010 unaonekana kwenye Kiambatanisho namba 13.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa huduma za Afya, katika mwaka wa fedha 2009/2010 Kikosi cha KMKM kimeweza kutoa mchango wa huduma za afya kwa wapiganaji na jamii kupitia Vituo vyake vya Afya Unguja na Pemba kwa kadri ya wezo wa nyenzo ulivyoruhusu. Lakini pamoja na juhudi hizi zilizochukuliwa bado kuna uchache wa vitendea kazi katika Vituo hivyo vya Afya;- kama vile madawa ya kutosha, vifaa vya maabara na kadhalika. Hata hivyo pamoja na hayo, Vituo vya Afya vya KMKM Unguja na Pemba vimehudumia wagonjwa wa aina mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa huduma za mawasiliano kwa njia ya Redio na Simu Kikosini kwa kipindi cha 2009/2010 hali imekuwa ni ya wastani kwani bado kunahitajika kupatiwa vifaa vipya vya mawasiliano, hali iliopo sasa ni kufanya ukarabati wa kila mara wa vifaa vya mawasiliano. Kwa upande wa mawasiliano ya usafiri wa ndani, Kikosi kimeweza kuzifanyia matengenezo gari zake kwa kila zinapohitajika matengenezo. Hali ya usafari Kikosini uko katika hali ya kuridhisha.

Mhe. Mwenyekiti, malengo ya Kikosi kwa mwaka 2010/2011 ni kama ifuatavyo:-

1. Kuendeleza kuimarisha nguvu za ulinzi na doria baharini.
2. Kuendeleza kuwapatia elimu ya kazi wapiganaji ndani na nje ya Kikosi.
3. Kuendeleza kuwapatia sare na vifaa vya kulalia wapiganaji.
4. Kuendeleza ujenzi wa Hospitali ya KMKM Kibweni.
5. Kuendeleza kufanya ukarabati majengo ya Kikosi cha Chuo cha KMKM Kama.
6. Kuvipeleka vyombo vikubwa chelezoni.

7. Kuimarisha sehemu ya uzamiaji KMKM.
8. Kuchukua jitihada za kukipatia Kikosi vyombo vya doria vya baharini na kifaa maalum cha kutambua vyombo vinavyopita mbali katika bahari ya Visiwa vyetu vya Unguja na Pemba.
9. Kikosi cha KMKM kitashirikiana na Wizara kusimamia ujenzi wa Kituo cha Askari wake Tumbatu.

Mhe. Mwenyekiti, Kikosi cha KMKM ili kiweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa mwaka 2010/2011, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya fedha Tsh. 6,109,300,000/= kwa matumizi ya kawaida na Tsh. 250,000,000/= kwa matumizi ya maendeleo.

KIKOSI CHA JESHI LA KUJENGA UCHUMI – JKU

Mhe. Mwenyekiti, Kikosi cha Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU) kina jukumu la Ulinzi wa Taifa, vile vile kinashughulikia na utoaji wa mafunzo kwa vijana yakiwemo uzalishaji wa mali, uraia, ulinzi na kazi za amali. Katika mwaka 2009/2010, Kikosi cha Jeshi la Kujenga Uchumi kilijipangia na kutekeleza majukumu yake kama inavyoonekana kwenye kiambatanisho namba 14 (a).

Mhe. Mwenyekiti, kupitia shughuli zake za ndani za uzalishaji, Kikosi cha JKU kwa mwaka 2009/2010 kiliweza kukusanya jumla ya Tsh. 173,519,000/= kutokana na maeneo yanayoonekana hapo chini.

1.	Kilimo na Ufugaji	30,000,000/=
2.	Viwanda	36,519,000/=
3.	Ujenzi	10,000,000/=
4.	Huduma ya Ulinzi	97,000,000/=
	JUMLA	**173,519,000,000/=**

Aidha, matumizi ya fedha hizi yalielekweza kwa maeneo ambayo pamoja na kutokutengewa kasma utekelezaji wake usingeweza kuepukika. Maeneo hayo ni kama yanavyoonekana hapo chini.

1.	Ujenzi wa Mabweni ya Askari	-	22,500,630/=
2.	Bwalo la Makao Makuu	-	15,430,000/=
3.	Milango ya maduka	-	8,032,000/=
4.	Afisi ya Mkuu wa Chuo – Dunga	-	2,200,000/=
5.	Nyumba ya Mkuu wa Kituo – Dunga	-	3,400,000/=
6.	Ujenzi wa Hospitali – Kama	-	2,500,000/=
7.	Ukarabati wa Afisi ya MP – Upenja	-	2,800,000/=
8.	Ununuzi wa Jenereta	-	26,000,000/=
9.	Ulipaji wa madeni ya Wakandarasi	-	42,000,000/=

10. Operesheni na huduma kwa vijana	-	41,636,370/=
11. Mchango wa Hazina	-	7,000,000/=
	JUMLA	**173,519,000/=**

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha 2009/2010 Vituo vya Afya vya Kikosi cha JKU viliendelea kutoa huduma mbali mbali kwa Askari wake pamoja na Raia.

Mhe. Mwenyekiti, Kikosi cha JKU ni moja kati ya wadau wakubwa wa sekta ya michezo hapa nchini. Timu zake zimekuwa washiriki wakuu katika michezo mbali mbali kwa wanawake na wanaume na kuonesha mafanikio makubwa ndani na nje ya nchi. Aidha, Kikosi kwa kupitia vikundi vyake vya utamaduni kimekuwa kikitoa mchango mkubwa katika kuendeleza utamaduni hapa nchini.

Mhe. Mwenyekiti, aidha, kwa lengo la kuongeza ufanisi wa kazi, Kikosi cha JKU kinaendelea kuwapatia wapiganaji wake nafasi mbali mbali za kujiendeleza kimasomo ndani na nje ya nchi. Kama inavyoonekana katika kiambatanisho namba 14 (b).

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2010/2011 Kikosi cha JKU kimejipangia malengo yafuatayo ikiwa ni pamoja na kukamilisha yale ambayo hayakukamilika mwaka uliopita kama yanavyojieleza namba 1 mpaka 8.

1. Kumalizia ujenzi wa nyumba za wataalamu kutoka Misri huko JKU Bambi.
2. Kuendeleza ujenzi wa Skuli ya Sekondari ya JKU eneo la Mtoni.
3. Kuwaendeleza kielimu wapiganaji katika fani na ngazi mbali mbali ili kuongeza ufanisi.
4. Kulima mazao aina mbali mbali ikijumuisha mpunga, mahindi, mtama, muhogo, bustani na miti ya matunda jumla ya ekari 350.
5. Kuendeleza mradi wa ufugaji kuku wa nyama na mayai pamoja na kienyeji kutoka 6000 wa sasa kufikia idadi ya kuku 7000.
6. Kuendeleza ujenzi wa hodhi la maji kwa ajili ya mradi mkubwa wa mboga mboga JKU Bambi.
7. Uchimbaji wa kisima cha maji kwa ajili ya skuli za ufundi na sekondari zilizoko Mtoni.
8. Kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira kuendesha mradi wa kilimo cha mbegu ya mahindi kwa upande wa Unguja na mbegu ya mpunga kwa upande wa Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, Kikosi cha Jeshi la Kujenga Uchumi ili kiweze kutekeleza malengo yake kwa ufanisi katika mwaka ujao wa 2010/2011, naliomba Baraza

lako tukufu kuidhinisha matumizi ya Tsh. 4,535,000,000/= kwa kazi za kawaida na Tsh. 500,000,000/= kwa kazi za maendeleo.

KIKOSI CHA VALANTIA (KVZ)

Mhe. Mwenyekiti, Kikosi cha Valantia kina askari walioajiriwa na askari wa kujitolea na kina majukumu ya ulinzi wa nchi, viongozi na mali za Serikali kwa kushirikiana na Vikosi vya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Vikosi vya Muungano, popote katika ardhi ya Tanzania kitakapoamrishwa kufanya kazi. Pia Kikosi kama vilivyo Vikosi vyengine kina utaratibu wa kujipangia malengo ya utekelezaji katika kila kipindi cha makadirio ya matumizi ya fedha kila mwaka.

Mhe. Mwenyekiti, Kikosi cha Valantia katika mwaka wa fedha wa 2009/2010 kilijipangia malengo yake kama yanavyoonekana hapo chini.

- Kujenga uwezo wa Kikosi kielimu, vifaa vya kutendea kazi na kuwajengea uwezo wapiganaji wake kimafunzo;
- Kuimarisha Kambi za Valantia Unguja na Pemba;
- Ujenzi wa Makao Makuu ya Kikosi yalioko Mtoni; na
- Kuendeleza kilimo katika Kambi zake za Kikungwi na Muyuni.

Mhe. Mwenyekiti, Kikosi cha Valantia kwa mwaka 2009/2010 kiliweza kutekeleza mambo 3 yanayojieleza hapo chini.

1. Kuendeleza wapiganaji wake kielimu katika fani mbali mbali:-

FANI	**CHUO**	**IDADI**
a) Radio program	Mbweni	2
b) Uhasibu	CBE Dodoma	1
c) Uashi	Mbweni	1
d) Secretary	Chuo cha UMMA	1
e) Ufundi	JKU	1
f) Diploma ya Ualimu	SUZA	1
g) Uandishi wa habari	TSJ DSM	1
h) Ujuzi	Idara ya Majenzi	1
i) Ufundi	Karakana Kuu	1
JUMLA		**10**

2. Ujenzi wa Makao Makuu Kambi ya Mtoni.

3. Kikosi kimeweza kulima miti ya mivinje katika Kambi ya Kikungwi na Muyuni.

Mhe. Mwenyekiti, Kikosi cha Valantia katika mwaka wa fedha 2010/2011 kimelenga kutekeleza mambo 4 ambayo yanajieleza hapo chini.

1. Kuendeleza na kuimarisha nguvu za ulinzi na usalama wa nchi.
2. Kuendeleza na kuwapatia elimu ya kazi za ziada wapiganaji wake.
3. Kuendeleza na kuwapatia vifaa muhimu kwa wapiganaji wake katika Kambi mbali mbali za Unguja na Pemba.
4. Kuendeleza kufanya ukarabati wa majengo ya Kikosi Unguja na Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, Kikosi cha Valantia ili kiweze kufanya kazi zake kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha wa 2010/2011 naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya Tsh. 2,182,000,000/= kwa matumizi ya kawaida na Tsh. 100,000,000/= kwa kazi za maendeleo.

KIKOSI CHA ZIMAMOTO NA UOKOZI (KZU)

Mhe. Mwenyekiti, Kikosi cha Zimamoto na Uokozi kuanzia mwezi wa Julai, 2009/2010 kimeripotiwa jumla ya matukio 125 kama vile moto wa majumbani na mahoteli ya kitalii (72), moto wa misitu na mashamba (27), ajali za ndege (3), moto wa mashine za umeme *(transformer)* (6), moto wa majaa (2), moto wa magari (3), moto wa uongo (2), kuingia binadamu visimani (5), kuingia wanyama kwenye visima (4) na moto wa meli (1).

Mhe. Mwenyekiti, matukio yote hayo kwa pamoja yameacha hasara ya Tsh. 881,000,000/= pamoja na vifo vya binadamu wanne (4). Aidha, jumla ya Tsh. 4,750,000,000/= ziliokolewa wakati wa kuyakabili matukio mbali mbali ya ajali na kuyaokoa maisha ya binadamu kumi na tisa (19) na wanyama.

Mhe. Mwenyekiti, aidha, kukosekana kwa umeme kwa kipindi kisichopungua miezi mitatu katika Kisiwa cha Unguja na kiangazi kikubwa kilichoikumba nchi yetu kulichangia kuongezeka kwa majanga ya moto yaliyosababishwa na matumizi makubwa ya majenereta, kandili na mishumaa.

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2009/2010 Kikosi cha Zimamoto na Uokozi kilifanikiwa kusimamia malengo kiliyojipangia na yale yote yaliyoshindikana 2008/2009 na kuyaingiza mapya kama inavyosomeka hapo chini.

1. Kusimamia huduma za Zimamoto na Uokozi kwenye Viwanja vya Ndege Unguja na Pemba katika viwango vinavyokubaliana kitaifa na kimataifa bila ya usumbufu wowote. Ambapo jumla ya ndege 2198 za aina na ukubwa tafauti zilihudumiwa na Kikosi wakati wa kutua, kuruka na zinapojaza mafuta.

2. Kuhudhuria na kutoa huduma za uzimaji moto na uokozi wa maisha ya watu pamoja na mali zao kila wakati ilipohitajika.

3. Uimarishaji wa vifaa na Magari katika Vituo vyote vya Zimamoto Unguja na Pemba.

4. Kuendelea kuimarisha rasilimali watu kwa kuwapatia mafunzo mbali mbali nchini na nje ya nchi:

    a) Kuwaendeleza wafanyakazi 10 katika fani ya Uhasibu na Manunuzi;

    b) Kufundisha wafanyakazi ishirini (20) katika fani ya Kompyuta, Takwimu, Mipango, Utunzaji Nyaraka na Ufundi;

    c) Kuwaendeleza kimafunzo *(Special Trainning)* katika Chuo cha Zimamoto na Uokozi, wafanyakazi hamsini (50) ngazi za kati na hamsini (50) ngazi ya juu endapo mradi wa Chuo cha Zimamoto utazingatiwa na kupatiwa fedha katika mwaka huo; na

    d) Kutoa mafunzo mbali mbali kuhusu tatizo la *HIV/AIDs* kwa wafanyakazi wote.

5. Kuyaendeleza majengo yaliyomo katika Vituo vya Zimamoto Unguja na Pemba.

    a) Umalizaji uzio wa Afisi Kuu ya Zimamoto Chanjaani Pemba na matayarisho ya

kutengeneza nyumba za makaazi kwa Maafisa na Wapiganaji wa Kikosi;

b) Kuanza maandalizi ya awali kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha Mchanga Mdogo Mkoa wa Kaskazini Pemba;

c) Matayarisho ya awali ya ujenzi wa maeneo mapya ya Muyuni, Tunguu, Uroa na Kiwengwa; na

d) Matayarisho ya awali ya Ujenzi wa Kituo cha Zimamoto wanakwerekwe eneo linaloegeshwa magari ya mawe, mchanga na kokoto.

6. Kutoa elimu zaidi ya kujikinga na majanga ya moto kwa jamii kwa kutumia mikutano, semina, vyombo vya habari, vipeperushi, magazeti na kadhalika.

7. Kuishauri Serikali (Shirika la Bandari) juu ya uanzishwaji wa kituo cha Zimamoto Bandari ya Malindi.

8. Kuendeleza kuwapatia sare maafisa na wapiganaji pamoja na vifaa vya kulalia.

9. Kuwapatia elimu ya juu ya Zimamoto Maafisa na Wapiganaji nje na ndani ya nchi. Nafasi (4) au zaidi kwa kutegemea wafadhili nje ya nchi na nafasi nane (8) kwa ajili ya mafunzo ndani ya nchi.

Mhe. Mwenyekiti, utekelezaji wa malengo kwa mwaka 2009/2010 umefanyika kama inavyojieleza hapo chini.

1. Gari moja la kuzimia moto lilipatikana na kupelekwa katika Kituo cha Zimamoto Chanjaani – Pemba.

2. Gari la kubebea wagonjwa *(Ambulance)* imepelekwa katika Kituo cha Karume Pemba.

3. Mipira ya kuzimia moto *(Delivery Hose)* ilipatikana na kusambazwa kwenye Vituo vya Unguja na Pemba.

4. Nguzo za kupambana na moto *(Ordinary Fire Suits)* zilipatikana na kusambazwa katika sehemu husika. Pamoja na kuwapatia sare Maafisa na Wapiganaji wa Zimamoto.

5. Kwa upande wa kuwapatia mafunzo wapiganaji, askari watatu (3) wanaendelea na masomo ya Sheria katika ngazi ya Shahada ya Kwanza katika Chuo Kikuu cha Tunguu, askari wawili (2) wamepatiwa mafunzo ya uongozi katika Chuo cha Utumishi – Zanzibar. Sambamba na hayo, askari wanane (8) wamepatiwa mafunzo ya kompyuta, Uhasibu na Manunuzi *(Procurement)* na askari kumi (10) wamepatiwa mafunzo ya Ufundi Magari, Umeme, Takwimu na Utunzaji Nyaraka. Aidha, umalizaji wa ujenzi wa uzio Afisi Kuu Chanjaani Pemba umekamilika.

Mhe. Mwenyekiti, mwaka 2009/2010 Kikosi cha Zimamoto na Uokozi kilikabiliana na changamoto mbali mbali ambazo zimeorodheshwa hapo chini.

- Askari sitini (60) tulioahidi kupatiwa mafunzo mbali mbali ya Zimamoto, hawakupatiwa kutokana na uchache wa fedha;

- Maandalizi ya ujenzi wa Kituo cha Zimamoto cha Mchanga Mdogo Mkoa wa Kaskazini Pemba, hayakufanyika kutokana na eneo tulilopewa kuambiwa sio letu na tumepewa kwa makosa wakati hatua za kulipia gharama za upimaji tayari zilikwisha kufanyika;

- Ujenzi wa Kituo cha Zimamoto Kiwengwa haukufanyika kutokana na kutokabidhiwa eneo la kiwanja husika kutoka Idara ya Upimaji ambako nako pia hatua za malipo ya gharama za upimaji zilikwisha kufanyika;

- Kikosi cha Zimamoto kinaendelea na tatizo la upatikanaji wa maji ya uhakika wakati wa kuyakabili matukio mbali mbali ya moto, jambo ambalo linasababishwa na ukosefu na uchakavu wa visima vya kuchukulia maji *(fire hydrants)* kwenye maeneo ya Miji yetu;

- Kuendelea kwa ujenzi holela na usio na mpango hususan katika maeneo ya ng'ambo ya miji yetu, ujenzi ambao husababisha kutolifikisha karibu na tukio la ajali gari la kuzimia moto pindipo inapotokezea; na

- Kujengeka kwa dharau ya waendeshaji vyombo vya aina mbali mbali barabarani wakati gari la Zimamoto linapokwenda kutoa huduma huwa halipatiwi nafasi ya njia itakayowezesha kukimbilia kwa haraka.

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2010/2011 Kikosi kinakusudia kuyakamilisha yale yote ambayo hayakukamilika kwa kipindi kilichopita kama yanavyosomeka kuanzia namba 1 mpaka 10.

1. Kuendelea kutafutwa vifaa na magari ya kuzimia moto na kusambazwa kwenye maeneo mapya na yale ambayo huduma zake bado hazijakamilika.

2. Suala la mawasiliano ya uhakika ndani ya Kikosi yatapewa kipaumbele kwa kutafutwa *Radio Call* na kusambazwa katika sehemu zote za kazi.

3. Kujenga jengo la mapumziko *(Rest House)* na Afisi Kuu ya Zimamoto Chanjaani Pemba.

4. Suala la upatikanaji wa sare na vifaa vya kulalia kwa ajili ya Askari wa Kikosi litapewa kipaumbele.

5. Hatua madhubuti zitachukuliwa za kuwapatia mafunzo mbali mbali Maafisa na Wapiganaji wa Zimamoto yakiwemo ya:-

   Zimamoto na Uokozi wa maisha na mali za watu (nje ya nchi wanne (4) na ndani ya nchi mia moja na ishirini na tano (125); Uongozi watano (5); Uhasibu na Uboharia kumi (10); Ufundi wa magari wanne (4); Uashi (4); Umeme wanne (4); Fundi Bomba wanne (4) na Kompyuta wanne (4).

6. Elimu zaidi itaendelea kutolewa kwa jamii ya kujikinga na majanga ya moto pamoja na uchimbaji wa visima vya maji na vyenye usalama.

7. Kuendelea kuishauri Serikali juu ya uanzishwaji wa Vituo vya Zimamoto na Uokozi Bandarini na kuomba kushirikishwa katika *Joint Building Committee* ya Manispaa ili kutoa ushauri katika majengo mapya yanayojengwa yaendane na matakwa ya Zimamoto.

8. Kushauriana na Taasisi husika juu ya kurekebishwa sheria ya kulazimika kuwekwa kwa vifaa vya huduma ya mwanzo vya kuzimia moto *(First Aid Fire Extinguisher)* katika magari ya biashara.

9. Kuboresha vifaa vya kinga *(Protecting tools)* kwa wafanyakazi ili waweze kutoa huduma kwa ufanisi zaidi.

10. Kuishauri Serikali juu ya kufanya manunuzi ya boti za kuzimia moto baharini na bandarini *(Fire Fighting Boats).*

Mhe. Mwenyekiti**,** Kikosi cha Zimamoto na Uokozi ili kiweze kutekeleza malengo yake kwa ufanisi zaidi naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya Tsh. 1,789,000,000/= kwa matumizi ya kawaida.

KIKOSI CHA CHUO CHA MAFUNZO (MF)

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2009/2010 Kikosi cha Chuo cha Mafunzo kinaendelea kutekeleza jukumu lake la kudhibiti na kuwalinda wanafunzi (wafungwa) na mahabusu pamoja na uzalishaji mali. Wakiwa vyuoni wanafunzi hupatiwa taaluma ya kazi za amali katika kilimo, ufugaji na ufundi ili wamalizapo kutumikia adhabu zao wawe raia wema na waweze kujitegemea kimaisha.

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha Aprili, 2009 hadi Machi, 2010 jumla ya mahabusu 2152 walipokelewa katika Chuo cha Mafunzo. Kati yao 2079 wanaume na 73 wanawake. Miongoni mwao 1538 waliachiwa na Mahakama kwa dhamana na wengine kuachiwa kabisa baada ya kuonekana kuwa hawana hatia. Aidha, katika kipindi hicho jumla ya wanafunzi 547 wamepokelewa katika Chuo cha Mafunzo; wakiwemo wanaume 532 na wanawake 15 sawa na ongezeko la asilimia 14 ikilinganishwa na idadi ya wanafunzi waliopokelewa mwaka jana. Umri na rika wa wanafunzi hao ni kama unavyoonekana katika jadweli.

UMRI	WANAUME	WANAWAKE	JUMLA
1. 11 – 20	68	2	70
2. 21 – 30	274	7	281
3. 31 – 40	152	4	156
4. 41 – 50	26	1	27
5. 51 na zaidi	2	1	13
JUMLA	**532**	**15**	**547**

Takwimu zinatuonesha kuwa bado idadi kubwa ya wanafunzi au mahabusu waopelekwa chuoni ni vijana na baadhi yao ni watoto walio chini ya miaka 20.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa shughuli za uzalishaji mali katika mwaka 2009/2010 Chuo cha Mafunzo kiliweza kutekeleza malengo yake ya kilimo cha vipando mbali mbali kama jadweli inavyosomeka.

AINA YA SHUGHULI	LENGO 2009/2010	UTEKELEZAJI	%
Mpunga wa umwagiliaji	Ekari 30	Ekari 20	75
Mpunga wa kutegemea mvua	Ekari 50	Ekari 54	108
Mahindi	Ekari 40	Ekari 40	100
Muhogo	Ekari 100	Ekari 100	100
Viazi vitamu	Ekari 10	Ekari 15	150
Migomba	Ekari 10	Ekari 5	50
Mboga mboga	Ekari 5	Ekari 5	100

Mhe. Mwenyekiti, michezo ni njia moja wapo ya kuwajengea wapiganaji ukakamavu wa kimwili na afya nzuri pamoja na kuwa na uwelewano wa karibu kati yao na wapiganaji wa Vikosi vyengine vya SMZ na SMT na raia kwa jumla.

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2010/2011, Idara ya Chuo cha Mafunzo imekusudia kutekeleza mambo 10 kama yanavyoonekana.

1. Kulima mpunga ekari 70
2. Kulima muhogo ekari 110
3. Kulima viazi vitamu ekari 10
4. Kuendeleza kilimo cha mboga mboga
5. Kuendelea na ukarabati wa Chuo cha Mafunzo Ubago
6. Kuendelea na ujenzi wa bweni la kulala wanafunzi Kinumoshi
7. Kuendeleza ujenzi wa nyumba ya koo mbili Kangani – Pemba
8. Kuendeleza ujenzi wa nyumba ya koo mbili Ubago – Unguja
9. Ufuatiliaji wa upatikanaji wa hati miliki eneo la kujenga Chuo cha Mafunzo cha kisasa Hanyegwa Mchana
10. Kusimamia ujenzi wa Ofisi ya Kamanda wa Chuo cha Mafunzo Wete.

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Chuo cha Mafunzo ili iweze kutekeleza kazi zake kwa ufanisi zaidi katika kipindi cha fedha cha mwaka 2010/2011 naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha Tsh. 3,766,000,000/= kwa matumizi ya kazi za kawaida.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mara nyengine tena, naomba kuutumia muda huu kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha mimi pamoja na kikao chako Kitukufu kuwa na ***ILHAM*** ya kuisikiliza na kupokea taarifa ya utekelezaji ya Wizara yangu. Aidha, naomba pia unikubalie niwashukuru watendaji wote wa Wizara ya Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ kwa juhudi zao walizozifanya kwa kuandaa makadirio haya ya mwaka 2010/2011 mpaka kufikia leo kuyawasilisha mbele ya Baraza lako Tukufu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba pia niwashukuru kwa dhati watendaji wangu wakuu wakiwemo Naibu Katibu Mkuu, Wakurugenzi, Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa, Wilaya, Madiwani, Masheha, Makamanda wa Vikosi, Makatibu wa Mabaraza ya Miji na Halmashauri za Wilaya pamoja na viongozi mbali mbali na wananchi kwa jumla kwa mashirikiano yao waliyoyaonesha katika kuzikabili shughuli za Taifa hili kwa bidii, ari, busara na uzalendo mkubwa katika kipindi hiki cha uongozi wangu.

Mhe. Mwenyekiti, nitakuwa sina fadhila kama nitaacha kuwashukuru watendaji wote wa Idara ya Upigaji Chapa – Zanzibar ambao pamoja na matatizo makubwa yanayowakabili wakati wa maandalizi ya shughuli hizi wamefanikisha uchapishaji wa Hotuba hii ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara yangu ya mwaka 2010/2011 kwa wakati na kuweza kuisoma mbele yako na Baraza lako Tukufu.

Mhe. Mwenyekiti, niruhusu pia nikushukuru tena wewe binafsi, Baraza lako Tukufu, pamoja na Kamati zako zote za Baraza hili kwa mashirikiano na miongozo mizuri waliyotupatia kila ilipohitajika. Aidha, Wizara inawashukuru wale wote kwa njia moja au nyengine waliochangia katika shughuli za maendeleo mbali mbali ya kiuchumi na kijamii katika maeneo tofauti hususan Taasisi za Kiserikali, zisizo za Kiserikali za ndani na nje na miongoni mwao ni:- UNDP, UNFPA, UNICEF, ADB, TASAF, SIDA, ZAYADESA, PADEP, ASSP/ASDPL, MACEMP, WORLD BANK, Watu Binafsi wakiwemo Waheshimiwa Wabunge, Wawakilishi, Wakuu wa Mikoa, Wilaya, Madiwani na kadhalika.

Mhe. Mwenyekiti, ili Taasisi yangu iweze kukabili utekelezaji wa majukumu yake kwa ufanisi zaidi katika kipindi cha 2010/2011 naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe matumizi ya Tsh. 25,886,300,000/= kwa kazi za kawaida kwa Wizara ya Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ na Tsh. 2,210,000,000/= kwa kazi za maendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Haji Mkema Haji (Makamo Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala): Mhe. Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii adhimu kutanguliza shukrani za dhati kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kuendelea kutujaalia neema ya uhai na afya njema na pia kutuwezesha kukutana tena hapa katika Baraza letu tukufu ili kuendeleza majukumu muhimu ya kitaifa kwa maslahi ya wananchi na Taifa kwa ujumla.

Mhe. Mwenyekiti, pili napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii kusimama mbele ya Baraza lako tukufu ili niwasilishe maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ kwa mwaka 2010/2011.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala inawapongeza sana watendaji wote wa Wizara hii kwa jitihada zao wanazozichukua katika kutekeleza majukumu yao kiufanisi na kwa moyo wa kujitolea kwa lengo la kuitumikia nchi na wananchi wake wote pamoja na ustahamilivu wao wanaouonesha katika kutekeleza majukumu hayo katika mwaka wa fedha 2009/2010. Vile vile napenda kuwapongeza na kuwashukuru tena watendaji wote wa Wizara hii kwa mashirikiano yao mazuri waliyotuonesha kwa Kamati yetu hii wakati ilipokuwa ikipitia Makadirio ya Bajeti ya Wizara hii kwa mwaka 2010/2011.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Katiba, Sheria na Utawala ya Baraza la Wawakilishi wanajulikana, naomba itoshe kutamka kuwa nawashukuru kwa mashirikiano yao makubwa waliyoyaonesha na ninauthamini mchango wao walioutoa katika Kamati yetu ilipokuwa ikipitia Bajeti ya Wizara Wizara ya Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ kwa mwaka wa fedha 2010/2011. Mhe. Mwenyekiti, baada ya shukrani hizo, naomba sasa nitoe maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Makadirio ya Bajeti ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2010/2011 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kutoa shukrani hizo naomba sasa uniruhusu nitoe maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ kwa mwaka wa fedha 2010/2011 kama ifuatavyo:-

VIKOSI VYA SMZ

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala inavipongeza Vikosi vya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa juhudi kubwa vinavyochukua katika kutekeleza vyema majukumu yao kwa lengo la kuhakikisha kuwa

wananchi wanaishi kwa amani na utulivu. Aidha, Kamati yetu imeridhika na juhudi ya Vikosi vyetu vyote hasa kwa kushiriki vyema katika shughuli mbali mbali za Kitaifa. Tunawapongeza kwa juhudi zao hizi na tunamuomba Mwenyezi Mungu awajaalie kila la kheiri hapa duniani na huko akhera kwenye maisha ya milele.

Mhe. Mwenyekiti, hali ya maslahi ya wapiganaji wetu ni madogo mno ukilinganisha na maisha halisi tuliyokuwa nayo. Hivyo, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala inaiomba Tume ya Utumishi ya Vikosi vya SMZ kuendelea kuifanyia mapitio mishahara ya Vikosi vya SMZ kwani umepita muda mrefu sasa Serikali haijaongeza mishahara ya watumishi hao wa umma.

Mhe. Mwenyekiti, sambamba na hayo, tunaiomba Serikali kupitia Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kuendelea kuviingizia Vikosi vya SMZ vinavyotoa huduma za afya kwa wapiganaji na jamii vifaa vya kisasa na madawa ya kutosha ili vikosi hivi viweze kutekeleza dhamira yao hiyo.

KIKOSI MAALUM CHA KUZUIA MAGENDO (KMKM)

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yetu imeridhishwa sana na utekelezaji wa majukumu ya Kikosi hichi ikiwemo shughuli kuu na muhimu ya kuimarisha doria za baharini na nchi kavu ambayo imekuwa ikitekelezwa kwa mafanikio makubwa. Mhe. Mwenyekiti, Kamati yetu inakiomba Kikosi hiki kuzidi kuendelea kutekeleza hili kwa nguvu zao zote, ili kunusuru mapato ya nchi yasipotee pamoja na kuzuia uingiaji wa watu nchini kinyume na utaratibu. Mhe. Mwenyekiti, ili suala hili liweze kutekelezwa kwa ufanisi mkubwa, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala inaiomba Serikali kuwapatia wapiganaji wa kikosi hiki vifaa bora na vya kisasa.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri katika hotuba yake katueleza kuwa kikosi hiki kitaendelea kusimamia Mradi wa Ujenzi wa Hospitali katika mwaka wa fedha ujao. Katika kutekeleza hili Kikosi hiki kimekisiwa kuingiziwa jumla ya Tsh. 250,000,000/-. Mhe. Mwenyekiti, Kamati yetu inaunga mkono hili kwani katika mwaka wa fedha 2009/2010 kikosi hiki kilisimamia vyema ujenzi wa hospitali hii. Hivyo, Kamati hii inaiomba Serikali kukipatia Kikosi cha Kuzuia Magendo fedha hizo mapema ili ujenzi huo ukamilike haraka na kianze kutoa huduma za matibabu kwa wagonjwa. Mhe. Mwenyekiti, tunasisitiza hili kwani hospitali hii haitoi huduma kwa askari wa kikosi hichi pekee bali hutoa hata kwa raia wa kawaida. Sambamba na hilo, kikosi hiki kina nia ya kutekeleza lengo la nne ambalo ni “Kupunguza vifo kwa watoto wachanga” na lile lengo la tano “Upatikanaji wa huduma bora za uzazi” ya Malengo ya Maendeleo ya Milenia kama Serikali yetu ilivyoahidi. Hii ni kutokana na kuwa hospital hii itatoa huduma za mama na wajawazito.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yetu inaiomba Serikali kupitia Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kutoa ushirikiano wa karibu kwa kikosi hichi hususan katika kukipatia wataalamu, ili hospitali hii iweze kufikia malengo na kuweza kutoa huduma iliyokusudiwa.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yetu haijaridhishwa na kitendo cha Askari wa KMKM kulitumia jengo la Afisi ya Wilaya Ndogo Tumbatu kama Kambi ya Askari hawa. Hii ni kutokana na kuwa afisi hii hutoa huduma kwa wananchi, hivyo, sio busara kuwepo wapiganaji hawa. Kutokana na hayo tunaiomba wizara hii kwa mwaka wa fedha ujao kuwapatia wapiganaji wetu hawa eneo mbadala ili kuwatenganisha askari na jamii katika shughuli zao za kawaida.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri katueleza katika ukurasa wa 76 kuwa Kikosi cha KMKM kwa mwaka ujao wa fedha kinatarajia kufanya ukarabati majengo ya KMKM Kama. Mhe. Mwenyekiti, Kamati yetu inaunga mkono lengo hili ili kuwapatia mazingira mazuri wapiganaji. Hata hivyo, kamati inaiomba Serikali kuyaangalia na majengo ya KMKM Pemba. Hii ni kutokana na kuwa majengo ya Kikosi hiki kwa Pemba hayaridhishi hata kidogo na yanatishia usalama wa wapiganaji.

KIKOSI CHA CHUO CHA MAFUNZO (MF)

Mhe. Mwenyekiti, tunaipongeza sana Serikali kupitia Chuo Cha Mafunzo kwa kuimarisha huduma za wanafunzi na mahabusu kwa kuwapatia chakula, magodoro pamoja na madawa, ingawa huduma hizo zinazotolewa bado hazijafikia kiwango cha kuridhisha. Mhe. Mwenyekiti, Kamati yetu inamshauri Kamanda wa Chuo cha Mafunzo kuipanga vyema ratiba ya chakula, ili wanafunzi na mahabusu wapate mlo unaoridhisha.

Mhe. Mwenyekiti, kamati yetu pia, imefarajika na tamko la Mhe. Waziri kuwa katika mwaka wa fedha 2010/2011 kikosi hiki kina lengo la kusimamia ujenzi wa Afisi ya Kamanda wa Chuo cha Mafunzo Pemba. Hii ni kutokana na kuwa jengo lake la afisi limeanguka na hivi sasa anafanya shughuli zake katika afisi ambayo hailingani na hadhi yake. Hivyo, kamati yetu inaomba suala hili lifuatiliwe kwa ukaribu zaidi ili kulinda hadhi ya Kamanda huyo.

KIKOSI CHA JESHI LA KUJENGA UCHUMI (JKU)

Mhe. Mwenyekiti, kamati yetu inakipongeza kwa dhati kikosi hiki kwa hatua na jitihada zao thabiti wanazozionesha kwenye mradi wa kilimo cha mboga mboga, mradi ambao unatekelezwa kwa ushirikiano kati ya Serikali ya Misri pamoja na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kupitia Kikosi cha Jeshi la Kujenga

Uchumi huko Bambi. Mhe. Mwenyekiti, kwa mara nyengine tena tunaiomba serikali kukiingizia Kikosi cha JKU jumla ya Tsh. 500,000,000/- mapema iwezekanavyo ili waweze kuendeleza shughuli za kilimo hicho.

Mhe. Mwenyekiti, sambamba na hayo, kamati yetu inaishauri serikali kufanya mazungumzo na wenzetu wa Misri kwa upande wa kuchagua aina za mboga mboga za kuzalishwa zinazopendwa na wanachi wa Zanzibar ambao ndio watumiaji wa mboga mboga hizo. Kwani imebainika kuwa mradi huu huzalisha mboga mboga ambazo wananchi wetu hawazipendelei. Jambo ambalo linakwamisha kupata soko la uhakika na kuupelekea mradi huu kupata hasara.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa Pemba tunaiomba serikali kukipatia matrekta kikosi hichi, kwani imebainika kuwepo kwa upungufu mkubwa wa nyezo hii muhimu katika uzalishaji hususan kwa zao la mpunga. Hali ambayo inapelekea kushuka kwa uzalishaji kutokana na kutokuwepo matrekta ya kutosha kwenye Kikosi cha JKU.

KIKOSI CHA VALANTIA

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri katueleza kuwa kikosi hiki kinatarajia kuendeleza kufanya ukarabati wa majengo ya kikosi Unguja na Pemba kwa mwaka wa fedha ujao. Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala inaunga mkono lengo hili na inakishauri kikosi hiki kuchukua juhudi za makusudi na kuhakikisha kuwa majengo ya Kikosi cha Valantia hususan kwa upande wa Pemba yanafanyiwa ukarabati huo kwa asilimia kubwa. Kwani mazingira ya afisi hizi hayaridhishi na hayaleti picha nzuri ya kiutendaji kwa askari hawa.

KIKOSI CHA ZIMAMOTO NA UOKOZI

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na jitihada zinazochukuliwa na kikosi hichi katika kuokoa majanga ya moto pamoja na ajali nyengine, bado kikosi hichi hakijaweza kufikia katika kiwango kizuri katika shughuli zao za uokozi. Hali hii inapelekea wananchi wengi kukosa imani na kikosi hichi kutokana na kuchelewa kufika kwenye baadhi ya matukio ya moto kunakosababishwa na ujenzi holela pamoja na kukosa nyenzo za kutosha kwa ajili ya shughuli za uokozi. Jambo hili hupelekea baadhi ya wananchi kuwakejeli waokoaji hawa kwa kuamini kwamba hawana msaada ambao wanaweza kuutoa. Hali hii ni ya kusikitisha hasa ukilinganisha na umuhimu wa chombo hichi kwa usalama wa raia na mali zao.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa Mhe. Waziri katueleza kuwa kikosi hiki kitaendelea kutafuta vifaa na magari ya kuzimia moto katika mwaka ujao wa fedha. Kamati yetu inashauri zichukuliwe jitihada za makusudi ili kukibadilisha hadhi na uwezo kikosi hichi na kuweza kufanya kazi kwa ufanisi na mafanikio zaidi ili kujenga imani kwa wananchi. Aidha, tunaiomba Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi na Taasisi zote za Serikali zinazohusika na masuala ya ujenzi kuwa makini wakati zinavyotoa vibali vya ujenzi sambamba na kukishirikisha kikosi hiki kwenye *Joint Building Committee*, ili tuwe na majengo na ramani nzuri itakayoiwezesha Kikosi cha Zimamoto na Uokozi kufika bila usumbufu kwenye matukio mbali mbali ya majanga.

Mhe. Mwenyekiti, tunaunga mkono lengo la 10 la kikosi hiki la kuishauri serikali kufanya manunuzi ya boti maalum za kuzimia moto baharini na bandarini. Hii ni kutokana na kuwa bandari ni sehemu muhimu sana katika shughuli mbali mbali za nchi. Hivyo, ni busara chombo hiki kikanunuliwa kwa ajili hiyo.

BARAZA LA MANISPAA

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya Katiba Sheri na Utawala inalipongeza Baraza la Manispaa kwa jitihada wanazozifanya katika kuyatekeleza majukumu yao waliyopewa kisheria. Hata hivyo, tunaliomba Baraza hili lijitahidi kuhakikisha kuwa mji wetu unakuwa safi wakati wote. Kwani kuna baadhi ya maeneo bado kimazingira hayaridhishi. Aidha, tunalipongeza Baraza la Manispaa kwa kuanza kuchukua hatua ya kuwakamata wanyama hususan ngo'mbe waliokuwa wanazurura ovyo katika maeneo mbali mbali ya mji. Kamati yetu inaunga mkono hili kwani litaondosha usumbufu kwa watumiaji mbali mbali wa barabara.

Mhe. Mwenyekiti, tunalipongeza Baraza la Manispaa kwa kuitikia wito wa Mhe. Waziri Kiongozi kuzitengeneza taa za barabarani kwa kushirikiana na mafundi wa Shirika la Umeme pamoja na Benki ya Dunia. Hatua hii ni muhimu kwani itapelekea kupungua kwa wimbi wa uhalifu na kuimarika kwa usalama wa raia, wageni na mali zao hususan katika nyakati za usiku.

MABARAZA YA MIJI NA HALMASHAURI ZA WILAYA

Mhe. Mwenyekiti, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilianzisha mfumo wa Serikali za Mitaa kwa kutambua kwamba Serikali za Mitaa ni nyenzo muhimu ya kupambana na vita dhidi ya umaskini, ujinga na maradhi. Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala inayapongeza na kuzithamini jitihada zinazofanywa na Mabaraza ya Miji pamoja na

Halmashauri za Wilaya kwa kushiriki kikamilifu katika shughuli mbali mbali za kijamii ikiwemo kutunza usafi wa miji yetu, kusimamia na kuweka utaratibu wa kuendesha biashara pamoja na kushiriki katika kuendeleza miradi mbali mbali ya kijamii kama vile; ujenzi wa mabanda ya skuli, ujenzi wa masoko, vituo vya afya na kadhalika.

Hata hivyo, baadhi ya Mabaraza ya Miji na Halmashauri za Wilaya hushindwa kutekeleza malengo waliyojipangia kutokana na uhaba wa fedha unaozikabili. Hivyo, kamati inaishauri serikali kuziongezea ruzuku taasisi hizi ili ziweze kutekeleza malengo ipasavyo.

Aidha, Kamati yetu inaziomba taasisi hizi kupanua wigo wa ukusanyaji mapato badala ya kuendelea kutegemea vianzio vilivyozoeleka. Kwani kuna baadhi ya vianzio hivi bado havijafikiwa na kusababisha Mabaraza ya Miji na Halmashauri za Wilaya kushindwa kukusanya mapato iliyokadiriwa kukusanya.

Mhe. Mwenyekiti, sambamba na maelezo hayo, Kamati yetu inaiomba serikali kuzipatia Taasisi hizi Wataalamu wa kutosha, ili kuzijengea uwezo mzuri kiutendaji. Kwani kwa hivi sasa shughuli ya ukusanyaji wa mapato hufanywa na vijana ambao hawana taaluma kuhusiana na kazi hiyo. Jambo ambalo hulikosesha mapato taasisi hizi.

MIKOA YA ZANZIBAR

Mhe. Mwenyekiti, tunazipongeza jitihada za Mikoa na Wilaya katika kutekeleza majukumu yake mbali mbali. Yakiwemo ya kuratibu na kusimamia vyema miradi mbali mbali ya maendeleo. Ili kuwasogezea kwa karibu huduma muhimu wananchi na kuwaondoshea usumbufu wa kuzifata huduma hizo Mjini. Hivyo, Kamati yetu inaiomba Mikoa na Wilaya kuzidi kuwa karibu na wananchi, kwa lengo la kuwahamasisha kujikusanya pamoja na kujaribu kubuni shughuli mbali mbali za maendeleo ili waweze kujiajiri wenyewe na hatimae kuweza kutatua changamoto mbali mbali za kimaisha zitakazowakabili.

Mhe. Mwenyekiti, katika hotuba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya Baraza la Wawakilishi – Zanzibar kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya kazi za Kawaida na Maendeleo ya Wizara ya Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ kwa mwaka wa fedha 2009/2010 aliyoiwasilisha mbele ya Baraza hili. Tuliishauri Serikali kuitengea kila Wilaya fungu lake ili kuondosha mifarakano baina ya Watendaji hawa, pamoja na kutekeleza wazo lililotolewa na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi – Zanzibar. Hii ni kutokana na kuwa Wilaya hupatiwa

fedha kidogo na Mikoa yao. Mhe. Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa napenda kuliarifu Baraza lako kuwa suala hili halikuchukuliwa hatua yoyote na wakati tunaipitia na kuichambua bajeti ya Wizara hii kasoro hii ilijitokeza tena. Kwa mantiki hiyo, Kamati yetu inaiomba Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Uchumi – Zanzibar kwa mara nyengine tena kuliangalia kwa kina suala hili kutokana na sababu niliyoieleza hapo awali.

Mhe. Mwenyekiti, wakati tunapitia Bajeti ya Wizara hii tulitaka kujua ni kigezo gani kinachotumiwa na Wizara ya Fedha na Uchumi wakati wa kugawa **"**Ceiling**"** kwa Mikoa?. Tunahoji hili baada ya kubaini kuwa Mikoa yenye wakaazi wengi hupata fedha kidogo na ile Mikoa yenye wakaazi kidogo hupata fedha nyingi. Kwa bahati mbaya hatukupata jibu lililoturidhisha kutoka kwa Watendaji wa Wizara ya Fedha na Uchumi. Hivyo, tunamuomba Mheshimiwa Waziri wa Nchi (AR) Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi atusaidie ufafanuzi wa swali letu hili.

IDARA YA USAJILI NA UTOAJI VITAMBULISHO VYA MZANZIBARI MKAAZI

Mhe. Mwenyekiti, tunaipongeza Idara ya Usajili na Utoaji Vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi kwa kuandaa vitambulisho vyenye ubora wa hali ya juu. Hatua hii ni muhimu kwani vitambulisho hivyo havitaharibika haraka endepo Mtumiaji kwa bahati mbaya atafikwa na janga lolote.

Mhe. Mwenyekiti, miongoni mwa malengo ya Idara hii kwa mwaka wa fedha ujao ni kuendelea kuwaelimisha wananchi juu ya matumizi bora na sahihi ya vitambulisho vya Mzanzibari.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya Katiba Sheria na Utawala inaipongeza Idara ya Usajili na Utoaji Vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi kwa kuwa na nia ya kuliendeleza hili. Kwani pamoja na jitihada kubwa zinazochukuliwa na Idara hii bado baadhi ya wananchi hawajaelewa matumizi sahihi ya vitambulisho hivyo, pamoja na hatua ambazo mtu anapaswa kuzifuata iwapo atakosa haki hiyo. Hivyo, tunapenda kuchukuwa fursa hii kuwaomba wananchi kufuatilia vipindi mbali mbali vya Redio na Televisheni pamoja na kusoma vijarida vinavyotaarishwa na Idara hii.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yetu iliidhinishia Wizara ya Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ jumla ya Tsh. 25,886,300,000/- kwa kazi za Kawaida na Tsh. 2,210,000,000/- kwa kazi za Maendeleo. Hivyo, kama tulivyowaidhinishia kwenye Kamati naliomba pia na Baraza lako Tukufu liyakubali makisio haya na kuwaidhinishia Wizara ya Nchi (AR) Tawala za

Mikoa na Vikosi vya SMZ na Taasisi zake ili wakatekeleze majukumu yao kwa mwaka wa fedha 2010/2011.

HITIMISHO

Mhe. Mwenyekiti, napenda sasa kuwashukuru Wajumbe wote wa Baraza kwa kunisikiliza kwa makini na utulivu, pia napenda kukushukuru kwa mara nyengine tena wewe binafsi kwa kuniruhusu kutoa maoni ya Katiba, Sheria na Utawala.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo napenda kutamka kwa niaba ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala na kwa niaba ya wananchi wa Jimo langu la Koani ninaunga mkono hoja ya Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ. Aidha, nawaomba Wajumbe wote wachangie na kuunga mkono Makadirio ya Bajeti ya Wizara hii kwa ajili ya utekelezaji bora wa majukumu na malengo waliyojipangia.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha maoni ya kamati.
Mhe. Mwenyekiti, baada ya maoni ya kamati, naomba unigaie dakika chache ili nitowe maoni ya wananchi wa Jimbo la Koani.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nishukuru Mkoa wangu wa Kusini Unguja kwa mafanikio tuliyoyapata katika mwaka wa fedha unaomalizika. Mafanikio haya yaliongozwa na Mkuu wangu wa Mkoa wa Kusini Mhe. Mustafa Moh'd Ibrahim, nampongeza sana kwani hata katika mwaka huu hata Jimbo la Koani tumepata mafanikio makubwa ambayo mimi mwenyewe yananiridhisha naweza kujivunia.

Pia sitomsahau Mkuu wangu wa Wilaya Mhe. Ali Hassan Khamis kwa mashirikiano yake mazuri tulipofanya kazi pamoja. Nawashukuru wabunge wa Wilaya ya Kati na wawakilishi wenzangu wa Jimbo la Chwaka Mhe. Moh'd Kombo Mkanga na Jimbo la Uzini Mhe. Tafana Kassim Mzee, kwa jitihada zao za kunishirikisha katika kunielimisha na kunisaidia kwenye miradi mbali mbali ili kuleta maendeleo kwa wananchi wa Jimbo langu la Koani, lakini kwa maendeleo ya Wilaya nzima. Nawashukuru sana kwa jitihada zao hizo.
Pia nitakuwa mkosefu wa fadhila kama sikumshukuru sana Katibu wangu wa Halmashauri, bwana Boniface Joseph Mwale, ambaye kwa muda mfupi tu amekuja katika wilaya yetu tumeona mafanikio yake mazuri na wilaya yetu sasa inakwenda vizuri katika ukusanyaji wa mapato pamoja na kuweka miradi ya maendeleo ya wananchi.

Vile vile madiwani wangu wa wilaya, hasa wa Jimbo la Koani, sitomsahau Shaaban Jabu Diwani wa Wadi ya Koani, Bi Sharifa Maabadi wa Wadi ya Jumbi, bwana Moh'd Haji Ushahidi wa Wadi ya Unguja Ukuu na ndugu Suleiman Ali Makame Diwani wa Wadi ya Uzi. Viongozi hawa tumeshirikiana vizuri katika kuleta maendeleo na tunamaliza mkataba wetu wa miaka mitano tukiwa tumefanya kazi nzuri katika jimbo hili.

Aidha, tunawashukuru wananchi wa Jimbo la Koani kwa kutupa mashirikiano mazuri katika kipindi chote hicho. Kwa hivyo, kutokana na mashirikiano ambayo wananchi wametupa ndio mafanikio tuliopata, hivyo ni lazima tujisifie tusingoje kusifiwa. Tumefanya kazi vizuri na kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka ujao tunawaomba mkataba kwa wananchi. Natumia nafasi hii kutangaza rasmi nia ya kutaka kuomba tena miaka mitano ijayo.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana.

Mhe. Mwenyekiti: Nilifikiria unataka kuomba kura hapa, nilitaka kukuambia sio pahala pake. Ahsante sana Mhe. Makamo Mwenyekiti, wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala. Sasa tumsikilize Mhe. Waziri Kivuli wa Wizara ya Nchi Afisi ya Rais Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: (Waziri Kivuli wa Wizara ya Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ): Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote, kwanza hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa ihsani yake ya kuendelea kutweka na uhai pamoja na afya njema katika kipindi hichi cha takriban miaka mitano sasa, na tukaweza kuitumikia nchi yetu kwa uwezo wetu wote, na hatimae tukaweza kuweka mikakati madhubuti ambayo kutekelezwa kwake kunaweza kuinasua nchi yetu na wananchi kwa jumla kutoka katika dimbwi la umasikini.

Mhe. Mwenyekiti, pia naomba niitumie fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa kuweza kuniruhusu nitoe mchango wangu kwa niaba ya Kambi ya Upinzani kuhusu bajeti hii iliyoko mbele yetu.

Pia, Mhe. Mwenyekiti, nadhani nitakua mchache wa shukurani kama sikuitumia fursa hii kuendelea kuwashukuru wananchi wa jimbo la Chonga, kwa uamuzi wao sahihi sana waliofanya mnamo mwaka 2005, kwa kunichagua mimi kuwa mwakilishi wao bila shaka wamejivunia mengi mazuri. Nadhani kwa mazuri hayo niliyowatendea wataendelea kunipa tena ridhaa zao kwa miaka mitano myengine na ijayo.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya dibaji hiyo fupi sana, nadhani sasa nianze kuiwakilisha kambi yangu tukufu ya upinzani kwa kusema machache kuhusu bajeti hii iliyopo mbele yetu.

Mhe. Mwenyekiti, kimsingi Wizara hii imegawika katika Idara tatu pamoja na vikosi vitano kama ifuatavyo:-

1. Idara ya Mipango na Sera
2. Idara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa
3. Idara ya Usajili na utoaji vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi
4. Kikosi maalum cha kuzuia magendo (KMKM)
5. Kikosi cha Mafunzo (MF)
6. Kikosi cha Zimamoto na Uokozi (KZU)
7. Kikosi cha JKU
8. Kikosi cha Valantia

Mhe. Mwenyekiti, mafanikio ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii pamoja na Taasisi zake hutegemea sana umahiri wa uongozi wa wizara kwa upande mmoja na uwezeshwaji wa kifedha na vitendea kazi kwa upande mwengine pamoja na uzalendo uliojaa nia safi katika utekelezaji huo wa majukumu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba hapa uniruhusu nisikitike kidogo. Kwani nyingi ya sifa nilizozitaja hapo juu, viashiria vyetu vinaonesha wizara hii imezikosa. Nani kutokana na mapungufu hayo ndio maana Wizara hii tayari sasa inakaribia kukamilisha miaka mitano bila ya kuonesha mafanikio makubwa ya kiutendaji.

Mhe. Mwenyekiti, nimelazimika kusema haya kutokana mambo yafuatayo:-

IDARA YA TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

Mhe. Mwenyekiti, Idara hii imejigawa katika sehemu mbili, ambazo ni Tawala za Mikoa kwa upande mmoja na Serikali za Mitaa kwa upande mwengine.

Upande wa Tawala za Mikoa ambao inajumuisha pamoja na Wilaya na Shehia wajibu wao mkubwa ni kusimamia maamuzi ya Serikali Kuu pamoja na kutatua matatizo na mizozo inayotokea katika jamii.
Mapungufu yanayojitokeza katika sekta hii ni ukosefu wa nia safi katika utekelezaji wa majukumu yao.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majukumu makubwa ya Wakuu wa Mikoa, wanajukumu pia la kuwateua masheha. Inasikitisha sana na inaudhi kuona

masheha wengi wao hawaonekani kuwa na sifa zinazohitajika za kuwawezesha kufanya kazi zao kwa ufanisi na uadilifu mkubwa. Uelewa wao katika mambo ya Uongozi wa Kijamii ni mdogo. Taaluma zao ni ndogo sana kiasi cha kushindwa hata kujieleza vizuri mbele ya Jamii. Hawajui hata majukumu yao ya msingi.

Mimi nilitarajia kuona kwamba masheha watakua watu wasioegamia upande wowote; uwe wa kidini, kikabila au kisiasa, lakini bahati mbaya sana masheha wetu wamekosa sifa hii muhimu na wanaonekana kujifanya mawakala wa CCM. Hayo yamedhihirika wazi wazi katika utekelezaji wa majukumu yao hasa hasa katika zoezi la usajili wa vitambulisho vya Mzanzibari mkaazi na katika zoezi la uandikishaji wa daftari la wapiga kura. Masheha wote wamekua wakiegamia sana upande wa CCM, jambo ambalo linawapotezea wananchi wengi imani kwa masheha hao.

Mhe. Mwenyekiti, kama kweli Wakuu wa Mikoa wana nia safi wangewateulia wananchi masheha ambao: wanauelewa mkubwa wa mambo katika jamii, wanaheshimika sana, wana busara za kutosha za uongozi na wasioegamia upande wowote wa itikadi za kisiasa.
Mhe.Mwenyekiti, ni aibu kubwa kwa nchi kama yetu ambayo takriban miaka kumi sasa inapania kuelekea kwenye utawala boara, lakini inashindwa kuwapata masheha waliona uwezo wa kuinganisha jamii badala ya kuigawa.

SERIKALI ZA MITAA

Mhe, Mwenyekiti, mafanikio makubwa na yenye kuridhisha katika sekta ya maendeleo ya jamii hupatikana kupitia mtandao mzuri wa serikali za mitaa. Serikali za mitaa ndizo zinazotoa picha halisi ya mgawanyo wa madaraka kutoka serikali kuu kwenda kwa wananchi wenyewe. Ni kupitia Serikali za Mitaa ndipo wananchi hupata fursa ya kujipangia mipango yao ya maendeleo kutokana na vipaumbele walivyojipangia wenyewe.

Pia wananchi hupata fursa ya kutambua matumizi ya pesa zao yalivyoendeshwa na hupata fursa ya moja kwa moja ya kuweza kuhoji, pale ambapo wanahisi pesa zao hazikutumika ipasavyo. Kwa mantiki hiyo basi tunaweza kusema kwamba mfumo mzuri wa serikali za mitaa, ndio kielelezo muhimu cha kuweza kupima kiwango cha utawala bora katika nchi.

Mhe, Mwenyekiti, ni bahati mbaya sena kwamba ni miaka mingi ilipita, serikali ya SMZ bado haikua imeona umuhumi wa kuunda Serikali za Mitaa hapa nchini. Hata hivyo, katika mwaka 1992 ndio kwa mara ya mwanzo serikali iliona umuhimu wa kuwepo kwa serikali za mitaa na kuanzia hapo ndio zikaanzishwa halmashauri za wilaya na mabaraza ya miji katika sura hii

inayoonekana hadi sasa, lakini ni bahati mbaya sana kwamba mfumo huu uliopo bado unakabiliwa na changamoto nyingi ambazo zimefanya mfumo mzima uwe hauna maana na hauleti tija iliyokusudiwa.
Mhe. Mwenyekiti, miongoni mwa mapungufu yanayozikabili Halmashauri na mabaraza ya miji hapa Zanzibar ni hizi zifuatazo:-

1. Sheria ziliopo zinazoendesha serikali za mitaa hazielezi vizuri juu ya majukumu ya Halmashauri, mabaraza ya miji pamoja na shehia.
2. Serikali za mitaa hapa Zanzibar zinakubaliwa na ukosefu wa watendaji wenye uwezo na ujuzi, wengi wao wameajiriwa bila ya kuwa na sifa zinazohitajika.
3. Kuna kinyangi'anyiro cha mapato baina ya serikali kuu na Mabaraza ya miji na halmashauri pamoja na mashehia jambo ambalo linazinyima serikali za mitaa mapato na kupelekea kushindwa kujiendesha.
4. Hakuna Idara ya Serikali za mitaa inayojitegemea inayoweza kusimamia majukumu yake pamoja na haki zake kwa ufanisi mkubwa.
5. Hakuna wataalamu wa sheria katika serikali za mitaa wanaoweza kusimamia haki zao.
6. Kutokana na mkanganyiko wa sheria inaonekena sasa sheha ambae kateuliwa na mkuu wa mkoa kutokana na sababu anazozijua yeye, ana nguvu zaidi katika jamii kuliko. Mhe. Diwani ambae ana ridhaa za wananchi walio mengi.
7. Kuna mgongano wa madaraka ya kiutendeji kati ya sheha na diwani, kazi nyingi ambazo ilikua azifanye diwani zinafanywa na sheha inaonekana kwamba madiwani na masheha bado hawajawekewa bayana majukumu yao.
8. Kutokana na uwezo mdogo wa kitaaluma walionao watendaji wa serikali za mitaa imepelekea kushindwa kudhibiti vyanzo vyao vya mapato, hali iliyopelekea serikali kuu kuhodhi vyanzo hivyo vya mapato na kuziwacha serikali za mitaa zikiwa hazina vyanzo vya mapato vya kutosha na kwa hivyo kushindwa kufanya kazi zake kwa ufanasi.

Mhe, Mwenyekiti, kutokana na mapungufu hayo na mengine kadhaa ambayo sikuweza kuyaainisha katika waraka huu kwa kuchelea kutumia muda mkubwa zaidi, mimi kwa niaba yangu na kwa niaba ya kambi yangu tukufu ya upinzani napendakeza mambo yafuatayo:-

1. Kuna haja ya kuwa na sera ya serikali za mitaa ingawaje tumepata maelezo kwamba kuna mchakato wa kuandaa sera hiyo, lakini inasikitisha sana kuona kwamba serikali bado haijatoa umuhimu

unaostahiki wa kupata sera hii kwani mchakato wa utayarishaji wa sera hii unakwenda taratibu sana.

2. Ili kuondosha migongano ya kiutendaji kati ya serikali za mitaa na serikali kuu ni lazima sheria zilizounda serikali za mitaa zifanyiwe mapitio na hatimae zirekebishwe.
3. Serikali kuu ikubali kupunguza madaraka yake na kuyapeleka katika serikali za mitaa.
4. Ajira katika serikali za mitaa zifanywe upya ili kuwapata watendeji wenye elimu na taaluma itakayokidhi haja na kuleta ufanisi.
5. Uwekwe mfumo unaofaa wa kugawana mapato baina ya serikali kuu na serikali za mitaa kutokana na vyanzo vilivyomo katika serikali za mitaa.
6. Ni vyema wizara inayoshughulikia serikali za mitaa ipunguziwe mzigo wa kushuhulikia vikosi ili ipate nafasi ya kutosha ya kuratibu ufanisi wa serikali za mitaa.
7. Mhe. Mwenyekiti, kambi yangu ya upinzani inaamini kwamba iwapo mapendekezo hayo yatafanyiwa kazi, basi siku moja wananchi wa Zanzibar watajikuta wamepata fursa zaidi za kupanga, kuainisha vipaumbele vya maendeleo, kufanya maamuzi shirikishi katika kudhibiti raslimali zao pamoja na kuweza kuwawajibisha viongozi wasiowafaa hali ambayo inaaweza kuleta picha nzuri ya utawala bora.

BARAZA LA MANISPAA

Mhe. Mwenyekiti, moja katika Taasisi muhimu katika nchi yoyote iliyomakini ni Baraza la Manispaa. Taasisi hii inajukumu kubwa la kuutunza mji, kupanga vizuri sehemu za biashara, mabustani pamoja na kutunza usafi katika mji.

Katika hutuba zangu nyingi zilizopita nimekua nikitoa lawama kali kuhusu jinsi Baraza la Manispaa lilivyokosa umakini katika kuundeleza mji wetu. Mji ulikua mchafu takataka za biashara hasa kutoka soko la mkunazini zilivyokua zikizagaa na kuleta udhia mkubwa kwa watu walioutembelea mji wetu. Mji ulikua hauna mitaro ya kupitia maji machafu na kwa hivyo nyakati za mvua mji huu ulikua hautamaniki.

Mhe. Mwenyekiti, hapa nataka nijisifu kidogo kwamba juhudi yangu ya takriban miaka mine ya kulipigia kelele hili sasa imezaa matunda. Tumeona jinsi manispaa sasa walivyopania katika kuweka usafi, tumeshuhudia magari ya kusombea taka yalivyoingia nchini na sasa yale mabaki ya vichwa vya ng'ombe pale Darajani hayaachwi tena yakaleta harufu mbaya. Pia tumeshuhudia mitaro ya maji taka ikijengwa upya takriban mji mzima na tulitazamia kuwa tatizo la kutuama maji kwa wingi katika mji wetu lingetoweka kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, jambo la kusikitisha, na kwa kweli linaudhi na linakatisha tama sana, ni kuona kwamba pamoja na juhudi za washirika wa maendeleo kutumia fedha za walipakodi wao katika kutusaidia sisi, ili tatizo la kutuama maji machafu katika mji wetu liondoke. Kuna watu hawaoneshi hata dalili ya kuthamini juhudi hizo za madampo ya kutupia taka, na kutokana na tabia hiyo huenda tatizo la kutuama maji machafu katika mji wa Zanzibar na kuchafua mandhari ya mji likarudi pale pale.

Mhe. Mwenyekiti, naiomba Manispaa ili kulinda heshima yake hasa mbele ya washirika na maendeleo waliofadhili mradi wa michili, wawe imara katika kuilinda mitaro hile ili pesa walizotusaidia zisiwe zimepotea bure.

WILAYA NDOGO KOJANI

Mhe. Mwenyekiti, Wajumbe wa Baraza lako tukufu kupitia kamati ya Katiba Sheria na Utawala ilifanya ziara mara kadhaa kukagua ujenzi wa Wilaya ndogo ya Kojani. Lakini kwa kweli kilichobainika ni kwamba mkandarasi aliepewa kazi ya kujenga jengo hilo anaonekana ama hana uwezo wa kazi aliyoiomba, au ni tapeli. Ujenzi hule una kasoro nyingi na kwa kweli hauridhishi hata kidogo na inasikitisha sana kuona wizara imenyamaza kimya, nyumba hile haikutumia kiwango cha kuwa ofisi ya serikali, inavuja, madirisha ni ya kienyeji sana, samani zilizomo ni za kughushi milango yote ni mibovu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli nyumba ile haifai, na mimi kwa niaba ya Kambi ya Upinzani siko tayari kuridhia bajeti ya wizara hii, mpaka waziri aliambie Baraza hili ni kwanini pesa za walipa kodi wetu zimefanyiwa udanganyifu katika kiwango kile. Pia atueleze hatua atakazozichukua katika kuhakikisha anaokoa pesa za walipa kodi wetu.

IDARA YA USAJILI NA UTOAJI VITAMBULISHO VYA MZANZIBARI MKAAZI

Mhe. Mwenyekiti, idara hii iliundwa kufuatia matakwa ya sheria namba 7 iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi mwaka 2005. Malengo makubwa ilikua ni kuwasajili Wazanzibari ambao wametimia miaka 18.

Katika tafsiri ya kawaida unaweza kuona kwamba ni jambo jema sana kuwapa vitambulisho Wazanzibari, kwani huo ndio utambulisho wao wa kuweza kumjua yupi ni mzanzibari na yupi si mzanzibari katika nchi yetu. Vitambulisho hivi ndivyo ambavyo vingeiwezesha serikali kutoa haki kwa wale wazanzibari halisi katika zile haki ambazo angestahiki mzanzibari pekee na sio mgeni, kama vile haki ya kupiga kura.

Mhe. Mwenyekiti, tangu kuundwa kwa idara hii na mimi Abdalla Juma nikawa Waziri Kivuli wa Wizara hii, takriban miaka mine iliyopita, nimekua na juhudi kubwa sana ya kubainisha mapungufu makubwa yaliyoonekana kuikabili idara hii katika sheria yake, katika sera yake na hata katika utekelezaji wa zoezi lenyewe la kusajili Wazanzibari na kutoa ID.

Miongoni mwa kasoro hizo ni kule kuelezwa katika sheria kwamba atakaesajiliwa na kupewa kitambulisho ni yule Mzanzibari mkaazi tu. Hii ni kasoro kubwa kwa sababu yule Mzanzibari asiyekua mkaazi anakua hana haki ya kupewa kitambulisho hicho na kwa hivyo kunyimwa haki zake za msingi kama Mzanzibari.

Kwa mfano, Katiba yetu ya Zanzibar inampa haki ya kupiga kura kila Mzanzibari alietimia miaka 18, mwenye akili timamu bila ya kujali anaishi wapi. Sasa sheria hii na kama kuna nyengine yoyote inayokiuka amri hii ya Katiba sheria hiyo ni batili na haitafaa kutumika. Hebu leo natuangalie ni Wazanzibari wangapi wamenyimwa haki ya kuandikisha kuwa mpiga kura kutokana na sheria hii. Kwa kweli katika hili, SMZ imefanya kosa kubwa la Kikatiba.

Si hayo tu, lakini tatizo jengine linaloikabili Idara hii ni kwamba; ile sheria imetamka wazi kwamba kila Mzanzibari mkaazi alietimia miaka kumi na nane atasajiliwa na kupatiwa kitambulisho cha Mzanzibari mkaazi, lakini katika utekelezaji wake, jambo linalozingatiwa zaidi ni cheti cha kuzaliwa, na pale inapotokea mtu kukosa cheti cha kuzaliwa, hata kama ana umri wa miaka mia (100) basi ananyimwa kitambulisho hicho. Jambo ambalo ndani ya sheria ya vitambulisho halikuainishwa. Mimi nilidhani anatakiwa mtu alete cheti cha kuzaliwa ili kuthibitisha umri, lakini anakuja mtu na nywele zimefanya mvi kama vile Mhe. Spika, lakini bado ananyimwa kwa kisingizio cha kukosa cheti cha kuzaliwa. Hivyo kweli mtu kama Mhe. Spika, kuna mtu anaweza kumtilia mashaka kuwa hafiki miaka 18? Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli kuna wananchi ambao hawapungui 20,000 wamenyimwa vitambulisho kutokana na visingizio kama hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na misingi hiyo, kwa kweli mimi kwa niaba ya Kambi yangu ya Upinzani tumepoteza imani na Idara ya Vitambulisho na tunahisi haikuundwa kwa nia safi. Ningemshauri Mhe. Rais akaishughulikia idara hii ipasavyo, ili kutuondolea wasi wasi tulionao.

VIKOSI VYA SERIKALI YA MAPINDUZI ZANZIBAR.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na ukubwa na majukumu mengi iliyonayo wizara hii, pia imepewa mzigo mwengine wa uratibu wa shughuli za vikosi vya SMZ. SMZ pamoja na kuongoza nchi yenye eneo dogo na watu wachache lakini inavyo vikosi vya ulinzi vitano ambavyo ni:-

KMKM, JKU, MF, KZU pamoja na KVZ

Mhe. Mwenyekiti, vikosi kwa uchache pamoja na uchache wa fedha unayoikabili serikali, lakini hulazimika kutumia zaidi ya Tsh. Bilioni 20 kwa mwaka. Hata hivyo fedha hiyo ukishaipiga mafungu matano inaonekana haitoshi na haileti ufanisi uliokusudiwa. Tumeona mara nyingi Baraza linapohakiki utendaji wa vikosi hugundua changamoto na mapungufu kadha.

Kwa mfano, KMKM inakabiliwa na upungufu mkubwa wa vitendea kazi kama vile boti zenye uwezo mkubwa wa kufanya doria, vifaa vya mawasiliano, mafuta ya kutosha katika kazi za doria. Lakini kubwa zaidi hawana rada, ambayo ingeweza kumulika mipaka yetu yote ya nchi na kugundua kila kinachoingia katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, Kikosi cha Chuo cha Mafunzo wao ndio kabisa wamekwisha, Nyumba za kuekea wahalifu (wanafunzi) ni zile za toka enzi ya Hittler, mbovu zilizokosa hata huduma ya vyoo vya kujisaidia wanafunzi. Hivi tunakaa leo kujadili makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hii, Kamanda wa Mafunzo Pemba hana afisi ya kufanya shughuli zake amelazimika kuhamia katika *cell* za wafungwa na bajeti hii haina fungu la ujenzi wa nyumba ya kamanda.

Mhe. Mwenyekiti, hali ni hiyo hiyo ukitembelea JKU na vikosi vyengine, kumejaa mapungufu kadhaa na ndio maana kumbe vikosi vikawa vinajiingiza katika shughuli za kisiasa, kutokana na kukosa la kufanya huko makambini kwao.

Mimi ningeshauri kwamba, kwa kuwa mzigo wa vikosi umekuwa mkubwa kwa serikali na serikali imeonesha dalili ya kushindwa kuvipatia uwezo wa kufanya kazi. Ni vyema vikosi vikapunguzwa badala ya vitano sasa vikawa vitatu, ili kutoa nafasi kwa serikali kupata uwezo wa kuvikimu *(Makofi)*.

Shughuli za vikosi vitakavyopunguzwa zipelekwe kwenye wizara nyengine. Kwa mfano shughuli za kikosi cha zimamoto zihamishiwe katika ofisi ya Waziri kiongozi kwenye Idara ya Maafa. Kikosi cha Valantia kikabinafsishwa

na kikawa Taasisi ya kutoa huduma ya ulinzi kwa mtindo wa biashara *(Makofi)*.

Mhe. Mwenyekiti, nahisi wakati sasa umefika wa kuwa na Wizara yetu ya Ulinzi na Usalama, ili tuweze kuvihamishia vikosi vyetu huko na kuipunguzia wizara mzigo, kwani wizara hii inaonekana kuelemewa na majukumu mengi kutokana na wingi wa taasisi ilizonazo *(Makofi)*.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho kabisa naitakia nchi yetu amani na utulivu wakati wa Uchaguzi Mkuu. *Inshaallah* kwa angalau mwaka huu matekeo ya uchaguzi yatangazwe kwa majibu wa matakwa ya wananchi kupitia kura zao.
Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuniruhusu kusema haya machache kati ya mengi niliyokua nayo. Pia nawashukuru wajumbe wenzangu kwa kunisikiliza kwa makini na naamini wamefaidika sana na mchango wangu huu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha *(Makofi)*.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, sasa tuanze na michango yetu, isipokuwa tukumbushane tu kwamba muda wa kuchangia kwa makubaliano ni dakika 15. Lakini tutakuwa tukiangalia jinsi michango inavyokwenda.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. Awali ya yote ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Baraza lako tukufu kwa ajili ya kuchangia Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ mwaka 2010/2011.

Kwa kweli ninawapongeza Mhe. Waziri, Naibu Katibu Mkuu, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Maafisa Tawala wa Mikoa na Wilaya, Makatibu wa Halmashauri, Makamanda wetu wa Vikosi vyetu vya SMZ pamoja na wapiganaji. Nawapongeza sana na Mwenyezi Mungu awajaalie awape afya njema na waendelee na kazi zao *(Makofi)*.

Mhe. Mwenyekiti, nazingatia muda sana lakini ninayo mengi isipokuwa nitasema kwa ufupi. Kwanza nalishukuru Baraza la Manispaa la Zanzibar, kwa kazi zake nzuri wanazofanya na hivi sasa mji wetu kwa asilimia kubwa umebadilika. Kwa kweli hali hii ndio inayotakiwa hasa tukizingatia kwamba nchi yetu tunapokea wageni kutoka sehemu mbali mbali duniani.

Kwa hivyo, nalipongeza sana Baraza hili kwa kazi zake nzuri inazozifanya. Lakini pamoja na juhudi hizo napenda nimkumbushe Mhe. Waziri kuwa kuna mambo ambayo yamefanywa na wahisani. Kwa mfano, usafi wa mji wapo wenzetu ambao wametupa misaada yao ya magari pamoja na nyenzo mbali mbali.

Kwa maana hiyo, naomba tuhakikishe kwamba magari hayo tunayatumia vizuri kwa ajili ya kuzoa taka katika maeneo yote ya majaa, ili mji wetu uwe kwenye hali ya usafi na kuvutia.
Vile vile kuna suala jengine ambalo limetokea kwenye nchi yetu. Kwa hiyo, naishukuru sana wizara kupitia Manispaa kwa mitaro iliyojengwa kwenye maeneo yetu ambayo ilikuwa na adha kubwa wakati wa kipindi cha mvua za masika au vuli.
Maeneo ambayo yamebahatika kujengewa mitaro hiyo, basi naliomba sana Baraza la Manispaa lihakikishe kwamba usafi wa mitaro ile unafanya kila siku, ili kuiweka katika hali nzuri. Vile vile kuwapa taaluma wananchi juu ya tatizo la kutupa taka ovyo kwenye maeneo hayo.

Mhe. Mwenyekiti, naishukuru wizara kwa mvua hizi ambazo zilizonyesha katika eneo langu la Kwahani uwanja wa Farasi, pia ukitokea kwa marehemu Mzee Kassim Ali basi tumepata nafuu. Kwa hivyo, kwa niaba ya wananchi wangu naishukuru serikali kwa asilimia kubwa sana, kuwa adha iliyokuwa inatupata imepungua sana.

Kwa maana hiyo, ili tuweze kufanikiwa kumaliza tatizo hilo, basi naliomba sana Baraza la Manispaa kuongeza wafanyakazi katika maeneo hayo, kwa ajili ya kusafisha mitaro ile na kuwa kwenye hali ya usalama siku hadi siku.

Mhe. Mwenyekiti, wananchi wa Jimbo la Kwahani sehemu ya Soko la Mikunguni, wamenipa agizo ambalo ni muhimu sana kuhusiana na soko hili. Mwaka 1995 wakati nilipoingia kwenye Baraza hili nilitoa ahadi kwa wananchi wangu kwamba mambo matano nategemea kuyafanya, miongoni mwa hayo ni suala la ujenzi wa soko jipya, ambalo nililianzisha na limefanikiwa.

Kwa hiyo, azma ya wafanyabiashara pamoja na wananchi kwamba soko lile litumike kwa manufaa mazuri na kuweka bidhaa katika hali ya nzuri pamoja na usafi. Lakini kwa bahati mbaya yapo matatizo ya hapa na pale, ambapo watumiaji wa soko wanapiga kelele, kutokana na biashara zinazofanyika kiholela kwenye maeneo hayo imekuwa ni adha na soko lile halitumiki ipasavyo.

Kwa maana hiyo, wafanyabiashara ambao wamo ndani wanapata shida sana juu ya ulipaji wa ada. Kwa hiyo, namuomba sana Mhe. Waziri kupitia Baraza la Manispaa, waangalie utaratibu mzuri kuhusu ada ambayo wanayotoza kila mwezi, ili wananchi wangu wasishindwe kulitumia soko lile, vyenginevyo wafanyabiashara wanatoka ndani na kwenda njema na huko ni kwenda kinyume na usafi wa mji.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana Mhe. Waziri hili alione na lifanyiwe kazi, ili wananchi wetu wasilete manung'uniko juu ya serikali yao.

Suala la taa za barabarani ni muhimu sana pia ni nyenzo moja ya kuweka mandhari ya nzuri ya mji wetu, pamoja na kitabu hiki kimeelezwa kwamba katika maeneo ya Mji Mkongwe, Michenzani. Kwa kweli hili ni suala la kudumu kwa maeneo haya, lakini bado kuna matatizo kwa maeneo yetu ya ng'ambo.
Kwa mfano, ukitoka Mwembeladu mpaka Amani kiza hakuna taa, ukitoka Ng'ambo *Station* mpaka *roundabout* Mwanakwerekwe, ambapo naamini ile njia mpya inayojengwa baadaye itawekwa taa. Lakini sijui kama zipo kwa sababu sijaona alama za waya au nguzo, kwa ajili ya kuonesha kwamba maendelo mapya yanakuja.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri haya maeneo yaendelee kama yalivyopangwa, kwa ajili ya kuleta ufanisi, mji wetu kuung'arisha pamoja na kuuweka katika hali ya usalama. Kwa sababu taa za barabara zina mambo mengine yakiwemo usalama pamoja na kumfahamisha mtu kile ambacho kinachotokea mbele yake anakiona.

Suala jengine ambalo nataka kulizungumza ni kuhusu bustani zetu za kupumzikia zikiwemo *Forodhani Pack Jamhuri Garden*. Hivi sasa bustani ya Jamhuri iko mbioni katika kutengenezwa upya na kuiweka kwenye mandhari nzuri. Kwa kweli watoto wengi siku hizi wanafurahika kutokana na vifaa mbali mbali vya michezo ambavyo vipo.

Kwa hivyo, naomba Baraza la Manispaa liongeze kasi kwa ajili ya kulifanya eneo kuwa zuri, ambalo litavutia hasa tukizingatia hapa ni kati ya mji wetu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa *Forodhani Pack* hali inaendelea kuwa nzuri, isipokuwa wananchi wanacho kilio ambacho nataka nikiseme. Kuhusu suala la ada ya *parking* ambayo hukusanywa kwa siku nzima, lakini kuanzia kama saa 3 au 4 za usiku kwenye maeneo bado watu wanaendelea kukusanya fedha hizi zinakwenda wapi. Tukizingatia kwamba ada zote zinatakiwa zikusanywe wakati wa kazi na fedha ikabidhiwe sehemu maalum yenye usalama. Je, fedha hizi wanaruhusika kuzichukua nyumbani na usalama wa fedha hizo uko wapi.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, wakati atakapokuja kufanya majumuisho atueleze, ili wananchi waliotutuma na wao wasikie.

Mhe. Mwenyekiti, Vikosi vya SMZ kila siku husema kwamba ninavipongeza kwa moyo wangu wote. Namuomba sana Mhe. Waziri pamoja na serikali kwa

jumla kwamba iwaongezee uwezo pamoja na nyenzo, kwa sababu bila ya vikosi hivi usalama wetu haupo. Kwa mfano, yapo maeneo mengi ambayo wanastahiki kufanyakazi wenzetu hawa, baadhi ya wakati wanashindwa kutokana na ukosefu wa vifaa.

Kwa maana hiyo, tukiangalia Kikosi chetu cha KMKM hivi sasa dunia imeharibika kutokana na uharamia uliojitokeza. Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana Mhe. Waziri kupitia serikali yetu tufanye kila jitihada za kupata vifaa vya kisasa kwenye boti zetu pamoja na mafuta ya kutosha, kwa ajili ya kuweza kufanyakazi katika hali ya usalama na hasa wakati wanapoingia kwenye maeneo ya bahari kuu.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana Mhe. Waziri suala hili aliangalie pamoja na kulifanyiakazi, kwa sababu maaskari wetu wanategemea usalama wao kutokana na dhana wanazotumia katika utendaji wa kazi zao.

Kwa kweli wenzetu hawa wanafanyakazi ngumu, kwa sababu askari kazi zake ni nguvu. Kwa hiyo, nimuombe Mhe. Waziri kama kuna masuala ya marupurupu au motisha basi wapatiwe, kwa sababu wenzetu hawa wanajali na wanafanyakazi katika mazingira magumu kama vile wakati wa mvua, jua, mchana na hata usiku.

Hata hivyo, niwapongeze Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa wote wa Unguja na Pemba. Nianze na Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja, kwa kweli nampongeza sana, kwa sababu mwenye kufanya vizuri lazima apongezwe yaani haki yake. Kwa hivyo, Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja ameanzisha afisi yake ambayo ni nzuri na tunategemea Mwenyezi Mungu akitulaalia itafunguliwa kabla ya kumaliza muda wetu huu *(Makofi)*.

Vile vile nampongeza kwa nguvu alizowapa Wakuu wa Wilaya ya Kusini na Wilaya ya Kati kwa kujenga asfi nzuri na kazi zake nzuri pamoja na Halmashauri ya Wilaya ya Kati, Halmashauri ya Kusini. Kwa hiyo, tunawapongeza wote kwa kuanzisha afisi zao nzuri ambazo zinapendeza.

Pamoja na kuona kwenye kitabu hiki kwamba zimewekwa fedha kwa ajili ya kuanza kujenga jengo jipya la afisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi. Mhe. Mwenyekiti, afisi yetu ya Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi ni aibu tuwe wazi tena mimi naona aibu sana, kwa sababu tunatembea sehemu za wenzetu. Kwa mfano, tunakwenda kwenye afisi nafasi ya kuweka gari kumi hapana.

Kwa hivyo, nadhani tubadilike huu ni mji na tunalo eneo letu kubwa pale Amani nimeona kitabu kimegusia. Lakini ilikuwa ndani ya miaka kumi hii

angalau tungepata ghorofa moja. Kwa hivyo, naiomba serikali tumuangalie Mkuu wa Mkoa wa Mji Magharibi, kwa sababu anapokea wageni mbali mbali kutoka duniani ambao ni mashuhuri, labda kinachovutia ni Mji Mkongwe, kwa upande wa afisi hasa haifai.

Mhe. Mwenyekiti, naomba suala hili litiliwe mkazo, ili afisi ile ijengwe kwa lengo la kuweka mazingira yetu katika hali nzuri *(Makofi)*.

Mhe. Mwenyekiti, pia Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja naye tunampongeza na Halmashauri zote tunazipongeza kwa kazi zao nzuri pamoja na afisi zao na walichoomba wapewe.

Vile vile tunazo Halmashauri zetu zikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Kati, kwa kipindi kifupi hiki nami niungane na wenzangu kwamba Katibu wa Halmashauri hiyo ameonesha mfano mzuri. Mhe. Mwenyekiti kila siku husema kuiga mazuri si vibaya, kwa sababu kuiga mazuri ni sahihi.

Kwa kweli Katibu wetu huyu wa Halmashauri ya Wilaya ya Kati ameonesha mfano mzuri, kwani amepindukia lengo kwenye bajeti hii na bajeti ya mwaka 2010/2011 ataongeza zaidi. Kwa hivyo, huu ni mfano mzuri, utekelezaji wake pamoja na mipango yake yote ameipanga vizuri. Basi ninampongeza sana kwa hili *(Makofi)*.

Mhe. Mwenyekiti, pia wapo wengine ambao wamepanga mipango yao mizuri, nawapongeza kama nilivyotanguliza pongezi za mwanzo na wala sina matatizo nao. Kwa kweli nataka nipate maelezo kidogo kuhusu Halmashauri ya Wilaya ya Kati, imesema kwamba inataka kuweka mtandao mpya katika maeneo, kwa sababu walianza Uroa, Pongwe Pwani pamoja na Marumbi kama sikosei.

Kwa hivyo, naomba kuulimuza Mhe. Waziri huu umeme utakao wekwa kwenye zile taa za mitaani watalipa wananchi au Halmashauri, kwa sababu hapa pasijekuwa na kitandawili taa zile siku mbili au tatu zikashindikana. Kwa kweli napongeza sana mpango huo, kwani tunategemea kwamba taa hizi ni nuru na mwangaza wa usalama katika maeneo yetu.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ambalo nitalizungumza kwa ufupi kabisa. Katika maendeleo ya nchi yoyote kuna mipango ya uendelezaji wa muda mrefu. Kwa kipindi hiki Wizara ya Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ imeshughulikia mambo mengi ya maendeleo kwa ufanisi kwa ajili ya kuleta maendeleo katika sehemu tofauti, yaani mjini na vijijini.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kwa kuwa baadhi ya maeneo kuna upungufu wa wafanyakazi, ambao unatokana na uwezo mdogo wa fedha. Mhe.

Mwenyekiti, namuomba afanye njia zozote zile pamoja na kushirikiana na wenzake wanaomsaidia, kwa ajili ya kupunguza au kuondosha kabisa tatizo hilo, kwa ajili ya kuongeza juhudi katika utendaji wa kazi zetu.

Mhe. Mwenyekiti, ninachokumbuka kitu kikubwa kilichokuwepo kwa wizara hii ni kwamba hukusanya mambo mengi. Kwa mfano, kazi ya ukataji wa majani barabarani, kwa sababu najua Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi wanashirikiana na wenzetu hawa wa Wizara ya Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ, kwa lengo la kuweka mazingira mazuri.

Pamoja na hayo, kwamba hali hii inaendelea vizuri katika maeneo mbali mbali ya barabara zetu yanafanyiwa kazi. Lakini ninamuomba sana Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, ikiwa atapata muda baada ya kumaliza bajeti yake, kama ataelekea Matemwe siku moja basi apitie Kiwengwa na aanzie Kipandoni mpaka afikie Mchekeni chini, maana hivi juzi kumetokezea ajali mbali kutokana na hali ya kutokuona mbele kinakuja nini. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri miti hii ifanyiwe kazi, kwa ajili ya kuepusha matatizo ambayo yanayoweza kutokea.

Mhe. Mwenyekiti, jambo la mwisho naomba niseme kwamba, idara zote za wizara hii nazipongeza pamoja na kuziunga mkono kutokana na maendeleo yao. Vile vile nawaombea heri kwa Mwenyezi Mungu kila walichokitaka wapate kwa ajili ya kuleta ufanisi kwa wizara hii (*Makofi).*

Baada ya hayo, naunga mkono bajeti ya wizara hii kwa asilimia moja pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Kwahani. Ahsante sana *(Makofi).*

Mhe. Omar Ali Jadi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kuweza kunipatia nafasi hii ya pili kwa ajili ya kutoa mawazo yako kuhusiana na wizara hii.

Nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia kuwa mzima wa afya na kusimama hapa, kwa lengo la kushirikiana na wenzako katika kutekeleza majukumu yetu ya kazi.

Vile vile nimpongeze Mhe. Abdalla Juma Abdalla (Waziri Kivuli wa Wizara ya Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ), kama ingekuwa uchangiaji si kila mtu na mawazo yake, basi ningesema yale aliyosema yanatosha. Lakini kwa kuwa na mimi ninayo haki ya kutoa mawazo yangu, basi niendelee kutoa mawazo yangu *(Makofi).*

Pamoja na hayo, nimpongeze Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ pamoja na watendaji wake, kwa jinsi ambavyo wamefinya

finya na kuweza kuficha ficha yale makucha yao, ili wajumbe tusifahamu yale yaliyofanywa.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye Wilaya Ndogo Kojani, katika mwaka 2009/2010 nilitoa masikitiko yangu kwa bahati nzuri Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ilipata muda wa kwenda kufanya tathmini ambayo niliieleza na kuona upungufu uliopo.
Kwa kweli yale ni masikitiko kuona fedha za serikali zinachezewa na watu wachache wasiopenda maendeleo ya nchi hii. Kwa mfano, Mhe. Abdalla Juma Abdalla (Waziri Kivuli) alisema haridhiki na mtu yule sijui alikuwa mkandarasi wa ujenzi alifanywa nini.

Lakini nathubutu kusema kila tukiangalia wakandarasi wa sehemu yoyote. Basi hatuangalii vipaji vyao pamoja na taaluma zao za kusimamia ujenzi, isipokuwa tunaangalia sura pamoja na familia katika shughuli hizi. Mhe. Mwenyekiti, kama hivyo sivyo basi tusingekubali kujengewa ujenzi kama ule, kwa sababu tokea mwaka juzi na mwaka jana nimekikataa kifungu kile kutokana na ujenzi wa afisi ile hailingani.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ni mhusika ingawa wengine wanasema sitembelei Kojani, lakini pale ninalo shamba langu la minazi nalima. Kwa hivyo, kila kinachofanyika ninakifahamu. Kwa hiyo, muomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, wakati atakapokuja kufanya majumuisho anipatie ufafanuzi kuhusiana na suala hili.

Nikiondoka hapo niende sehemu za Madiwani. Mhe. Mwenyekiti, madiwani wameshindwa kufanyakazi zao ipasavyo kutokana na maelezo yalivyo. Katika kitabu hiki kinatuelekeza kazi za madiwani pamoja na kusimamia mazao. Lakini ukifika kwenye maeneo baada ya leseni huna kazi nyengine ya kufanya.

Naomba niungane na Mhe. Abdalla Juma Abdalla (Waziri Kivuli) ni vyema Mhe. Waziri akafuatilia suala hili na kutoa hasa utaratibu na ilani za mipaka ya kazi za Madiwani na Masheha, ili tuweze kuishi kwa usalama na kwenda katika ustaarab mzuri, kwa ajili ya kuzuia mapato ya serikali yasipotee.

Lakini uwiano unapokuwa mkubwa wa kazi, hata mapato yanaweza kupotea. Kwa hivyo, ninaimani Mhe. Waziri kwa sababu ni msikivu anaweza kulifuatilia na kupata jawabu kuhusu kazi za madiwani na masheha.

Mhe. Mwenyekiti, suala la jengine kuhusu Baraza la Manispaa la Zanzibar. Kwa kweli kuhusiana na Baraza hili ninatoa ushauri kuhusiana na wale wanaosimamia mapato ya wafanyabiashara wadogo wadogo. Kwa mfano, wakati wa jioni utawaona wafanyabiashara wale wanakwenda mbio, kweli

maeneo yale wanakatazwa kufanya biashara, lakini ndimo kwenye mapato yao na biashara huwezi kuuza mwituni.

Nadhani ni vyema wakaandaliwa utaratibu mzuri wa kuweza kutozwa kodi ndogo ikiwa ni njia moja ya mapato ya serikali na wale wakaachiwa kuendelea na kufanyabiashara zao, kwa ajili ya kujipatia riziki pamoja na watoto wao, vyenginevyo ni kuwasumbua na kuwatia umasikini. Kwa mfano, unaweza kumuona muuza samaki amewatengeneza vizuri samaki kwenye gari ambayo ni safi na wala maji hayamwagiki chini.

Lakini hatima yake kwenye saa 11 jioni anachukuliwa pamoja na mkokoteni wake na akifika kule faini ni shilingi 60,000/- au 70,000/- wakati huo mradi wake ni shilingi 20,000/-. Matokeo yake mradi wote unakwenda pamoja na kutafuta chengine cha kuongezea na hali hii inazisisha umasikini.

Mhe. Mwenyekiti, azma ya serikali yetu hii ni imani kwa wananchi pamoja na kuwanyanyua katika nyanja zao. Kwa hivyo, tungefuatilia kwenye utaratibu wa Serikali Kuu, ili wananchi wale tukawawekea utaratibu wa sehemu pamoja na makato yao pale mtu anapokamatwa na wala sio kumkandamizi au kumuua kabisa katika miradi yake.

Nikiendelea na mchango wangu Mhe. Mwenyekiti, nizungumze kwenye Kikosi changu cha KMKM ambacho mara nyingi niko karibu nacho. Kwa kweli kila mtu anao utaratibu wake pamoja na uongozi wake. Lakini nathubutu kusema kikosi kile ambacho kiko katika jimbo langu, hata mtu awe ni katili kiasi gani, basi akifika pale huwa ni sharifu sijui kama wanapewa mafunzo au dua maalum ama kuna mambo gani yanafanyika, isipokuwa ni watu wa kupigiwa mfano katika vikosi pamoja na kazi zaop nzuri *(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti, naiomba wizara kuwaangalia kwa vitendeakazi, kwa sababu tunawapa kazi ngumu lakini vitendeakazi hatuwapi na huku ni kuwaonea, yaani ni kutowatendea haki kikosi kile. Kwa mfano, Kikosi kilichopo Msuka cha KMKM, labda vespa iwe na mtu maalum lakini hakuna kipando, ikiwa askari atatokewa na dharura askari basi sijui afanye nini.

Hivi juzi wakati wa kipindi cha Maswali na Majibu, kuna Mhe. Mjumbe mmoja aliuliza kuhusu maharamia ambao walitaka kuvamia meli, baada ya kufukuzwa basi walifanya kuelekea huku na kutaka kukishambulia kituo na askari wale hawana vifaa vya kujikinga au kujihami. Hatima yake wakikaribia juu ni kukimbia kituo na kukimbia kituo kama kile, maana yake tumeshindwa.

Mhe. Mwenyekiti, naiomba serikali kupitia wizara hii tusiwasifu kwa kazi na tuwasifu kwa kuwapa vitendeakazi, yaani tuwape moyo. Kwa mfano,

tukiangalia kikosi changu ambacho kipo pale Bandari ya Kojani kuna bahari kuu mara moja maharamia wakifukuzwa wanaweza kuingia pale bahari ndogo ya juu, askari wale hata kile kidau kidogo hawana unaweza kuja kuwafukuza kazi kwa sababu wamepita maharamia wameshindwa kuwashambulia kumbe hawana chochote.

Katika bajeti hii Mhe. Waziri ameshafanya vifungu vyake lakini kwa uwezo wake Mungu kama tutakuwa hai na nitakuwa mjumbe tena wa baraza hili, nina imani sana kwa uwezo wake Mwenyezi Mungu nitakuwa tena basi kikosi hiki kuja hapa kukipangia maharage kilo moja bila ya kuwapa vitendea kazi vya ukweli hatutoridhiana. Jamani tuwaheshimuni sio tunawafanyia kazi lakini kuwaendeleza tunashindwa, nina imani katika kikosi kile pale Pemba gari yao ipo pale Makao Mkuu Wete tu basi, lakini vituo vyote vilivyobakia pale havina usafiri tuwatendee haki jamani tuwaoneeni imani askari hawa, mtu ambae unamuweka katika kituo kwa mwezi mmoja au miwili hajaonana na wanawe ni kazi, lakini kitendea kazi hata kimoja hana apate baskeli ya kuazima au kwa mguu.

Mimi ningeomba Mhe. Mwenyekiti, tulishauriana kuhusu masuala ya umeme *alhamdullilahi* umefika sasa hivi leo wanaangalia kombe la dunia pale pale kituoni pao, basi ni vyema vituo kama vile havipatiwi gari japo tuchangishane mimi na wewe mimi muwakilishi na wewe Waziri tuwapatie angalau usafiri mdogo mdogo, lakini tunamuona mkuu wa kituo pale anatoka kwa mguu masikini aibu kama haiwezekani kupatiwa gari basi japo vespa tuchangizane lakini tuwapatie usafiri mdogo mdogo wale.

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka hapo niende katika Halmashauri ya Wilaya yangu ya Wete hapa mimi nina masikitiko sijui nieleze kama yale ambayo Mhe. Abubakar Khamis alisema juzi kwamba kompyuta ilisahau kuandika au vipi sijui? Halmashauri hii kwa kweli imenisikitisha kidogo mwaka jana nilikuwa niseme lakini nikasema aa tuiwacheni, lakini mwaka huu naona unapotumia fedha za Halmashauri unatakiwa kuziidhinisha kama nimetumia hivi, na unapotumia shilingi kumi basi uidhinishe kwamba shilingi kumi sio kwamba umetumia kumi uandike hamsini ni *wrong*.

Mimi naelewa kuna mradi mmoja ambao kuwa juzi juzi umepokewa kwenye wadi yangu ya Kojani hapa sijauona sijui kama watu wamesahau, au mashine imekosea katika kujengwa vyoo Kojani naona ni laki nne na ishirini kilichopatikana ni kikubwa zaidi nasema kwa awamu hii, kilichopatikana awamu ya mwaka juzi 2009/2010 kilikuwa ni kidogo lakini matumizi yakawa makubwa! Lakini mara hii kilichopokewa ni kikubwa lakini matumizi ni madogo. Hapa Mhe. Waziri ukija nataka nielezwe hawa walisahau kuchapa au

walikosa kupeleka mahesabu au vipi? Saruji pakiti zaidi ya sitini kuweza kuandikwa shilingi laki nne na ishirini.

Sisi tunataka tupate maelezo pengine binaadam tu wamekosea, bahati nzuri katika halmashauri hii hii niende katika miradi ya mwaka 2010/2011 nashukuru katika upangaji wake utaratibu kusaidia angalau na mimi jimbo langu limebahatika kuingizwa japo skuli moja mungu atujaalie mafanikio pesa hizi ziingizwe na miradi ifanyike.

Lakini kuna jina moja kidogo limenipa utata nataka nielewe tu jina hili pengine kwa sababu ya ushamba sana au sijatembea sana nieleze jina la skuli hii. Skuli ya Ukoto maana kule Pemba tulikuwa na jamaa mmoja akiuza duka kwa Mshihiri mmoja akiitwa Mbaraka alikuja akaona pesa nyingi sana na kwa sababu hazielewi akamwambia tajiri wake kwamba pesa hizi umezisahau, *wowo kuziokoto*, sasa isijekuwa jina lile limetumiwa kwa skuli ikawa ni mifano. Sasa nataka nielewe tu skuli hii ipo katika kijiji gani na maendo gani. Kuna Kokota mbali na Okoto maana usije kusema Kokota lakini kuna Kokota mbali na Okoto, sasa nataka nifahamu iko katika kijiji gani na maeneo gani?

Lakini Mhe. Mwenyekiti nikitoka hapo bahati nzuri nipongeze Wizara katika kupitia bajeti lake la Mji la Wete kuweza kufanikisha machinjio ya ng'ombe yaliyokuweko Wete kuwaza kuyakarabati vizuri na leo likawa katika hali nzuri kidogo yangaliko, lakini bado kukarabatiwa kweke usafi bado haujafanya kazi. Ningeomba basi Baraza la Mji la Wete kama usafi wake pale chini panatowekwa wale ng'ombe kuchinjwa basi ungesafishwa zaidi kwa sababu ukarabati wa jengo na usafi wa pale mazingira zaidi ni yale ya usafi.

Lakini Mhe. Mwenyekiti kwa kulinda muda wako niende katika Idara ya Vitambulisho vya Uzanzibar Mkaazi.

Mhe. Mwenyekiti: Nakuomba umalizie.

Mhe. Omar Ali Jadi: Na mimi hiyo ndio namalizia hoja yangu Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli idara hii nina masikitiko makubwa Mhe. Waziri Kivuli wangu katoa mifano ya Mhe. Spika, lakini Mhe. Spika, inaonyesha pengine ni mzee lakini na mvi kuja haraka kabla ya uzee. Lakini cha kusikitisha zaidi hapa anaipataje haki mjukuu lakini babu ikawa hana haki na ndie aliyemzaa baba yake au mama yake na Akaka pale pale nchi hii, leo mtu wa miaka thamanini mpaka tisini mimi nina mjomba wangu anafika miaka 121 mpaka 130 sasa hivi, juzi amekosa kuandikishwa kwa sababu hana cheti cha kuzaliwa!

Mjomba huyo amewazaa dada zangu, kaka zangu na wengineo mpaka kufikia mimi ambae kuwa karibu ya mjukuu wake, mimi nikapata haki wakati kanizaa

akiwa pale pale, kawazaa wote yeye hajaondoka lakini akakosa haki kwa sababu hana cheti cha kuzaliwa, kafika kutuzaa sisi jamani apate cheti gani tena? Hili ni kutowatendea haki wale ambao wako katika maeneo yale.

Mhe. Mwenyekiti bahati nzuri wananchi wetu kwa sababu sheria inaeleza wazi raia wowote ambae ana sifa na ameshafikia umri wa miaka kumi na nane kuwa na kitambulisho za Mzanzibari mkaazi ni haki yake, sasa labda pengine zielezwe taratibu gani kwa sababu pengine ameshakuwa mzee sana unaweza kuelemea mwanao tu japo siye kwa hivyo sheria haikuruhusu anatakiwa kijana mwenye akili timamu ambae kuwa bado hazijababaika akili zake.

Lakini kama ni kila Mzanzibari Mkaazi ambae kuwa maeneo yale ni mzaliwa na bado hajapoteza akili bado anazo basi ni vyema ingeangaliwa ili tusiwaache wananchi wakavunja sheria wakati sheria ipo wazi, sheria inasema yoyote asiyekuwa na kitambulisho hichi na ameshafika umri na ana sifa basi ni kosa la jinai kwa nini tuwatie matatizoni wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti nina masikitiko zaidi najua muda wako tayari umeshamaliza ni kuwa kuna sentensi moja inanitia wasi wasi, kuna sehemu ambayo kuwa inasema katika kutekeleza majukumu yake ya vitambulisho ni kwamba kutakuwa na vitambulisho maalum vya wageni. Sasa hapa nataka nipate ufafanuzi. Vitambulisho hivi maalum wageni hawa watakaopewa ambao kuwa watafanya kazi za serikali wataweza kupiga kura hapa wakati sio wazaliwa au ni vitambulisho vya aina gani?

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu ya muda wako tayari umeshapotea nikipata majibu hayo basi sina matatizo naweza kumuunga mkono Waziri katika hotuba yake, lakini kwa kupata majibu ya kuridhisha . Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti; Waheshimiwa wajumbe nakuombeni ninaposema tuchunge muda tukubaliane, tuchunge muda tafadhalini sana vyenginevyo itakuwa kikao hakiendi kama tulivyokubaliana kiende.

Mhe. Said Ali Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi kuchangia machache sana katika hotuba ya bajeti ya *swahibu* wangu sana miongoni mwa mawaziri wa serikali hii, naomba nianze pale alipomalizia Mhe. Omar Ali Jadi kuhusu suala la vitambulisho.

Mhe. Mwenyekiti idara hii ni muhimu sana katika nchi na kwa umuhimu wake na utekelezaji wake wa kazi lazima nao wawe na uadilifu mkubwa vyenginevyo umuhimu wake utakuwa hauna maana hata kidogo, sasa kelele hizi zinazopigwa kunaonekana kuna tatizo ndani ya Idara hii na kwa kweli sio busara kuzipuuza hata kidogo haiwezekani kuwe hakuna tatizo watu wazima na

akili zao walalamike tu . Idara hii imekuwa ikilalamikiwa sana sasa kwa sababu inalalamikiwa, Mhe. Waziri hapaswi kupuuza malalamiko haya lazima ayaangalie na ayatafutie dawa.

Sasa mimi ningesema kwamba tatizo kubwa ambalo naliona mimi ni upatikanaji wa vitambulisho vyenyewe umekuwa na matatizo makubwa, mimi ninavyoona tatizo sio Idara yenyewe katika hili lakini tatizo ni Waziri mwenyewe. Baraza hili lilitunga sheria kuhusu vitambulisho sasa Waziri kaiteka nyara sheria ya vitambulisho ametumbukiza kanuni halafu ame *in power* ile kanuni kuwa na maana zaidi kuliko sheria yenyewe, sasa ndio tatizo kubwa hilo. Mkurugenzi sasa yeye anaangalia kanuni ya Waziri inayohusiana na cheti cha kuzaliwa hapo tu sasa hili sio tatizo la Mkurugenzi na Afisi yake, ni tatizo la *swahibu* wangu Waziri kwamba ameiteka nyara sheria ameingiza neno cheti cha kuzaliwa sheria haina hilo, sheria tuliyopitisha hapa haitaji hata kidogo cheti cha kuzaliwa.

Sasa Waziri ametumbukiza hii cheti cha kuzaliwa na Mkurugenzi anaburutwa na kanuni sheria inakaa kando, sasa mimi nimesema mara nyingi kwamba kanuni inapovuka nguvu za sheria hiyo kanuni ni badili, sasa bado tunasema kwamba suala hili ndio msingi wa tatizo kubwa na bahati mbaya cheti cha kuzaliwa nacho kupatikana kwake mtihani watu wengine hawajapata vyeti vya kuzaliwa tokea wazaliwe, ili upate kanuni ya Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Katiba na Utawala Bora ili uipate uwe na shilingi zaidi ya thalathini elfu. Mtu wangu wa Gando ana watoto watatu au watano ndani ya nyumba thalathini elfu mara tano ni laki moja na nusu atoe, ameuza ndizi mwaka mzima hajapata hiyo hawezi kushughulikia mambo mengine akasema hii nakwenda kushughulikia mambo ya vitambulisho.

Sasa kanuni nyengine ya Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Katiba na Utawala Bora ya kulazimisha kuwa awe na cheti cha kuzaliwa lazima atoe hizo pesa nyingi nalo ni tatizo, mara nyingi tulikuwa tukizungumza kwamba kanuni zinazotungwa imekuwa bodi zikapita kwenye Baraza hili kwanza ili zikatiwa baraka, au kwenye kamati zake ili zisikwamishe zile sheria ambazo tumezitunga. Sasa nasema kwamba hilo ni tatizo kubwa na ambalo kanuni hizi zimewafanya watu wetu wengi wakose haki zao.

Mhe. Mwenyekiti juzi mimi nimeandikisha kupiga kura Pemba Zanzibar katika jimbo langu la Gando, zaidi ya watu elfu moja ambao hawakuwa na vyeti vya kuzaliwa na kwa hivyo hawakuwa na vitambulisho wameandikishwa ambao ZEC hawakuandikishwa kwa sababu ya dudu hili la cheti cha kuzaliwa ambalo Mhe. Waziri ameliweka. Na zaidi elfu moja hawa walioandikishwa wale wenye asili ya bara ni kumi na mbili tu sasa hili ni tatizo ambalo nasema kwamba lishughulikiwe, mara moja nilikaa na Mkuu wangu wa Wilaya pale na

Mkurugenzi wa vitambulisho tukalizungumza hili ukweli Mkurugenzi akakubali kulichukua na kulifanyia kazi lakini mpaka leo naona kimya ni jambo ambalo linahitaji kushughulikiwa.

Jambo jengine ambalo nimeliona katika Afisi ya Vitambulisho ni bajeti yake ya mwaka huu, mwama jana bajeti yake ya kawaida ilikuwa ni shilingi milioni mia tatu na sabiini na moja bajeti ya kawaida. Mara hii Waziri anaomba milioni mia nane ni nyingi kutoka milioni mia tatu sabiini na moja zimechupa mpaka milioni mia nane sasa bajeti ya kawaida ni mishahara na *other charges.* Sasa labda Mhe. Waziri aje anishawishi labda anataka kuajiri watu wengine zaidi au wanataka kununua nini humu mna *other charges* na mambo mengine madogo mdogo, sasa hapa kunataka kufanywa jambo gani la maana ambalo limechupisha bajeti ya kawaida ya vitambulisho kiasi hiki naomba maelezo hii Wizara mimi sitaki kuitia mdomo sana kwa uzoefu wa watendaji wake isipokuwa Waziri kidogo amenitia tafrani katika hii kanuni yake.

Lakini hapo hapo pia kuna fungu la takrima ambalo limeanzwa katika bajeti kuu na lionja kidigo hapa nitalimalizia kwenye Wizara ya Fedha na Uchumi, limewekewa 2. 22 milioni sio jambo la kawaida. Sasa jibu la Mhe. Waziri wa Fedha alipokuwa anajibu bajeti kuu sikulifahamu sasa ilivyokuwa mwenyewe yupo leo na ndiye anayeniomba niruhusu matumizi haya naomba maelezo ya uhakika, imekuwaje hili fungu likawa na fedha nyingi namna hii, nimeangalia mafungu yote ya takrima hili kubwa Mhe. Mwenyekiti hakuna fungu isipokuwa kifungu kimoja ambacho sipendi kutaja kwa nini nayo ikawa na fungu kubwa hilo tu naogopa kwa uzoefu wake hiyo idara hiyo. Lakini hii ndio ya pili ambayo ina fedha nyingi sana katika takrima sasa naomba maelezo ya Mhe. Waziri kwa nini hili fungu likawa hivi?

Jengine ambalo napenda nilizungumze Mhe. Mwenyekiti na mimi ni vikosi, vikosi vina umuhimu wake katika nchi yetu jambo ambalo mimi sifahamu ni namna ambavyo vinapangiwa kazi, mfano KMKM ni kikosi muhimu sana kwa uzoefu wa nchi yetu na bahari lakini mfano mwaka huu imeomba zaidi ya *sixty bilioni* kutumia, sasa hizi kwa uchumi wetu ni pesa nyingi sana wanachokifanya ni kipi wakati ambapo watu wanatuibia samaki ovyo ovyo huko nje mabilioni ya pesa yanapotea kila siku? Tunaambiwa mameli yanaranda na kuiba samaki tuna kikosi hiki muhimu lakini sasa kinatumia pesa nyingi kinakaa kwenye fukwe tu hawaendi kule ambako wezi wanatuibia, sasa hapa hakijapangiwa kazi za msingi ambazo zingeweza kuisaidia nchi yetu. Wangeweza kutumia bilioni mbili au bilioni nne kwa kutafutiwa zana wakenda kuwafukuza wezi ambao wanatuibia rasilimali yetu. Nasema ni kikosi muhimu lakini hakijapangiwa mambo ya maana ya kufanya.

JKU inatumia zaidi ya 4.5 bilioni kikosi ambacho uchumi wetu mbaya sasa kama tumeweka nia ya kujenga uchumi tuangalie 4.5 bilioni ambazo Mhe. Waziri anatwambia tumpitishie zitarudi vipi na zitaweka misingi gani ya kujenga uchumi, haya ndio majibu ambayo tungeweza kuyaangalia.

Kikosi cha Valantia kinahitaji 2 bilioni ni pesa nyingi kuna idara nyengine muhimu hapa zinakuwa *allocated three hundred million* mfano tulikuwa tunazungumza juzi na jana Idara ya Kinga, Idara ya Sekondari 150 milioni kwa mwaka. Lakini Valantia 2.8 bilioni pesa nyingi sana sasa unapozifanyia *evaluation* hizi pesa Mhe. Mwenyekiti ilikuwa tuambiwe kwamba sasa pesa hizi ambazo Valantia *ame- allocated* nchi inavuna nini ,ni *product* gani nchi inategemea kupata? Sasa mimi ningeshauri kwamba ipangiwe basi majukumu Mhe. Waziri amesema ibinafsishwe ningekubaliana nae lakini kama hatukona hilo basi tukubaliane na tukipangie majukumu kiwe kama *local* polisi ya nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti kuna nchi nyengine zinazoungana kuna *federal police na local police* sasa katika mazingira ya nchi yetu wacha wale polisi wa Said Mwema wawe kama ni *union police* wafanye kazi zao na hawa wawe ni *local police* wa Zanzibar, lakini kuchukua 2.8 bilioni hazina matumizi wala hakuna mipango ukweli ni kupoteza *resorce* chache ambazo tunazo.

Kikosi chengine muhimu sana ni Zimamoto mwaka jana ni kikosi pekee ambacho kilipunguziwa bajeti sijui kwa nini wakati ni kikosi muhimu sana, vikosi vyengine vyote ukiangalia bajeti zao zimepanda baina ya asilimia 2,3,4,5 lakini hii bajeti yao imepungua. Kikosi ambacho kila mmoja hapa akisikia kwake kuna moto, roho yake imeshamrufai lakini bajeti yao inapunguzwa, mimi nadhani hichi ni kikosi ambacho kingeweza kuwekewa bajeti kubwa zaidi kama alivyosema Mhe. Waziri Kivuli kikosi hichi kingehamishiwa Afisi ya Waziri Kiongozi kwenye Idara ya Maafa ingelikuwa jambo la maana sana. Juzi moja nilikuwa bandarini ikaungua meli ya Serengeti muda wa saa moja haijafika poti ya kuzima ni mtihani mkubwa, sasa bado tunahitaji sana kukiimarisha hiki kikosi kama kweli tuna nia ya kuimarisha masuala yanayohusiana na maafa.

Jambo jengine ambalo nilizungumzie katika vikosi hivi kwa jumla ni suala la mafungu yao Pemba tulikubaliana hapa kwamba taasisi nyingi kuwe na vocher la jumla na kuwe na *sub vocher* Pemba, hizi zinaruhusu Wizara ya Fedha na Uchumi kutoa pesa moja kwa moja kutoka Hazina kwenda katika Afisi zao Pemba ili waweze kutekeleza majukumu yao, bahati mbaya sana vikosi vyote havina *sub vocher* Pemba, matokezeo yake zile afisi zinadumaa kimatumizi, wakubwa wakishatumiwa pesa hapa hufanya mambo yao ambayo yana *priority* halafu ndio huwapelekea pesa chache sana ambazo zinawafanya wakuu wa

kule kuwa na matatizo makubwa sana ya matumizi na kuendesha kazi. Sasa hii ni kasoro kubwa. Tulikubaliana kwamba taasisi kama ipo Pemba iwe na *sub vocher* ili watu wa Wizara ya Fedha wa Hazina waweze kuingiza pesa moja kwa moja kwa wakubwa watakaokuwa na mamlaka ya matumizi Pemba, sasa hili ni tatizo kubwa la vikosi vyote kwa jumla hazina na hili naomba maelezo ya Mhe. Waziri.

Mhe. Mwenyekiti eneo jengine ambalo naomba nizungumze ni madiwani hili ni kilio cha siku nyingi, *reform ya local government* imechelewa sana na kwa kweli inawasononesha sana madiwani, tatizo lao la malipo ni jambo ambalo tunalizungumza siku nyingi haiwezekani kwamba sisi tumechaguliwa kwa pamoja Rais wa Zanzibar, Mwakilishi na Diwani. Rais wa Zanzibar na Mwakilishi wanakula mshahara lakini Diwani yeye kila siku anakuwa hana kitu hili jambo halipendezi. Mhe. Mwenyekiti lazima *reform* ziletwe na lazima ziwe na kipengele cha malipo ya madiwani, lakini hata hawa Masheha nao pamoja na kuwatumia sana wanafanya kazi kubwa wanatumika anavyotaka Mkuu wa Mkoa kadri ya amri anayopewa lakini malipo yake hayatoshi. Hata anapofukuzwa hapewi hata kiinua mgongo au pencheni hakuna utaratibu huo.

Mhe. Abdalla Mwinyi hapa *swahibu* wangu akishasema hamtaki tena sheha basi anamuondoa na atakuwa yeye wamemaliziana sasa sio utaratibu mzuri huo wa kiutumishi. Tukubaliane kuwa na utawala bora katika nchi na masuala haya ni muhimu, mtu kama umemuajiri anafanya kazi miaka miwili, mitatu, minne mpaka mitano au kumi. Sisi hapa tunaajiriwa na wananchi baada ya miaka mitano japo kidogo tunapewa kama penchenia japo kidogo, sasa na hawa masheha kama tumeona wanafanya kazi baada ya kuwaajiri kwa miaka miwili, mitatu apewe chochote iwe ni bahashishi yake lakini kumuacha tu aondoke na mkoba wake si jambo zuri hata kidogo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba nizungumze kidogo katika masuala ya nyumbani Wilaya ya Wete kwanza naomba nimpongeze sana Mhe. Mkuu wa Wilaya ya Wete kwa mashirikiano aliyokuwanayo katika utekelezaji wa kazi zake, ukweli anafanya kazi vizuri sana anajitahidi sana, ila anajitahidi kutafuta watu wa kumsaidia inaonekana anazungurukwa na watu ambao hawana uwezo kidogo sasa jitihada zake nzuri za kufanya kazi zinayumba yumba kwa hivyo ni jambo ambalo ningemuomba sana alifanyie kazi. Mwenyewe binafsi anafanya kazi nzuri sana yuko *very serious* anafuatilia mambo na anachukua hatua lakini wanaomsaidia wanamyumbisha kidogo, kwa hivyo hili ningemuomba alifanyie kazi kidogo.

Sasa kidogo ningeomba nizungumzie suala la pencheni hawa watu wanaopata msaada wengi wanalalamika kwamba hawapati malipo yao hili naomba Mhe. Waziri alifuatilie. Lakini baya zaidi nimeliangalia katika hili buku kubwa Mhe.

Mwenyekiti kifungu kinachohusu pencheni mara hii hakikutiliwa pesa katika wilaya zote za Unguja na Pemba. Sasa hili ningeomba maelezo kutoka kwa Mhe. Waziri, ni vipi kifungu hiki cha pencheni mfano katika Wilaya ya Wete fungu 05 kifungu kidogo 12030 Msaada kwa jumla mara hii hawakuingiziwa hata shilingi moja na katika wilaya zote nimefanya utafiti nimeona hivyo. Sasa hili ni jambo ambalo nataka kuelewa kutoka kwa Mhe. Waziri je ana maana wale wazee wetu waliokuwa wanapata angalau sabuni mara hii hawana kitu au vipi.

Mhe. Mwenyekiti naona unanitizama naomba nimalizie kwa masuala ya Baraza la Mji Wete na Halmashauri ya Wilaya dakika moja moja tu, Baraza la Mji la Wete nalo linafanya kazi nzuri lina mashirikiano mazuri na madiwani naomba waongeze kasi katika masuala mawili matatu. Kwanza masuala ya vyoo mjini watu wanasema ukitaka uiangalie utaarabu ingia katika vyoo vyao vya mjini utakavyoviona ndio jamii ilivyo sasa tuangalieni hili jambo ni muhimu sana katika vyoo vyetu vya mji vikoje wenzetu wanachukulia ni kama kupima *paramitte* ya kupima hali halisi ya tulivyo na ustarabu wetu uko je. Ukienda katika choo ukikiona ni kichafu ana basi hiyo jamii ndivyo tunavyopimwa, kwa hivyo hili ni jambo la kuliangalia sana naomba waongeze vyoo mjini na pia ile *stand* pale naambiwa zamani ilikuwa na lami siji sasa hivi imebakia mawe matupu.

Halafu eneo la Bopwe kuna mtaro mbaya sana unaozana kuhatarisha mazingira ya nyumba za wananchi ningeomba hili kidogo washirikiane na madiwani waliangalie, lakini pia tunahitaji kuanzisha eneo la bustani ni muhimu sana katika mji kama hakuna eneo la bustani ni matatizo, ile bustani ya Afisini kwa Mkuu wa Mkoa naona imeshamaliza maliza naomba kuna maeneo manzuri mfano Uchozini au Bopwe Makaoni kuna maeneo ambayo tunaweza kufanya bustani nzuri.

Mwisho Mhe. Mwenyekiti katika maeneo ya Halmashauri ya Wilaya ya Wete naomba tukiangalie sana kisiwa cha Fundo ni kisiwa kikubwa katika Wilaya ya Wete na Mkoa wa Kaskazini Pemba kwa jumla mbali ya kile cha Kojani, kina wakaazi wanaofika elfu mbili, kina skuli ya msingi na sekondari kina hospitali ya daraja la kwanza, kina vituo vya afya na kuna nyumba nzuri sana ya madaktari imejengwa na Mhe. Mugheri lakini kuna tatizo la umeme na wananchi wa kisiwa kile ni wavuti ambao wanajitahidi sana, lakini umeme unawaangusha sana katika kuona kwamba wanaondoa umasikini.

Kwa hivyo ningeiomba Halmashauri ya Wilaya na Afisi ya Mkuu wa Wilaya na Afisi ya Mkuu wa Mkoa kubuni mradi wa kukipatia kisiwa cha Fundo umeme *alhamdullillah* Waziri Mansour na serikali imejitahidi kuona kwamba sasa Pemba ina umeme wa uhakika. Haitakuwa vizuri kwamba Pemba ina

umeme mzuri lakini kuna wananchi ambao wanauhitaji sana kwa ajili ya maisha yao. Hili ni jambo ambalo naiyomba sana Halmauri ya Wilaya, Afisi ya Mkuu wa Wilaya na Afisi ya Mkuu wa Mkoa kuangalia kutafuta aina yoyote ya mradi tukishirikiana na mimi kama mwakilishi kuona kwamba kisiwa kile tukijaaliwa kinapata umeme wa uhakika.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana.

Mhe. Ali Denge Makame: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kunipatia nafasi hii nami nikawa mchangiaji wa hotuba ya Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ.

Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote nampongeza Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake kwa kutuletea kitabu hichi ambacho kina mambo yanafahamika na yanaeleweka. Nitaanzia ukurasa wa 11 kifungu 24 Usajili na Kadi za Utambulisho. Nawapongeza kitengo hichi kuwa tokea kilivyoanzishwa mwaka 2005 kwa sheria Nam. 7 ya mwaka 2005. Hili limekuwa ni muhimu sana kuanzishwa hapa nchini kuwepo na vitambulisho vya Uzanzibari.

Hili ni muhimu na inasaidia sana kwa kila mwananchi kuwa na kitambulisho chake kile ambacho akitembea nacho ukipatwa na matatizo au maafa mbali mbali inakuwa ni urahisi kutambuliwa. Kwa hivyo pindipo ukiwa na kitumbulisho hichi kitakusaidia kwa mengi, mbali kutambua serikali watu wake lakini hata na wewe mwenyewe mtu binafsi.

Nawashukuru Afisi hii tokea ilipoanzisha inajitahidi sana kutangaza masuala ya fitambulisho. Kwa kweli mtu mwenye sikio anasikia na mwenye macho anaona kama kunahitajika vitambulisho kila mtu awe navyo. Lakini utakuta tokea vilipoanzwa kila siku malalamiko wengine sijui hawajapata wengine sijui hawajapewa. Huwanashangaa kwani wanakuwa wapi kwa muda mrefu vinatangaziwa wanakuwa wapi. Hayo yanainika wazi kuwa watu wanafahamu lakini kwa makusudi huwa hawataki kujiorodhesha ili kupata vitambulisho hivyo ili wapate malalamiko.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa kipindi hichi mara nyingi suala la vitambulisho linatangazwa na huwa linarejea rejea kila mara aliyekuwa bado hajapata aende. Lakini mimi naamini wazi aliyekuwa hataki kwenda ana niya yake nyengine, lakini kwa kuhitaji vitambulisho wote itakuwa wameshapata. Naipongeza taasisi hii kwa juhudi yake inayochukua isipokuwa kubwa tu ninalohofia kelele zimeshakuwa nyingi. Kipindi hichi kila siku zinaongezwa muda mpaka sasa waliotuleta hapa wanalalamika muda huo hauwishi tu, utakwisha lini. Ningeomba maafisa wanaohusika na Afisi hii ya usajili wa vitambulisho wawe

na ustahamilivu na msimamo wao uwe huo huo anayekuja kwa wakati wake sawa na aliyekuwa hakuja iwe basi.

Mhe. Mwenyekiti, nakuja kifungu cha 78 ukurasa za 47 Baraza la Manispaa. Mhe. Mwenyekiti, nawasifu sana kwa juhudi zao kubwa walizochukua za kuubadilisha mji wetu ukawepo katika haiba nzuri. Kipindi kingi cha nyuma ilikuwa mji wetu kuutemele kwa kweli unaona kinyaa, Sasa hivi *alhamdulillah* ukipita barabara za ndani utakuta kuna *tails* nzuri, ukipita katika majengo mengi tu yamekarabatiwa vizuri. Utakuta sura ya mji imeleta matumaini

Ninachowaomba baadhi ya sehemu zilizotiwa *tails*.ambamo zimevunjika au zimetoka basi hali ile irejeshwe ili haiba ile iyendelee kung'arisha.

Nije katika soko la samaki la Marikiti Darajani. Hili soko kwe kweli ni muda mrefu limekuwa ni kiivutia kwa wageni wetu wengi wanaotoka nchi mbali mbali wakiwemo watalii kuja kutembelea katika soko hili na ni soko kwa kweli lipo mjini.

Ninachomuomba Mhe. Wziri kwa kuwa kuna kipindi angalau wawe na vizibao wale wanaouza samaki au shughuli zao zile za kupata ili kuonesha sura ya mji wetu. Kwa kuwa Wizara ilikuwa haiwezi kuwapa vizibao vya kuwapa wachuuzi wa pale Darajani soko Kuu. Mimi ningeshauri kwa kuwa wao wanafanya biasahra kwa faida, washauriwe ili mtu awa na vazi lile la kuleta haiba pale kwenye soko letu.

Mhe. Mwenyekiti, kuna masoko mengine yapo ng'ambu hayo si tatizo sana maana ndiyo yapo mbali, lakini lile la pale mjini ambalo ndio kivutio cha wageni wetu mbali mbali wanaofika pale ni vyema wakafanyiwa mashauri ili angalau wakavaa mavazi yaliyokuwa yanaonesha kama hawa ni watu wanadiaji, hawa waparaji samaki angalau likaleta sura nzuri. Kwa hivyo ningemuomba Mhe. Waziri akaliangalia hilo na akawashauri watendaji wa pale wakawemo katika hali kama hizo.

Nije katika suala la Kikosi cha Jeshi la Kujenga Uchumi. Kwanza nampongeza sana Mhe. Waziri wa Wizara hii kwa umakini wake na uangalizi wake waswahili wanasema ukimuona kainama kumbe anatunga sheria. Namshukuru ile kuinama kwake kumbe anabuni mambo ambayo ya kuleta maendeleo katika vikosi vyake. Hili nampongeza Mhe. Waziri.

Kwa kuwa shughuli za Vikosi vya JKU mara nyingi inakuwa kuzalisha uchumi na kuimarisha uchumi na juhudi zao tunaziona katika maeneo yao mengi ya kilimo yanakuwa katika hali nzuri na wanajitahidi vya kutosha. Ingawaje tuna

uhaba wa ardhi na baadi ya wananchi wetu wengi wanahitaji ardhi ile pamoja na wana kijiji kwa kujipatia maisha.

Ningemuomba Mhe. Waziri akaliangalia zaidi na maeneo ya uwanda ambayo tunayo makubwa sana. Maeneo hayo yanaweza kuimarishwa na vyakula vinaseza vikaota, kuna vyakula vya mahindi, mitama, viazi vikuu, migomba n.k. Kwa kuwa vikosi hivi vinauwezo wa kuomba serikalini au kuomba misaada taasisi mbali mbali wakalenga kuyaimarisha maeneo kama haya yenye uwanda kwani tunayo maeneo matupu kama haya mengi sana wakaweza kulima vilimo mbali mbali. Tungeliiomba Wizara ya Kilimo ili kutafuta mbinu na zana wakaimarisha humo. Katika maeneo mengine yanayolimwa limwa mpunga wakayagema, machache wakawa nayo wao na machache wakawapa na vijiji kwa sababu mule ukulima wake kidogo unakuwa rahisi ili kuwapa nafasi zaidi wana kijini na wao wakapata maeneo ya kulima kwa kutumia zana zilizokuwa nyepesi.

Ningeshauri Mhe. Waziri hapa vikosi vyetu akaviangalia zaidi katika maeneo hayo kwa kuwa tunayo mengi ili kupata kuimarisha zaidi vilimo kama hivyo nilivyovitaja. Na kuwapa nafasi wakulima wetu wadogo wadogo ili na wao wafaidike wkwa yale maeneo yaliyokuwa mepesi.

Mhe. Mwenyekiti, ukurasa wa 73 kifungu cha 116 Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo KMKM. Juhudi zake tunaziona sana za kikosi hichi kuimarisha ulinzi kwenye maeneo yetu ya bahari ili kuzuia mambo mbali mbali ya magendo na kupata nafuu ya usalama katika maeneo mbali mbali. Nataka kusema Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa hapa karibuni paligundulikana meli ya kutoka nje zikivua samaki katika maeneo yetu ya bahari zetu.

Inaonesha dhahiri kuwa samaki wengi sana wamevuliwa nje kwa njia iliyokuwa si halali. Tunakikosi chetu hiki KMKM katika shughuli zake za ulinzi mimi ningeliomba Waziri akaliangalia sana hili kwa kuwatafutia nyenzo zilizokuwa za uhakika wakawemo kama katika shughuli za uvuvi wa bahari kuu lakini kumbe wanafanya kazi zao za ulinzi, ili kupata kuzipata zile meli zilizokuwa zinavua kinyume na sheria au wale watu wanaokusudia kuja kwa nia mbaya kuja katika visiwa vyetu wakapata kuwadhibiti.

Kwa mfano kama hapa karibuni tulisikia baadhi ya waliokuwa wakizifanyia uhalifu meli za kigeni walikuja wakakimbilia katika visiwa yetu, lakini kwa bahati Jamuhuri yetu ya Muungano na vikosi vyetu vya majeshi viliweza kudhibiti sehemu hiyo na kwa bahari walikimbia hawakupatikana.

Kwa hivyo kama tutaviimarisha vikosi vyetu hivi tukavitafutia vifaa ikawa kazi zao wakawa wanafanyia nje ya bahari zetu hizi kwa hivyo vitasaidia kulinda

maeneo yetu kwa mambo mbali mbali ambayo yaliyokuwa yanataka kutokezea. Ningemuomba Mhe. Waziri hili akaliangalia ili kuliimarisha jeshi letu hilo na kupata kuleta faida zaidi katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, nakuja katika ukurasa wa 19 kidungu cha 37 Idara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Tawala inaunganisha nguvu zake katika mikoa na Wilaya hadi shehia katika kutoa maelekezo mbali mbali ya kufanikisha mambo ya maendeleo katika mitaa. Hapa ni vyema Idara hii ikaangalia sana kwa upande wa Masheha. Masheha wetu wanakuwa wana kazi nzito na kazi zao wanakuwa wanafanya saa 24 huwa wanawajibika katika utendaji wa kazi zao.

Ningeomba idara hii ikawaangalia sana kwani huwa wana majukumu mengi ambayo mpaka wanashindwa kuyatatua. Kwa hivyo angalau katika kipindi chao cha miaka mitano wakawa wanafikiriwa kupewa nyenzo zilizokuwa muhimu. Afisi ya Sheha mara nyingi inakuwa kama kituo cha polisi, wageni hawaondoki kwa hivyo angalau wakapewa nyenzo za kutafutia vifaa kama meza, viti, mabusati, hata kulipia mambo ya umeme wakawa wanafikiriwa kila baada ya miaka mitano. Kwa sababu wanakuwa wana kazi nzito matokeo yake baada ya kuzifanya wao wanakuja kwa waheshimiwa wao wabunge au wawakilishi ambayo mambo yenyewe ni madogo madogo tu ili wawatatulie.

Ningeomba Mhe. Mwenyekiti, wakaangaliwa sana hawa Masheha katika masuala ya kuwafanikisha katika shughuli zao hizo. Kama inavyoeleweka kuwa na masheha mambo mengi au makero mbali mbali mitaani yanapungua na mambo mengi ya uharibifu wa mali za serikali pindipo zinapotokezea wanakuwa haraka kuripoti ili kuokoa uharibifu ule. Ningeomba Masheha, Madiwani wakaangaliwa sana ili kupunguza makero yao kwa kila kipindi kinapofikia miaka mitano kupata nyenzo za kufanyia kazi zao.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia nakuja katika Halmashauri za Wilaya na Miji. Mara nyingi huwa tunasikia Halmashauri za Wilaya baada yakusanya mapato yao huwa wanasaidia shughuli za maendeleo za jamii katika maeneo mbali mbali kama kujenga skuli, mitaro, hospitali. Kwa hapa mjini tunayo manispaa ambayo inalingana na shughuli hizo za halmashauri za Wilaya, kukushanya mapato kwa wananchi maduka mbali mbali. Kitu kinachonishangaza kwa upande wangu Jimboni kwangu Shehia za Kilimahewa nina skuli lakini sikupata msaada hata mmoja wa kumbiwa huu saidia kufanyia matengenezo ya skuli.

Mfano kuna mtaro wangu wa maji kutoka skuli ya Kilimahewa mpaka Msikiti wa Ziwatuwe, niliomba mwaka 2008/2009 nikakubaliwa kipindi kile cha Mkurugenzi yule. Kuwa *phrase* itakayokuja na ADB mtaro ule utatekelezwa.

Lakini mpaka leo bado sijaona mafanikio. Mimi wananchi niliwambia kama hili jambo litatekelezwa kwa hivyo sijuia Mhe. Waziri atakuja kunijibu nini kuhusu kipande cha mtaro huo ambao unaleta kero kwa makaazi ya wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia naishukuru wizara hii kwa utendaji wake kama nilivyokwisha eleza. Mimi pamoja na wananchi wenzangu wa jimbo la Amani tunaiyunga mia kwa mia pindipo tukikubaliwa kujibiwa masuala yetu haya. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Nassor Ahmed Mazrui: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi ya mwisho kwa kipindi hichi cha asubuhi na kwa sababu muda ni mdogo naomba kuchangia kwa haraka haraka.

Kwanza kabisa naomba kuchukua fursa hii kumshukuru Mhe. Waziri kwa namna alivyoileta bajeti hii na kuweza kuichangia. Tunamshukuruu sana na tunamuombe kila la kheri katika kipindi cha awamu ya saba.

Mhe. Mwenyekiti, nakwenda moja kwa moja katika ukurasa wa 11,12,13,14,15,16,17 mpaka 18 unaozungumza habari ya Afisi Usajili na Kadi za Vitambulisho katika ukurasa wa 17 utaona kwamba Afisi yetu imepata vyeti vya *ISO* 27001, imepata *Quality Management Systerm* imepata *IQnet*, hizi ni sifa nzuri na wanastahili sifa hiyo. Kwa sababu sisi tumekwenda katika kituo chao tumeona kwamba wanafanya kazi nzuri na wana zana nzuri za kufanyia kazi, wana ari na wana ujuzi mkubwa ni taasisi moja kwa Zanzibar ya kujivunia.

Wasi wasi wangu kwamba taasisi hii imeingiliwa kisiasa tu basi. Lakini ni taasisi nzuri kabisa, inafanya kazi zake vizuri na za kwa mfano wa kimataifa. Kipande hichi mimi nasafiri nacho dunia nzima hata wakitaka tiketi natumia hichi kitambulisho cha Uzanzibari na kinafanyakazi bila ya matatizo yoyote. Suala lililoharibu katika taasisi hii ni kuingiliwa katika masuala ya kisiasa.

Kutokana na sensa ya mwaka 2002 tulikuwa tunawakaazi laki tisa thamanini elfu mia sita ishirini na tano katika kisiwa cha Unguja na ikifika mwaka 2010 kama tulivyosema kitabu hichi kwamba tutakuwa na wananchi wapatao milioni moja laki mbili thamanini na tatu mia nane na thalathini na nne (1,233,834). Ukikisia katika nchi yoyote asilimia 48 huwa ni watu waliofikia umri wa miaka 48 kwa hivyo kisiwa chetu kitakuwa na watu 600,367. Idara ya Vitambulisho imesema kwamba ilitarajia itatoa vipande 573,225 hapo tayari pana nakisi ya kiasi ya watu 35,000 ambao kwamba hawakutiwa katika takwimu zao. Hata hivyo ukiangalia waliosajiliwa ni laki tano sitini elfu (560,000) kwa mantiki hiyo kwa wao ni asilimia 98.

Mimi nataka nichukue hizi takwimu zao hizi zangu mimi niziweke upande. Mhe. Mwenyekiti, malalamiko ni mengi kama wako watu wengi sana Wazanzibari halisi kabisa hawakupata kuandikishwa, huu ukweli usiopingika na ushahidi tunao na upekuzi ukifanywa utaonekana. Mhe. Mwenyekiti, yote haya yamesababisha kuingiliwa kisiasa katika taasisi hii. Hili sasa hivi hatulijui lakini baadaye litatupa taathira kubwa sana huko mbele tunakokwenda.

Kwa mfano upande wa Nungwi kote kule kwenye Mahoteli mengi Kiwengwa na sehemu nyenginezo, Wazanzibari wengi wanalalamika kwamba nafasi nyingi za ajira hatupewi sisi wanapewa watu kutoka Tanga, kutoka Kenya kutoka sehemu nyengine nyingi. Hili ni kweli lakini ukenda kiundani ukimwambia bwana wewe si Mzanzibari anakwambia mimi Mzanzibari anakutolea kadi ya Uzanzibari anakwambia kadi yangu hii hapa.

Taathira hii tutakuja kuiona mbele huko utakapoona mwanao uliomzaa anakosa haki anapata mtu mwengine ambaye amekuja mwaka jana anachukua haki yako kwa sababu ya kutafuta jambo dogo tu, raha ya dakika tano unapata maangamizo ya maisha. Naomba hili suala tuliangalie kwa uzuri kabisa, kwamba tusikubali kuenda huko kwani tutaitia nchi yetu katika madhara makubwa sana. Mimi ningeomba kama iwezekanavyo ufanyike utafiti wa kina kuona kwamba kitengo hiki tusikiharibu, ni kitengo kizuri kinafanya kazi nzuri na kina uwezo mkubwa, kwa nini tukitie katika mambo ya kisiasa.

Mhe. Mwenyekiti suala moja hapa nilizungumza juzi na leo nalizungumza tena. Kwa mfano huyu kijana Idara hii ya Vitambulisho ni 050014921 naomba waziri atuletee hapa tumuone ni mtoto wa skuli ni mdogo tu na hawa wapo wengi na wengine ninao hapa. Mfano mwengine huu hapa mtoto mdogo tu wa miaka 14 ana kitambulisho 100178812 na aletwe hapa mtamuona kama ni mtoto mdogo wa skuli kabisa. Hii mifano miwili ambapo watu wamepewa vitambulisho hapastahiki na ni vijana wadogo kabisa.

Ukiaangalia huyu hapa mwenye kitambulisho 290150061 huyu ana paspoti ya Msumbiji namba DD 005787 bado kapewa kitambulisho. Haya ni makosa ambayo kwamba yameingia katika utashi wa kisiasa na kwamba Idara ya Vitambulisho wanawapa watu ambao hawastahiki na kuwanyima wale wanaostahiki, badili yake utakuta nambari inapanda juu lakini waliopewa ni watu ambao hawastahiki. Haya ni madhara makubwa sana ambayo yatakuja kujitokeza katika nchi yetu. Ningemuomba Mhe. Waziri achukue tahadhari kubwa sana kuhusu masuala haya na kuona kwamba mara moja yanasafishwa.

Kama vile Mhe. Hamza alivyotueleza hapa kwamba idadi ya wapiga kura imepungua kwa kiasi cha watu laki moja kutokana na mchakato uliofanywa katika uandikishaji huu kuwachuja wote ambao kwamba hawastahiki kupigwa

kura wasiandikwe. Basi naomba na Idara ya Vitambulisho nao wale wote ambao kuwa hawastahiki kupewa vitambulisho wasipewe waondoshwe ibakie idadi halisi ya watu wanaosatahiki kufanya hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia katika majimbo mawili jimbo la Donge na Jimbo la Mji Mkongwe wenye vitambulisho ni zaidi ya idadi ya *population*. Kwa mfano Donge wamepewa vitambulisho watu elfu kumi na mbili, mia nne thalathini na moja (12,431) wakati hawapo watu hao lakini kwa mujibu wa takwimu za sensa. Mji Mkongwe wamepewa watu elfu kumi na mbili mia tisa na kumi na nane (12,918) ambao kwa mujibu wa takwimu hawafiki watu hao.

Kwa hivyo bila shaka kuna watu wengi sana ambao kuwa wamepewa kitambulisho hawastahiki. Ningeomba suala hili lisafishwe na liwe safi ili huko tunakowenda tuwe na uchaguzi huru na wa haki na vile vile tuwe na Idara ya Vitambulisho ambayo kwamba sisi idara hii tuiamini na tuipe hadhi yake inayostahiki kama ilivyopewa vitambulisho vya ISO 9001 na 27001

Mhe. Suala la vikosi. Vikosi tunavyo KMKM ni kikosi cha magendo ambacho kwa muda mrefu kazi yake ni kukamata karafuu hiyo ndio kazi kubwa pamoja na magendo mengine. Kadiri biashara inavyokuwa na kadiri tunavyotanua wigo wa kuungana tumeungana Tanzania, tunaungana na Afrika Mashariki utakuta Kikosi hichi kinazidi kukosa kazi zake. Mfano karafuu zikibinafsishwa tayari magendo yanaanza kupungua.

Suala la uvuvi ukiwa uvuvi huu vile vile utapewa nguvu zinazostahiki kikosi hiki vile vile kitakosa kazi ya kufanya. Lakini kikosi hiki kina kazi kubwa sana katika nchi hii na ningeomba hili jila la KMKM lingebadilishwa ili suala la magendo likaondoshwa likapewa kazi inayostahiki. Sisi tumo katika kisiwa, tunataka ulinzi wa kisiwa, ulinzi wa mali zetu, raia zetu na uokozi wa maisha wa watoto wetu ambao watafanya kazi katika uvuvi na usafiri.

Tukenda katika JKU, tunasema ni jeshi la kujenga uchumi. Mimi ninavyofahamu miye ndio lijenge uchumi, sasa uchumi gani linalojenga jeshi hili kuwa kila mwaka lipewe mabilioni. Ilikua jeshi hili la kujenga uchumi liweke mikakati mizuri ya kujenga uchumi kweli, lizalishe uchumi, lisaidie serikali na wao wenyewe wajiendeshe liwe *sustainable*. Lakini badili yake jeshi hili kila mwaka bajeti inakuja linapewa kasma ya fedha. Kwa hivyo hili limekuwa si jeshi la kujenga uchumi, hili limekuwa jeshi la kuuwa uchumi. Lingeundwa jeshi la kujenga uchumi lipewa nafasi ya kujenga uchumi sio kuuwa uchumi.

Mhe. Mwenyekiti, tulikwenda katika kuangalia tuliponana nao wale jamaa wa JKU, tukakuta pale kuna Mkuu JKU anakaimu sehemu hii kwa miaka miwili

sasa hivi, sijui kama mpaka sasa hivi anaendelea kukaimu. Lakini ningemuomba Mhe. Waziri mambo ya kukaimu kwa muda mrefu yana madhara yake na kama huyu bwana kama bado anakaimu mimi ningeomba kama keshakaimu kwa miaka miwili basi anao uwezo apewe nafasi hiyo awe yeye ndiyo kiongozi au atafutwe mwengine anayefaa awe kiongozi wa JKU. Hii imo katika ukurasa wa 76 na 77.

JKU inaweza kupewa nyenzo za kuweza kujiimarisha kwenye kilimo cha biashara, kwenye viwanda vidogo vidogo na mambo mengine kadha wa kadha ambavyo inaweza kuingiza fedha nyingi na ikaweza kujenga uchumi na ikaweza kutoa mafunzo kwa watu wetu kwenye mambo ya masuala ya *inter preneurship.*

Katika ukurasa 33 Kikosi cha Zimamoto, kikosi hichi ni muhimu sana, tunaleta watalii nchini, tunapanua uwanja wa ndege, tunaongeza idadi ya watalii kuingia nchini ilikuwa kikosi hichi kizidi kuongezwa kiongezee mapato zaidi kiimarishwe zaidi ili ndege zinazotua uwanja wa ndege na wale watalii wanaokuja hapa waone kwamba wakifika hapa ni pahala salama, sio pahala pa kuja kumalizana na moto. Bado kikosi hichi hakijapewa nyenzo zake zinazostahiki wala hakijapewa cheo chake kinachostahiki ningeomba kiangaliwe zaidi na kipewe nguvu zaidi ili kiweze kuimarisha uchumi. Kwa sababu Watalii wakiingia nchini na ndege zikitua nchini ndio tutaweza kuwa na uchumi bora zaidi na wafanyabiashara biashara zao zitakuwa katika *safe side* wataweza kuwa na moyo zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, Kikosi cha Valantia kikosi hichi kazi zake mimi sijaziona kila nikiangalia kwenye nchi yetu kazi zake sijaziona, lakini ndio kipo kimewekwa kama chunjua, naomba kifanyiwe utafiti kionekane kwamba namna gani wataweza kutumiwa ili waweze kuleta faida katika nchi yetu isiwe wamekaa kitako tu kama chunjua kupamba uso kupamba ngozi au kupambua ngozi, wapewe kazi ambayo kuwa itastahiki kuweza kufanya kazi, itakayoweza kusaidia katika maisha yetu.

Mhe. Mwenyekiti, nakwenda kwenye masuala ya Baraza la Mji. Baraza la Mji, ningewaomba tuelewe kwamba Zanzibar ni nchi ambayo kuwa kwamba ina watu milioni moja laki mbili na ushei. Watu hawa wote wenye uwezo walioajiriwa na serikali arubaini na saba elfu mia tano na hamsini na moja kwa hivyo kuna watu katika nchi hii laki tano na hamsini elfu na arubaini na sita hawana kazi, ni *informal sector* watu hawa tunasema asilimia sabiini wamo katika suala la uvuvi na kilimo ambao ni laki tatu thamanini tisa elfu na sabiini na moja. Kwa hivyo kuna watu laki moja sitini na tisa elfu na arubaini na nne ni nguvu kazi hawa hawana kazi kabisa. Lakini mabaraza ya miji yameshindwa kuwatumia watu hawa kuweza kufanya biashara zao, kuzalisha mali na kuleta

maendeleo katika taifa letu na kutanua wigo wa mapato katika nchi yetu. Watu laki moja na sitini na sita elfu kazi zao ni za kuzagaa zagaa tu, kufanya biashara ndogo ndogo. Hawa wangeweza kutumiwa vizuri Mabaraza yetu ya Manispaa yakaweza kuwajengea masoko mazuri mwahala mwingi mwa kufanya biashara naamini kwamba wengepata fedha nyingi zaidi na wangeweza watu wetu kupata kazi zaidi.

Mabaraza ya miji mpaka sasa hivi yameshindwa kuwatumia watu kuzalisha mali katika nguvu kazi hii. Kwa kweli nasikitika sana kuona serikali ya CCM imo kwa muda wa miaka 10 hii ya mwisho lakini watu walioajiriwa hawajafika hata laki moja ambao wameajiriwa katika *private sector* na serikali. Ningeomba kazi zaidi ifanywe kuona kwamba watu angalau laki moja na nusu wanaajiriwa katika nchi hii ndio nchi hii itakuwa katika stebility ya kiuchumi. Kwa sababu asilimia zaidi ya 50 ya watu waliokuwepo Zanzibar wanachumiwa, wanaochumiwa ni wengi kuliko wanaochuma. Kwa hivyo hali hii inakuwa ngumu kimaisha na inapelekea matatizo mengi sana.

Jengine ningeomba katika Baraza la Manispaa kuna JBC, Baraza la Manispaa ya Pemba linahusika moja kwa moja na kubomoka Wizara ya Fedha. Kamati hii ina mainjinia, ina wabunifu, wametoa kibali cha kujengwa jengo hili wakati jengo hili linajulikiana kwamba dizaini yake *foundation* ilikuwa si sahihi. Lakini JB ya Chakechake ilishindwa kuliona hilo na inalipwa ili kwenda kukagua majengo haya, ilishindwa kujua ujenzi huu si ujenzi wa pahala pale. Kwa hivyo mimi ningeomba. Miye ningeomba Mhe. Waziri waiwajibishe mara moja Kamati hii iache kazi kwa sababu haiwezi kazi, itatutia hasara nyingi sana katika nchi hii.

Mhe. Mwenyekiti, muda wangu ni mdogo sana kwa kweli siwezi kumaliza yote mambo niliyonayo ni mengi na muda umemalizika, na siwezi kuyaeleza. Nikuombe unipe muda tena jioni kama haikuwezekana. Ahsante sana. *Asalaamu Aleykum warahmatullahi wabarakatu.*

(Sasa 7:00 mchana Baraza liliahirishwa hadi Saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe, Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii ya mwanzo Mwenyezi Mungu akubariki. Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia jioni hii ya leo kuweza kuchangia hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na

Vikosi vya SMZ juu ya Mpango wa Matumizi ya Mwaka wa Fedha wa 2010/2011.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nianze kumpongeza Mhe. Waziri kwa hotuba yake hii nzuri, imepangika, hatukupata tabu sana kuisoma, pamoja na watendaji wake wote tunawashukuru na kuwapongeza sana kwa hotuba yao hii.

Hotuba hii ni ndefu sana na unaweza kuichangia tokea asubuhi mpaka jioni, ni kwa sababu imegusa karibu maeneo yote ya nchi nzima. Lakini kwa leo Mhe. Mwenyekiti, mimi nitachangia katika maeneo makubwa matatu.

Eneo la kwanza ni eneo linalohusika na utambulisho au usajili na kadi za vitambulisho. Kwanza nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mkurugenzi wa Vitambulisho kwa kazi nzuri anayoifanya ya kutusajili na kutupatia Vitambulisho wa Mzanzibari Mkaazi. Takwimu zinaonesha kwamba karibu asilimia 98 ya Wazanzibari wamepatiwa vitambulisho vya Mzanzibari wale wenye sifa. Kwa hivyo, nitumie nafasi hii kumpongeza pamoja na watendaji wake kwa kazi nzuri anayoifanya.

Lakini jengine Mhe. Mwenyekiti, amezungumzia juu ya malengo yaliyopita na malengo mapya. Ametuelezea kwamba, katika bajeti hii atatengeneza vitambulisho vipya na kubadilisha vile vitambulisho vya zamani. Hiyo kazi nadhani sasa hivi inaendelea. Kitu ambacho ningetaka kusema, vitambulisho kwa mtizamo wa vitambulisho ni vizuri, lakini mimi wasiwasi wangu ni mmoja. Pamoja na kwamba ametueleza hapa ameshapata kutunukiwa vyeti vinne vya kimataifa vyenye ubora wa vitambulisho. Lakini badi nina wasiwasi mmoja.

Wenzetu wa Tanzania Bara walitaka kuitumia afisi hii kwa ajili ya kutengenezea vitambulisho, lakini baadae wakaghairi na kwa sababu wamesema vitambulisho vyetu haviendani na wakati na wao wanataka vitambulisho vinavyokwenda na wakati, ambapo vitambulisho vinajumuisha mambo mengi. Sasa vitambulisho vyetu hivi havina mambo mengi au havina uwezo wa kutoa taarifa za aina nyingi ambazo wenzetu tayari wanazo.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, mimi ningeiomba serikali, pamoja na vitambulisho vipya ambavyo wanavitoa sasa hivi, basi tupange mipango ili tuone tunakwenda na wakati, ili vitakapomalizika hivi vya sasa hivi basi vijavyo tayari tuandane na hivyo vitambulisho ambavyo vinakwenda na wakati vilivyojumuisha mambo au taarifa nyingi juu ya yule mtu. Kwa hivyo, niiombe serikali kwa makusudi kwa kushirikiana na Idara ya Vitambulisho tufanye kila linalowezekana twende kwa wakati, tumeanza mwanzo tusije tukaachwa nyuma.

Pamoja na kwamba tumeshazowea kwenda kwa utaratibu huo. Tulianza televisheni mwanzo lakini sasa hivi tuko nyuma walioanza mwisho wako mbali. Kwa hivyo, na hili nalo bado tusikae nyuma twende kwa mujibu wa wakati unavyokwenda. Hilo ni eneo moja.

Eneo jengine Mhe. Mwenyekiti, ambalo ningependa nilizungumze ni Baraza la Manispaa la Zanzibar. Kwanza nimpongeze Mkurugenzi wa Baraza la Manispaa la Zanzibar kwa juhudi yake kubwa anayoichukua katika kuendeleza mji wetu huu wa Zanzibar. Kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, kuna mabadiliko makubwa ambayo tunayaona tokea kukamata wadhifa huu. Kumekuwa na ongezeko la mapato, taa sasa za barabarani maeneo ya Michenzani tunaziona zinawaka na mambo mengine, nikiyataja hapa siwezi kuyamaliza.

Kwa hivyo, mimi nitumie nafasi hii kumpongeza sana kwa juhudi na uzoefu wake kwa kuweza kufanya mambo haya mazuri. Nimuombe aendelee kufanya hivyo ili tuone mji wetu unabadilika.

Suala la ng'ombe wanaozurura sasa hivi limeshaanza kuchukuliwa hatua jambo ambalo hapo mwanzo lilikuwa ni kero kubwa. Ni jambo ambalo kwa kweli lilikuwa linatusononesha.

Mimi Mhe. Mwenyekiti, naishi pale Magomeni karibu na *roundabout* ya Mwanakwerekwe. Huwa nasononeka sana kuona kwamba ng'ombe wanazagaa pale. Kwa hivyo, sasa hivi hatua zinachukuliwa ili kuona kwamba ng'ombe wale wanapotea.

Lakini jengine niwapongeze kwa miradi ile ya michirizi. Kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, Manispaa imefanya kazi kubwa kupata mradi ule wa michirizi ambao utaondosha kero kwa wananchi mbali mbali hasa wa ng'ambu. Wananchi wangu wamekuwa wakipata tabu sana hasa katika maeneo ya Sebleni, Mwantenga, Ziwatuwe. Kwa mujibu wa ramani ya michoro ya kuondosha maji katika maeneo hayo na wao watafaidika. Kwa hivyo, nitumie nafasi hii kuwashukuru na kuwapongeza sana.

Mhe. Mwenyekiti, nije sasa katika eneo moja la Halmashauri ya Wilaya ya Kati. Hili nalo nimesema kwa makusudi nilizungumze, juu ya msamaha unaotolewa na serikali wa makontena ya saruji. Kama unakumbuka Mhe. Mwenyekiti, tumekuwa tukisema mara nyingi. Mimi mwenyewe nikiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi nilikuwa nikilizungumza kila wakati na Waziri Anayeshughulika na Masuala ya Fedha ni shahidi. Ni kwamba misamaha au fursa ya misamaha inatolewa vibaya, mara nyingi huwa

tunapata majibu kwamba misamaha hii kuna kamati inapitia na mambo mengine, lakini kwa kweli misamaha inakuwa mikubwa mno.

Hata juzi kwenye Bajeti ya Serikali Mhe. Waziri alisema kwamba wanategemea kupitia sera au na zile taratibu za utoaji wa misamaha. Lakini Mhe. Mwenyekiti, sera na utaratibu wa kupitia misamaha sio tatizo, tatizo liko katika utekelezaji wa jambo hili. Taarifa zinaonesha kwamba, kwa mwaka huu wa 2009/2010 serikali imesamehe zaidi ya shilingi 23.8 bilioni, na makusanyo ni 54 bilioni ya mwaka.

Ukiangalia nchi kama Zanzibar nchi masikini kiwango hiki ni kikubwa mno kinakaribia asilimia 50 ya makusanyo. Kwa kweli hili ni jambo ambalo sisi kama wawakilishi wa wananchi tunahitaji kuliangalia kwa makini.

Nimepata taarifa hivi karibuni kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Kati kwamba kuna kontena 50 za saruji ambazo zimetolewa msamaha, na msamaha uliotolewa pale ni shilingi 58 milioni na thamani ya saruji hiyo ni 114 milioni. Kwa kweli mimi nilikuwa najiuliza, Halmashauri ya Wilaya ya Kati kuna miradi gani ya kuagiza saruji kutoka Pakistan kuleta huku? Na sasa hivi kuna saruji nyengine inateremshwa kontena mia moja na Halmashauri ya Wilaya ya Kati nazo zinatolewa misamaha vile vile!

Hili ni jambo la kusikitisha na sijambo la kukaa kimya linahitaji kuchukuliwa hatua zinazofaa. Na kwa sababu tumekuwa tukilalamika sana na hata wenyewe watu wa Halmashauri ya Wilaya ya Kati wanalalamika. Hivi inakuwaje leo misamaha kama hii, fedha nyingi kama hizi zinatolewa misamaha.

Nimejaribu kupitia taarifa hizi za Halmashauri za Wilaya ya Kati kwamba wao wanasema makusanyo yao ya mwaka 2009/2010 ni shilingi 72 milioni, leo wamewezaje kununua saruji ya shilingi 114 milioni wakati mapato yao ni shilingi 72 milioni? Mbali ya hayo, sasa hivi kuna saruji inateremshwa kontena mia moja sijui hizo zitatolewa misamaha kiasi gani. Inaonekana hapa pana ujanja unaofanyika na msamaha huu umetolewa kwa sura ya miradi ya wananchi na miradi ya wananchi humu katika kipindi cha mwaka 2009/2010, fedha zilizokwenda kwa miradi ya wananchi ni shilingi 11 milioni tu na mia tano.

Kwa kweli Mhe. Waziri hili jambo haliwezi kuvumilika, tumekuwa na kelele nyingi, mbinu hizi zimekuwa nyingi. Waziri wa Fedha sisi tunalalamika sana. Mimi kama Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi nilikuwa nikilalamika sana.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri utakapokuja kufanya majumuisho naomba unipe taarifa za uhakika zisizo na shaka, unitoe mashaka juu ya jambo hili. Unitoe mashaka juu ya msamaha wa kontena hizi zinazotolewa ni miradi gani ya wananchi saruji hii inapelekwa, fedha hizi za saruji zilizonunuliwa kutoka nje zimepatikana wapi wakati humu hazioneshi kiwango kama hicho. Unitoe mashaka ili na wananchi nao wawe hawana mashaka juu ya jambo hili.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, mimi nisingependa kuingia sana, ninazo *document* za kutosha nimeletewa, kumbe kilio changu cha siku zote zile nalalamika sina *document* basi zimeletwa hapa hapa. Kuna hili, hili na hili, wananchi wema wametuletea *document* juu ya fedha za walipa kodi zinavyokwenda. Wananchi wetu wamekuwa wakisumbuka huko wanalipa kodi mbali mbali, lakini inaonekana kuna ujanja ujanja. Mimi nasema kuna ujanja hakuna ukweli katika kusimamia jambo hili.

Sasa Mhe. Waziri naomba sana utakapofanya majumuisho unipe taarifa ya kutosha juu ya jambo hili, niridhike kwa sababu wewe ni rafiki yangu sana. pengine mambo haya yanafanyika huna habari, lakini kwa kuwa wewe ndio uko humu hatuna wa kumuuliza itabidi tukuulize wewe juu ya kadhia hii. Utueleze namna gani Halmashauri yako ya Wilaya ya Kati inachukua misamaha kinyume na taratibu.

Kwa hayo machache Mhe, Mwenyekiti, muda wangu umemalizika, kwa niaba ya wananchi wa jimbo langu naunga mkono hoja ahsante.

Mhe. Najma Khalfan Juma: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, jioni hii na mimi kupata nafasi kwa kuchangia mawili matatu katika wizara hii ninayoipenda sana ya Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ. Kwa sababu waziri wake rafiki yangu mpenzi. Wizara hii ni wizara ambayo inakwenda moja kwa moja mambo yake kwa wananchi, ni wizara ambayo wananchi wanaitumia sana kwa sababu kuna Tawala za Mikoa, mna Vikosi vya SMZ, lakini pia mna Manispaa, Mabaraza ya Miji na Halmashauri za Miji.

Kwa hivyo, ni wizara ambayo ina mkabala na wananchi moja kwa moja na ndio maana kukawekwa Mabara ya Manispaa na Halmashauri za Miji kwa ajili ya kuwahudumia wananchi.

Moja katika shughuli zinazohudumiwa wananchi ni usafi wa mazingira yao. Usafi uko katika nyanja nyingi, lakini usafi mmoja wanaoshughulika nao watu wa Manispaa ni kusafisha pengine vyoo vya watu au karo kwa magari yao baadae kwenda kutafuta pahala wakamwaga. Lakini jambo linalonisikitisha katika hii kusafisha karo au vyoo, hili gari la Manispaa SMZ 6678 huwa hawana pahala maalum pa kumwaga huo uchafu na kwa bahati mbaya uchafu

huo humwagwa moja kwa moja kutoka ndani ya makaro au vyoo basi unamwagwa tu bila ya kutiwa dawa.

Nchi za wenzetu huu uchafu ukishakufyonzwa katika vyoo na makaro huwa unatiwa dawa kwanza halafu ndio unamwagwa tena haumwagwi pahala popote tu, unamwagwa pahala maalum. Hii hapa picha ya TATA la Manispaa na hii hapa nyengine picha ya TATA la Manispaa SMZ 6678. Kwa sababu tukisema mambo lazima tuseme na ushahidi, wakishakunyonya uchagu wao basi si kama wana pahala maalum pa kumwaga, watakwenda pwani penye ufukwe wamwage, tena wanamwaga usiku au magharibi watu wasiwaone, wanamwaga hao halafu wanakimbia, wakati mwengine wala hawafiki huko pwani wanamwaga karibu na makaazi ya watu yalioko sungo sungo hivi.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa tunaomba hizo picha na sisi tuzione, mpe mhudumu yuko nyuma yako hapo.

Mhe. Najma Khalfan Juma: Sawa utaziona. Sasa hili si jambo zuri kwa sababu unapofanya jambo kama hili maana yake umekwenda kusafisha huko basi na hao wengine usiwamwagie. Desturi ya bahari haili kitu kilichokuwa sichake, hata kama umemwaga pale baharini uchafu wako yakija maji hata kama yatachukua lakini halafu itatema kwa sababu sichake. Kwa hivyo, madhali sichake hakikai baharini kitakuja juu tu, sasa kikija juu uchafu huu unabakia ufukweni. Sasa jamani Manispaa mnatufanya vipi?

Jambo la pili tuna vikosi vya SMZ vinafanya kazi yake wakati mwengine nzuri, lakini wakati mwengine havifanyi kazi vizuri sana hasa wakati wa uchaguzi. Wakati wa uchaguzi uliopita mwaka 2005 vikosi vya mafunzo na baadhi ya vikosi vyengine historia lazima isemwe waliingia katika majimbo fulani wakapiga kura majimbo ambayo hayawahusu. Nataraji katika uchaguzi wa mwaka huu Mhe. Waziri vikosi hivi havitokwenda tena kuharibu chaguzi katika majimbo ya watu, kila mmoja atapiga kura katika jimbo lake. Kwa sababu askari nao ni wananchi wana majimbo yao ya uchaguzi watapiga katika majimbo yao.

Halafu Mhe. Said Ali Mbarouk wakati fulani alipokuwa akichangia alishangaa kwamba pesa hizi zimekuwa nyingi kutoka shilingi milioni mia tatu mpaka milioni mia nane. Lakini kuna utengenezaji mpya wa vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi. Mimi natoa rai, kwa sababu zinazotumika ni pesa za wavuja jasho, basi isiwe kila baada ya miaka mitano kubadilisha kitambulisho iwe kila baada ya miaka kumi tubadilishe vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi.

Hata mwanadamu miaka mitano mimi bado sijabadilika, lakini baada ya miaka kumi utaniona kubadilika kwangu. Sasa tusitumie pesa kila baada ya miaka mitano tukazichezea kwa kubadilisha vitambulisho, tungojee miaka kumi tubadilishe na hii ndio kimataifa kubadilisha kitu kila baada ya miaka kumi.

Jambo jengine karibu vitatolewa hivi vipande vipya, lakini kuna tatizo kwa masheha. Alipokuja mwananchi kuandikisha ulimwambia unakaa wapi? Nakaa Mtoni kwa Mazrui na wewe ndivyo ulivyomwambia Mtoni kwa Mazrui, nakaa Mtoni kwa Kisasi, nakaa Mtoni kwa nani, lakini siku anayokuja kuchukua kitambulisho chake unamuuliza wewe unakaa wapi? Nakaa Mtoni kwa Kisasi hakuna jina hilo hapa, hakuna Mtoni kwa Kisasi hapa. Aka, sote tunaua daladala Mtoni wapi Mtoni kwa Kisasi, Mtoni Mazrui unamwambia jina hilo hakuna hapa. Sasa mwananchi yule unamhangaisha na pengine jina lake lipo unamkosesha haki yake. Kwa hivyo, tunaomba kabisa masheha safari hii wasije wakatufanyia mambo hayo.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ujenzi wa afisi mpya katika mikoa yetu hasa Mkoa wa Kaskazini na Kusini Pemba. Afisi za Wakuu wa Mikoa sio nzuri ni mbovu. Nikienda katika afisi ya Mkuu wa Mkoa wangu Kusini namuonea huruma kwa sababu ni mbovu, imeliwa na mchwa haipendezi kuambiwa hii ndio afisi ya Mkoa na Kaskazini pia. Kwa hivyo, mimi naomba basi mana sikuona humu kama kuna chochote kilichotiwa kwamba watajengewa. Sasa naomba na hawa Kaskazini na Kusini Pemba wajengewe.

Vile vile katika kuna utiliaji mkazo ukulima wa viungo na matunda. Sasa mimi ninachokiomba wananhi huko katika mikoa basi watiliwe mkazo kweli kulima biashara za viungo. Kwa sababu manjano ina bei, tangawizi ina bei, pilipili manga na mambo mengine mengi ya viungo yana bei ukilinganisha pengine na karafuu sasa hivi. Na matunda wananchi wa Zanzibar tunakula yale yale miembe aliyoipanda babu, bibi, lakini sisi siku hizi siwapandaji sana kama wazee wetu waliopita. Kwa hivyo, tunaomba katika mikoa hiyo mbali ya kuhimiza wananchi walime muhogo tu na migomba, lakini wahimizwe pia kupanda miti ya matunda.

Pia naomba ukulima wa kisasa wa utumiaji umwagiliaji maji, tusilime tu katika ule mtindo tuliouzowea wa kungojea mvua pia na mboga mboga. Ni aibu wananchi wa Zanzibar kununua tungule kutoka Tanzania Bara au Kabichi hasa tukizingatia wakati mwengine zinaleta maafa hizi.

Hivi karibuni nilisikia katika vyombo vya habari watoto wamekufa na wengine wamelazwa katika hospitali na wazee wao kwa sababu ya kula mboga mboga hasa kabichi ambazo zimepigwa dawa ya vyandarua sijui. Dawa hiyo imepigwa ili kuuwa wadudu katika zile mboga mboga, sasa zile sumu zinabakia,

zikibakia na sisi tunakula na tukila hatari sasa. Kwa hivyo, mimi naomba tuwahimize wananchi.

Vile vile soko kwa wafugaji wa kuku na mayai hawana soko la uhakika. Nilikwenda katika afisi ya *TASAF* Pemba, wafugaji wa kuku wanazunguka mwisho wanashindwa mayai yao wanayapeleka *TASAF* pale wauziwe, sasa *TASAF* hawana duka. Kaw hivyo, mimi naomba tunapowahimiza wananchi wafuge na kulima basi tuwatafutie soko la uhakika watakalouza bidhaa zao. Mayai Pemba kwa mujibu wa *TASAF* yanakaa mpaka yanaoza kule afisini kwao na hakuna watumiaji wa mayai sana kule Pemba, wengi kila mmoja ana kuku wake anakula mayai yake ya kuku wa Kiswahili.

Naomba jambo jengine kuhusu bustani. Bustani zipo hapa Unguja kama Forodhani pamoja na *Jamhuri Garden.* Naomba kwa mikoa yetu, halmashauri, mabaraza yetu yalioko Pemba, yatafute sehemu basi kwa watoto na wazee wa Pemba kila wilaya tujengewe na sisi bustani. Wapelekwe wataalamu wa kujenga bustani maeneo yakipatikana ili na watoto wa kule Pemba waweze kupata raha kama wanazozipata wenzao hapa Unguja. Naona choyo nikipita *Jamhuri Garden* nikikuta pembea za watoto wanacheza jioni au Forodhani, lakini nasikitika kwa watoto wangu wa Micheweni, Chake Chake, Wete au Mkoani ikifika jioni hawana pa kwenda wanakaa vibarazani basi. Hii kwa kweli inatia huzuni.

Umeme Pemba upo sasa hivi, lakini taa za barabarani haziwaki kabisa, hakuna hata taa moja barabarani Pemba inayowaka. Tunajua umeme ni ghali, hapa pengine ni mashirika ndio yanayolipa, lakini basi tujitahidi kidogo angalau taa moja hapa moja kule lakini ziwake ili na sisi tuweze kufaidi huo umeme.

Jambo jengine kwa sababu muda ni mdogo, ufufuaji wa mitaro hapa Mnazi Mmoja. Mnazi Mmoja ipo mitaro hapa, lakini inasikitisha inapokunya mvua maji yanatuama kwa sababu ile mitaro imekufa. Basi pafanywe mipago ili mitaro hii ifufuliwe na maji yasijae na wanamichezo waweze kufaidi matunda.

Vile vile jambo jengine kuna haja sasa ya kuharakishwa maendeleo katika Manispaa yetu ya Unguja, pia katika Mabaraza ya Miji ili hii Manispaa ya Unguja iharakishe baadhi ya mambo iweze kuwa jiji la Zanzibar. Na yale Mabaraza ya Miji kule Pemba yaharakishwe baadhi ya mambo yafanywe ili yageuke kuwa Manispaa tusibakie tu kuwa Baraza la Mji na zile halmashauri baadhi yake ziharakishwe ziwe Mabaraza zisiwe Halmashauri tu.

Kwa mfano, Wilaya ya Magharibi inakuja na maendeleo haraka haraka, Wilaya ya Chake Chake inakuja na maendeleo ya haraka haraka pamoja na Wilaya ya Wete. Basi haya yaambiwe yafanye nini katika miji yao ili waweze kuwa

Manispaa, hapa Unguja pafanywe nini katika huu mji ili tuweze kuwa na jiji tubadilike.

Hivi juzi tu nimemsikia Rais Kikwete kayapa hadhi baadhi ya Mikoa ya Tanzania Bara huko Arusha kawa nani, wapi kwengine sijui wamepandishwa kutoka Mabaraza wamekuwa Manispaa. Kwa hivyo, na sisi iko haja ya kufanya mambo kama hayo ili tuweze kuwa vizuri.

Jambo jengine ni kuhusu Darajani sokoni, sehemu ya soko ya mboga mboga kule kunakochinjiwa kuku. Kwa kweli ile sehemu ni mbovu jamani, mnaitengeneza kidogo kidogo, lakini itengenezeni kwa haraka ili watu tuweze kwenda pale sokoni tukijisikia, tuache kusikia ile harufu mbovu pale.

Mhe. Mwenyekiti, lakini sio hilo tu pia soko la Chake Chake la mboga mboga ni bovu mno na ni dogo na ile stendi pale ni mbovu na imeshaliwa liwa. Lakini ile sehemu iliyobakia basi hata lami haitiwi na wale madereva wanatoa kodi pale, hizi kodi zinafanya nini kama haziwarudii wenyewe wale wavuja jasho pale, walipa kodi. Lile soko letu pale Chake Chake wala lisijengwe tena, lakini ni soko la historia. Litengenezwe japo lile paa na vibaraza vyake vifanywe vizuri, litiwe tarazo ili lile soko lipendeze.

Mhe. Mwenyekiti, wananchi wakaazi wa Chake Chake mjini hawana soko la samaki. Samaki wanauzwa humo tu vichochoroni na susu, hilo susu lenyewe ukikamatwa nalo Baraza la Mji likupeleke jela. Kuna watu wameshakaa jela wiki mbili au wiki tatu kwa sababu wanauza samaki. Lakini wauza dawa za kulevya wako nje tu wanadunda.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe nakuomba umalizie.

Mhe. Najma Khalfan Juma: Haya namaliza mheshimiwa wangu. Kwa hivyo, mimi nasema soko hilo litengenezwe na soko hilo la Darajani litengenezwe ili tupate masoko mazuri.

Mwisho kabisa kwa sababu mengine nayakata, nakuja kwenye Kikosi cha KMKM. Kikosi hiki nyumba zao kweli ni mbovu kule Wete, ni aibu hata ukiambiwa hii nyumba anakaa askari ni aibu. Vile vile hawa KMKM wanataka kiona mbali, kukaa bila ya kiona mbali meli zinaingia huko wao hawana habari maskini. Boti zao ni chache walizokuwa nazo, basi jamani hata hicho kiona mbali. “Hebu tukateni pua tuunge wajihi” ili tuwapatie kikosi chetu cha KMKM vifaa. Sitaki kusema lile neno, kwa sababu lipo neno linalotumika, lakini mimi ni mtu wa habari silisemi, lakini nikisema kiona mbali nadhani mtajua. Wapatiwe kiona mbali hawa ili waweze kuona mbali, masafa ya mbali kutoka nchi kavu mpaka baharini.

Mhe. Mwenyekiti, na Kambi ya Msaani nao zile nyumba zao ni mbovu wanazokaa wale wanajeshi wetu. Kwa hivyo, zitengenezwe zile nyumba za Kambi ya Msaani, vile vile wapewe matrekta. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Haji Faki Shaali: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana mimi sina mchango mkubwa. Mimi kwanza nataka nizungumze kwa ujumla, kuhusu utafiti wa APRM Tanzania ulivyoziona serikali za mitaa hapa Zanzibar. Mwenyekiti, kumradhi nitasoma kama vile ilivyoandikwa kwa lugha ile ile waliyoandika wao, ili nisije kuharibu maana watakuwa wenzangu wamenifahamu.

Kwanza hii ni nambari D wanasema;

"*Weak transparence and accountability and local government revenues"*. Nyengine wanasema; "*Inadequate capacity of local government authorities to develop and execute local plans and budget to general revenue for under taken development and decadent programs"* nyengine anasema; "*Tendency of central government to interfere with operation of local government authorities".*

Sasa huu ni utafiti sio maneno yangu ni wataalamu tena ni wataalamu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania waliofanya utafiti. Wanasema kwamba katika hizi serikali zetu za mitaa, hakuna uwazi na uwajibikaji, hasa katika masuala ya fedha. Hilo ni suala moja ambalo wataalamu wameliona.

Jengine waliloliona wanasema uwezo mdogo wa katika kupanga bajeti na ku-*generate revenue* na kufanya mipango mingine ya maendeleo. Hilo ni tatizo jengine wameliona wenzetu.

Vile vile wakagundua tabia ya Serikali Kuu kuingilia shughuli za Halmashauri za Wilaya.

Kwa hivyo, huu ni utafiti wa wataalamu wakubwa, watu wasomi wakubwa waliofanya utafiti katika Tanzania Bara na Zanzibar, wao wamesema hivyo kuhusu serikali za mitaa.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, kwa ufupi hapa niseme kwamba Mhe. Waziri unakazi kubwa katika masuala haya matatu. Kwanza kuhakikisha kwamba kuna uwazi na uwajibikaji katika fedha kwenye Halmashauri zetu za Manispaa. Kwa sababu hilo wataalamu wameliona, ukilikataa sio la Haji Faki Shaali.

Halafu suala hili la utaalamu katika mambo ya bajeti na kutafuta fedha, huu utaalamu wa halmashauri mdogo. Wewe angalia halmashauri za Pemba, makusanyo yao kwa mwaka ni milioni 9, milioni 12 au milioni 13 ni halmashauri gani hiyo. Nadhani Bara hata halmashauri ya kijiji wanapindukia makusanyo kama hayo. Lakini halmashauri nzima ya wilaya kwa mwaka inakusanya milioni 12, 9 au 13 halmashauri nzima ya wilaya. Kwa hivyo, nadhani utafiti huu wa wenzetu utakuwa una ukweli.

Jengine ni hii tabia ya Serikali Kuu kuingilia shughuli za serikali za mitaa, hili liko wazi. Nadhani wakati umefika sasa pamoja na jukumu la serikali kuzisaidia halmashauri na kuziwezesha, lakini bado wapewe uhuru wa kufanya shughuli zao bila ya kuingiliwa na Serikali Kuu. Nimetaja mambo haya machache sana, lakini ndio ya msingi katika utafiti wa wataalamu, ili nipate pakuanzia.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo na mimi nizungumzie kwa uzoefu niliouona katika uandikishaji wa daftari katika jimbo langu. Kwa bahati nzuri mimi katika uandikishaji wa daftari kwenye awamu ya mwanzo kwenye jimbo langu nilikuwepo na awamu ya pili nilikuwepo.

Katika awamu ya kwanza Mhe. Mwenyekiti, kuna watu walipojiandikisha mimi nilistaajabu, kwa sababu ni Wazanzibari ambao hawaishi Tanzania, wanaishi nje ya Tanzania wala hawafanyi kazi za serikali. Kwa sababu kama Mtanzania yuko nje, lakini anafanyakazi ya serikali au anaiwakilisha serikali anayo haki ya kupata kitambulisho halafu akajiandikisha. Lakini mtu kenda mwenyewe tu kutafuta maisha nje, basi kaja kapewa kitambulisho na kajiandikisha.

Lakini mwananchi aliyeondoka kutoka Jimbo la Mkanyageni akenda kuhamia Jimbo la Mkoani kakosa kitambulisho, Sheha anamwambia wewe hukai hapa kwa hivyo mimi sikupi fomu. Akienda kule Mkoani anaambiwa wewe hapa hukai. Kwa hivyo, utakuta kuna wananchi wengi ndio hawa aliyowazungumza Mhe. Said Ali Mbarouk waliokosa vitambulisho, sio kwa sababu hawana vyeti vya kuzaliwa. Wengine vyeti vya kuzaliwa wanavyo, lakini wanaambiwa wewe bwana kachukulie sehemu fulani, akienda huku anaambiwa kachukuwe huku. Matokeo yake sasa wamekuwa Watanganyika wameandikishwa kwenye daftari la Jamhuri ya Muungano.

Mhe. Mwenyekiti, nina ushahidi tena mtu yeyote akisema twende ukatuoneshe, nitamwambia twende sasa hivi. Nina ushahidi wa watu kutoka Tanga ambao wako Kisiwa Panza, wamekaa pale miezi sita haijafika wamepewa vitambulisho na wameandikishwa katika daftari la wapiga kura. Sasa tukisema mambo kama hayo Mhe. Mwenyekiti, huwa tuna ushahidi na mtu akisema

twende tukawaone, namwambia twende Kisiwa Panza sasa hivi, labda wale watu waondoshwe watoroshwe, lakini hata wakitoroshwa majina yao tunayo na namba za kumbukumbu zao zote tunazo.

Kwa hivyo, hapa tukizungumza waheshimiwa sisi ni watu wazima, tuna dhamana zetu tunaziheshimu na tunachokizungumza kina ukweli. Lakini waheshimiwa mimi niseme kitu kimoja, mtu miaka 70 au 80 umlazimishe cheti cha kuzaliwa ndio apate kitambulisho. Kwa kweli humfanyii haki, kwa sababu hata hawa wengine wenzetu kutoka Tanzania Bara hata vyeti vya kuzaliwa hawana na wanapata vitambulisho.

Mhe. Mwenyekiti, mimi siku moja nilizungumza hapa kitu, labda watu walichukulia utani. Hata hao Masheha wenyewe wengine hawana vyeti vya kuzaliwa. Haya mambo mimi nasema *mindset* zetu zilikuwa hazijabadilika, nina imani zitabadilika. Sasa mimi ombi langu kwa serikali, kwa sababu hii hivi vitambulisho vimeingiliana na utashi wa kisiasa, wacha hawa waliokosa sasa hivi wacha wakose.

Mhe. Mwenyekiti, ombi langu na kwa sababu vitambulisho ni muhimu basi ukishamalizika uchaguzi mimi naomba hawa watu wote waliokosa Mhe. Waziri wapewe. Sasa hivi ni wakati wa uchaguzi tuseme haya wacha tusiwape, lakini ukishamalizika uchaguzi na mambo ya siasa yote yatakuwa hayapo tena, mimi naomba wote wapewe kila aliyekuwa ni Mzanzibari ana haki ya kupewa apewe.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye manispaa ambapo nataka niungane na wenzangu kumpongeza mMkurugenzi mpya. Ni lazima tukubali kwamba anachokifanya kinaonekana. Kwa sababu angalia soko la Darajani, angalia soko la Mwanakwerekwe, angalia maeneo mbali mbali ya mji na angalia uchagu uliokuwepo Darajani, kwa kweli huyu mkurugenzi, mimi simjui lakini nampa pongezi zangu za dhati kabisa. Kwa kweli anachokifanya kinaonekana, namuambia *keep it up*.

Mhe. Mwenyekiti, nataka niulize swali moja kwa huyu mkurugenzi mpya, yeye kafanya jambo moja hili mimi silielewi naomba maelezo Mhe. Waziri atanijibu. Hii *Jamhuri Garden* hapa naona siku hizi pamewekwa mapembea pembea pamependeza, kuna kipindi niliona watu wa mataifa ya nje. Je, hii *garden* ameuziwa nani au amekodishwa nani au pana ubia na nani? Kwa sababu inaonekana kwa hali ilivyo serikali imeingia ubia na kampuni au watu kuiendeleza hii *Jamhuri Garden*. Kwa hivyo, hili naomba nijuwe.

Mhe. Mwenyekiti, halafu jengine nilikuwa nizungumze suala ambalo mwenzangu ameniwahi. Sasa hivi Tanzania Bara kuna miji minne au mitano

yenye hadhi ya majiji. Kwanza kuna jiji la Dar es Salaam, jiji la Mwanza, jiji la Arusha, jiji la Mbeya na hata Tanga nayo sasa ni jiji.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, nikiuangalia mji wa Tanga na Zanzibar basi nauona mji wa Zanzibar ni mkubwa zaidi na ni mzuri na unastahiki zaidi kuitwa jiji. Sasa ni kitu gani mpaka sasa hivi hatujaamua kuupa hadhi mji wetu ukawa ni *city*? Kwa nini mpaka leo Zanzibar *town* tu, lakini nikiangalia naona mji mkubwa, labda vigezo vya kitaalamu ambavyo Mhe. Waziri atatueleza, kwa nini bado mji wetu haujapewa hadhi ya kuwa jiji. Au kwa sababu michirizi ya maji bado hatujaiweza wakati wa mvua maji yanakuwa mengi, inawezekana pengine ni sababu hiyo.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, ninachopendekeza kwa serikali kuiangalia upya mipaka ya mji wa Zanzibar. Mimi sasa hivi naona mji umekuwa, ile barabara kubwa ya kutoka Kiembesamaki kwenda Mtoni isitudanganye ile. Mimi nadhani kuna haja ya kutanua mipaka ya mji wa Zanzibar. Nikisema hivyo najua Halmashauri ya Wilaya ya Magharibi watanilaani, kwa sababu watakosa mapato. Kuna maeneo sasa hivi kuyaita kuwa hayamo katika mji itakuwa hatuyafanyii haki.

Kwa hivyo, mimi napendekeza kwamba mji wa Zanzibar lazima mipaka yake ifanyiwe mapitio. Dar es Salaam nakumbuka zamani ilikuwa lango la jiji lilikuwepo Ubungo, pale ndio unaanza kuingia katika jiji la Dar es Salaam. Lakini sasa hivi mipaka imetanuliwa na imekwenda mbali sana. Kwa hivyo, na hapa ipo haja kutanua mipaka ya mji wetu. Wilaya ya Magharibi naomba wasinielewe vibaya, nina nia njema kuzungumza hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, halafu na mimi nataka nije katika mkoa wangu sasa. Mimi nataka niungane na mwenzangu Mhe. Najma Khalfan kwamba wenzetu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja wameanza kujenga afisi yenye hadhi ya mkoa. Kusini Unguja vile vile. Mjini Magharibi kwa bahati nzuri wao wana bahati ya kuridhi majumba makongwe. Mhe. Abdalla Mwinyi analo na yeye haidhuru pana makaburi mbele yake ya kizamani, lakini analo. Sasa mimi nadhani ipo haja na Afisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kusini Pemba naye akaanza kupatiwa afisi ya kisasa yenye hadhi.

Mhe. Mwenyekiti, hata ile Afisi ya Mkuu wa Wilaya ya Mkoani ni aibu, ukiingia kule nyuma ukienda katika Afisi ya Mkuu wa Wilaya sehemu ya mabanda kama sehemu ya uwani, kwa kweli haipendezi. Mtu kama Mhe. Bi Raya hawezi akaingia hata siku moja, labda apitie maeneo maalum, lakini sio rahisi kupita pale na kuteremka ndani, inatia aibu kuambia hii ndio Afisi ya Mkuu wa Wilaya unaingia na mgeni pale. Kwa hivyo, nayo inafaa kuangaliwa upya.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo nataka kuzungumza kwa haraka haraka ni kuhusu KMKM. Mimi nawapongeza sana KMKM kwa kazi zao. Lakini kuna jambo moja siridhiki nalo, ni kuhusu utaratibu unaotumika hivi sasa wa kukamata magendo Mhe. Mwenyekiti, siridhiki nao. Kwa sababu sasa hivi wakikuta magendo mfano ya karafuu, basi wanachukua zile karafuu, mashine na ile mashua kisha wale vijana wenyewe wanawaachia.

Mimi nadhani Mhe. Mwenyekiti, utaratibu mzuri wa kumkamata mtu ni kumpeleka mahakamani. Kwa sababu kama hukumpeleka mahakamani basi utakuwa wewe ni mwizi, itakuwa chombo cha serikali kimegeuzwa kimekuwa mwizi. Kwa sababu kama wale ni waalifu kwa nini serikali inashindwa kuwapeleka mahakamani. Sasa Mhe. Mwenyekiti, ukitafsiri hapo serikali inaweza ikatiwa hatiani ikaambiwa mwizi, kwa sababu gani? Kwa sababu siku zote muhalifu anakamatwa na kupelekwa mahakamani.

Kwa hivyo, mimi ushauri wangu utaratibu huu uachwe, watakapokamatwa wapelekwe mahakamani. Nadhani huo ndio utaratibu mzuri. Lakini muhalifu haachiwi kisha ikachukuliwa mali yake yeye akaambiwa nenda, huo sio utaratibu hata kidogo wa kuwashughulikia wahalifu.

La mwisho Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima zote nawaomba wenzetu walioko madarakani, nasema nawaomba kwa heshima zote kwamba kambi za ulinzi ziwe za ulinzi zisiwe za siasa, ni dhambi kubwa kuzitumia kambi za ulinzi kwa shughuli za kisiasa.

Nina mfano hai Mhe. Mwenyekiti, katika Kambi yangu ya Chokocho ikiwa hakuna uchaguzi aghlabu kunakuwa na vijana idadi yao tunawajua ni wachache, tunajuana nao ndugu zetu, siwezi kusema ni wangapi, hayo mambo mengine tuyawache hapa hapa, lakini tunajuana. Ukifika wakati wa uchaguzi hali inabadilika. Hilo dogo.

Kuna wakati iligeuzwa ilikuwa kambi ya umoja wa vijana na palikuwa na mafunzo ya umoja wa vijana miezi mitatu, umoja wa vijana wa CCM. Bahati nzuri siku moja nilikuwa na mbunge wangu Mhe. Mnyaa, tukakutana na mtu mmoja pale Dar es Salaam akatuambia, aah! juzi nilikuwa kwenu nilikuja kule kufungua kambi ya umoja wa vijana kule Chokocho katika Afisi ya Bunge pale. Nikasema Muhammad! Huyu mwanamke anatoa siri za watu sasa. Lakini ndio Mwenyezi Mungu alikuwa anatuambia kweli ile ni kambi ya umoja wa vijana.

Kwa hivyo, Mhe. Nyanga kaka yangu nakuomba sana usiruhusu kambi za askari kugeuzwa au kutumiwa kwa shughuli za kisiasa, kwa sababu utapoteza

imani na baadhi ya raia, na raia wote wanatakiwa wawe na imani na serikali yao. Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Hasnuu Moh'd Haji: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa fursa hii ya kuchangia hotuba ya bajeti ya Wizara ya Nchi Afisi ya Rais Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka nimpongeze waziri pamoja na watendaji wake wote katika wizara yake, kuanzia Manispaa, Mabaraza ya miji, KMKM, JKU, Valantia na wengine. Kwa kweli wanastahiki pongezi wote kwa utekelezaji wa kazi zao za kila siku wanazozifanya katika sehemu zao.

Vile vile napenda niwapongeze Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kusini Pemba, Kaskazini Pemba na Wakuu wa Wilaya wote, kwa kuweza kusimamia zoezi zima la uandikishaji wa wapiga kura kule kisiwani Pemba mara hii kwa jinsi walivyosimamia na likaenda vizuri.

Pia Mhe. Mwenyekiti, nawapongeza masheha. Uandikishaji wa mara hii unaonekana ni uandikishaji wa aina yake katika kisiwa cha Pemba, pamoja na maneno yanayozungumzwa, lakini uandikisha na uchaguzi uliopita basi Wakuu wa Mikoa tulipokuwa na vikao kama hivi basi walikuwa hapa hawabaki na walikuwa kipindi chote wako Pemba na Wakuu wa Wilaya halikadhalika. Kwa sababu ulikuwa ni uandikishaji uliojaa vurugu tupu! Mara hii inaonekana uandikishaji umekwenda salama, pamoja na maneno yanayozungumzwa bila shaka ulikuwa ni wa huru na wa haki. Kwa hivyo, sina budi niwapongeze Wakuu wa Mikoa na Wilaya kwa kusimamia hizo shughuli vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka hapo nataka niungane na waheshimiwa wenzangu kumpongeza Mkurugenzi wa Manispaa ya Zanzibar. Kwa kweli manispaa ya Zanzibar inaonekana kwa sasa inaendelea vizuri sana, ila kuna mambo madogo madogo. Mimi nataka nimuambie Mhe. Waziri tatizo la mifuko ya plastiki, tatizo hili la mifuko hii ya plastiki bado halijawezekana ipasavyo. Mifuko hii bado ipo na inauzwa, tatizo liliopo sasa ni kwamba kuna watu wakikamatwa na mifuko hii baadhi yao wanaadhibiwa, lakini wengine hawapati adhabu. Ndio maana ile mifuko ikawa inaonekana kila kipindi bado inaendelea.

Ukienda kununua chipsi mfuko utaukuta, ukenda kununua nyanya mfuko unapewa. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri suala hili liendelee kushughulikiwa. Vile vile namuomba Mhe. Waziri aiangalie *roundabout* inayokwendea Kiembesamaki, ile barabara iliyokata katikati kutokea Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na ikaenda zake Mbuyu mnene. Ile *round about* ilioko pale basi inaridhisha *roundabout* kama ile kuwepo Michenzani.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri na ile *roundabout* ilioko pale Michenzani aiangalie kwa jicho la huruma. Yale maji yaliyokuwa yakiruka juu katika kipindi cha nyuma basi na kipindi hiki yawepo, kwa sababu kwa sasa sijui Mhe. Zakiya Omar analala vipi pale? Kwa sababu nina wasi wasi yale ni mazalio ya mbu. Maeneo yale aliopo Mhe. Zakiya Omar na pale ni karibu sana na mbu ikifika wakati wa Magharibi basi walipo popote huwa wanatoka kutafuta rizki nao.
Jengine hasa linalonisikitisha ni magari. Mhe. Mwenyekiti, ile barabara iliyokata kutoka Michenzani, ikapita katikati mpaka ukapata barabara iliyoelekea Bububu pale wakati wa usiku ukipita utafikiria kuna maegesho ya magari pale. Nakusudia kusema kwamba magari yanalazwa barabarani na kwa kweli vile sio vizuri katika mji wetu kuwa na mambo kama yale.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nielekee katika Afisi ya Mkuu wa Wilaya ya Chake Chake. Mhe. Mwenyekiti, bajeti iliyopita niliizungumza ile afisi na nilivyoizungumza kulitokea vichekesho na nililetewa vikaratasi vingi tu, nilitegemea kuwa lile nililolizungumza kwenye ile afisi angalau ningeona kwa mara hii limetekelezwa. Lakini afisi ile bado iko vile vile haijaulizwa chochote, kile choo nilichoomba kijengwe bado hakijajengwa.

Mhe. Mwenyekiti, lile jumba kwa sasa ni bovu na kwa kweli kufanywa Afisi ya Mkuu wa Wilaya kwa kweli ni tatizo, kwa sababu kuna kipindi hujaa watu vibaya sana na ikinyesha mvua zikipiga radi tu madongo yanaporomoka. Kwa hivyo, na mara hii namuomba Mhe. Waziri basi ile afisi aiangalie.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, nataka niwapongeze watendaji wa Halmashauri ya Mkoani na Halmashauri ya Wilaya ya Chake Chake. Mhe. Mwenyekiti, makatibu hawa wa halmashauri wanafanyakazi wakiwa katika wakati mgumu. Makadirio wanayojipangia ya fedha ambayo kwamba wana uwezo wa kuyakusanya, basi mimi nikiyaangalia, inawezekana yakafika mara mbili iwapo watapewa vitendea kazi na pembejeo halmashauri zao.

Mhe. Mwenyekiti, kuna kipindi nilikwenda sehemu, sitokutajia, ukitaka kwa maandishi nitakupa. Katika kutembea kwangu nikahakikisha kwamba kama ingekuwa Halmashauri ya Wilaya ya Chake Chake wana vitendea kazi na wakaongezewa wafanyakazi, basi wangefanyakazi nzuri kupita kiasa ukilinganisha na sasa hivi wanavyofanya. Ni jambo la kusikitisha sana, kuangalia kware zilizopo Vitongoji na zilizopo Mwambe na kwere zile baada ya kufanyakazi wafanyakazi wenyewe wa Halmashauri ya Wilaya wakaweza kukodisha. Nathubutu kusema kama wanaruhusiwa kuajiri wafanyakazi na wakaweza kupeleka wafanyakazi wao, wakakusanya mapato ipasavyo basi nina uhakika halmashauri zetu zingetononoka vizuri sana na misaada wanayoitoa kwa wananchi vile vile ingezidi.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri Halmashauri ya Wilaya ya Mkoani na Wilaya ya Chake Chake aziangalie. Vile vile nimpongeze Katibu wa Halmashauri ya Wilaya ya Chake Chake kwa kuweza kusimamia jengo lake, haidhuru halijesha lakini sasa hivi kapata jengo jipya la kufanyia kazi. Kwa hili nampongeza.

Mhe. Mwenyekiti, namuonea huruma Katibu wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkoani, ukilinganisha afisi aliyonayo kwa kweli haina hadhi ya kuwa ni afisi. Unaweza ukaitafuta hujui ilipo. Nyumba ni kongwe na ni ya kizamani kama nyumba ya kawaida tu sijui kama sio ya udongo. Kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri kwa hili aiangalie Halmashauri ya Wilaya ya Mkoani kwa jicho la huruma.

Lakini vile vile nataka nimpongeze Katibu wa Baraza la Mji Chake Chake pamoja na watendaji wake wote nao vile vile kwa kusimamia kazi zao kikamilifu na nimpongeze kwa sasa nae vile vile kwa kuweza kuhamia jengo jipya haidhuru halijesha, lakini wanaendelea kufanya kazi zao wakiwa ndani ya afisi mpya.

Mhe. Waziri, katika mji wa Chake Chake sasa kuna tatizo la maegesho ya magari na vile vile kuna tatizo la soko la mboga mboga pamoja na mihogo na matunda pale Chake Chake soko ni dogo na halikidhi haja kulinganisha na mji wa Chake Chake, kama unavyoelewa Mji Mkuu kwa Pemba ni Chake Chake watu wanatoka Micheweni, wanatoka Kojani hata huko Wete kwenyewe wanakuja kutafuta mahitaji pale. Sasa utakuta wafanyabiashara wa mazao wameanza ndani ya soko mpaka kwenye *stand* ya magari, sasa magari hayana nafasi tena ya kukaa unayakuta yako eneo la benki pamoja na iliyokuwa hoteli ya kitalii zamani.

Kwa hivyo ipo haja Mhe. Waziri na soko la mji wa Chake Chake kufanyiwa marekebisho au kutafutwa pahala pengine pakuwekwa soko na watu wakenda kuhudumiwa, Mhe. Waziri lilipojengwa soko la Mwanakwerekwe watu walikuwa wanapiga kelele sana kwa nini waliondoshwa mjini na kupelekwa kule, lakini sasa hivi pale sokoni ukienda kutafuta mlango huupati na hata kama ukiupata basi ni kwa bei kubwa kwa sababu shughuli zinazokwenda pale ni kubwa mno na watu wanaoingia pale ni wengi mno. Sasa ipo haja kwa Pemba ilivyo ikapatiwa soko la kisasa na wafanya biashara walioko Pemba nao vile vile wakaweza kustarehe kuuza biashara zao.

Juzi tu lilitoka suala likauliziwa kuhusu *stand* ya magari na tukaambiwa kuna *stand* itajengwa Mavambarouk tulikuwa tukijiuliza lakini alitokea Mheshimiwa mmoja akapata wasi wasi na akauliza, lakini baada ya kuuliza Mhe. Waziri

ukasema utafuatilia sasa mimi naomba tu hili suala ulifuatilie ipasavyo na ule msongamano wa magari uliopo pale bank uweze kuondoka. Lakini vile vile ikiwezekana basi hapa itakapowekwa *stand* ya magari na hilo soko lijengwe hapo ili wale wananchi waweze kupata mahitaji yao pale na magari yapo pale pale.

Mhe. Mwenyekiti nakushukuru na mimi naunga mkono hotuba hii mia juu ya mia ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Zahra Ali Hamad: Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti na mimi kunipa nafasi hii ya kuchangia, Mhe. Mwenyekiti wewe jana ulikuwa shahidi hapa wakati tunasikiliza kauli ya Waziri kuhusu siku ya mtoto wa Afrika, siku ambayo huwa inaadhimishwa kila mwaka tarehe 16 mwezi wa sita kupitia ile kumbu kumbu ya watoto waliouawa wasio na hatia, waliouwawa na askari wa makaburu katika kitongoji cha Soweto.

Mhe. Mwenyekiti kutokana na suala lile kuwa zito likapelekea nchi kukaa na mikataba mbali mbali ikafikiwa, moja ikiwa ni mkataba wa kimataifa wa haki ya mtoto, katika mkataba ule kuna mambo manne mazito ambayo yalizingatiwa. Moja ikiwa ni haki ya kuishi, haki ya kulindwa na haki ya kushirikishwa.

Mhe. Mwenyekiti, bahati mbaya mpaka leo hii sisi kama Zanzibar ambayo tuko ndani ya Jamhuri ya Muungano tumeridhia hii mikataba ya haki ya kulindwa kwa mtoto lakini haki hii Mhe. Mwenyekiti inavunjwa ndani ya mikono ya serikali,

Mhe. Mwenyekiti Chuo cha Mafunzo mpaka leo hii ninavyokwambia bado hatujaiona haki ya mtoto kulindwa, watoto wetu bado wanachanganywa na watu wazima waliokubuhu Mhe.Mwenyekiti. Mhe. Waziri bahati nzuri katupa takwimu ya wananchi ambao wako Chuo cha Mafunzo na vile vile akatueleza ni watoto wangapi ambao katika mwaka huu wamepitia katika Chuo cha Mafunzo watoto sabiini Mhe. Mwenyekiti, kuanzia miaka kumi na moja mpaka miaka ishirini.

Mhe. Mwenyekiti mchanganyiko uliopo ndani ya Chuo cha Mafunzo ni aibu unatuumiza kama wazazi na mwenyekiti hili ninalolisema sio kama nimehadisiwa nimeliona mwenyewe *live*, tumekwenda juzi katika kamati *round* hii ya mwisho katika kutembea kwetu tukenda katika eneo ambalo wanawekwa watoto wetu ndani ya chumba cha kuwekea watoto tuliwatoa mababa wa miraba saba mpaka nane. Mhe. Mwenyekiti aibu kuna wengine walikimbia wakafungua geti wakenda katika ile sehemu ambayo wanakaa, lakini kuna

wengine walishindwa kukimbia kamati nzima tulikuwepo na wanaohusika wenyewe Makamanda wa Chuo cha Mafunzo walikuwepo.

Mhe. Mwenyekiti aibu wengine wana vipensi, wengine wana vishuka wako tayari tayari Mhe. Mwenyekiti wewe kama mzazi mwanamke unakwenda pahala unaikuta hali kama hii inakujiaje katika akili yako? Hali mbaya tunatarajia watoto wetu wawe vipi, inauma unatarajia watoto wetu wanakwenda pale kama Chuo cha Mafunzo wanakwenda kufundishwa maadili mazuri. Leo mtoto anatoka pale badala ya kuwa mtoto wa kiume anakataa jina lake, anasema mimi sio Salum tena ni Salma.

Mhe. Mwenyekiti tukawaita wale ambao hawakuwahi kukimbia njoo wewe humu umekwenda kufanya nini? Anasema yule uliyemuinamia ni nani ? Anasema yule ni ndugu yangu nilikwenda kuzungumza nae juu ya mambo machafu yanayofanywa humu ndani! Tukamuuliza mambo gani yanayofanywa humu ndani? Anatwambia kamanda anajua huyo mambo ambayo yanafanywa ndio nilikwenda kumnasihi asishirikiane na watu kufanya hayo mambo.

Mhe. Mwenyekiti sasa zamu ya mtoto tukamuita njoo! Akaja , tukamuuliza kaka yako huyu amekataa. Akasema sio kaka yangu mie, ni nani? Ni mtu tu , huwa anakuja humu. Alikuwa anakwambia nini? Mtoto anasugua kuche na kuzitizama kama wari wa kizamani wale walivyokuwa na aibu ukimwambia kitu basi ndio alivyokuwa anasugua kucha yule mtoto. Tukamwambia sema anasema alikuwa ananambia mambo mabaya yule anasema nimekuja kumkataza mambo mabaya yeye anasema alikuwa ananambia mambo mabaya.

Mhe. Mwenyekiti hali hii ndani ya Chuo cha Mafunzo ndani ya mikono ya serikali unatarajia nini mwenyekiti, unatarajia taifa gani Mhe. Mwenyekiti, taifa la kuwa vijana wetu wawe kama sisi mama zao tukivua wanavaa, kwa kweli jambo hili linaniuma na yule kijana mpaka leo hajanitoka machoni mwangu watoto sabiini ndani ya mwaka mmoja vitendo vinavyofanyika jela ni hivi, tunaposema jamani wenzenu tusikilizeni. Mhe. Waziri tusikilize msipande ndege mkiteremka tu mnatuua fanya siku utembelee kule uende bila ya taarifa kwa uwezo wako unaweza kwenda ukaone hali halisi ilivyo, leo watoto tunawapeleka wanavuta unga wakifika kule unga wanavuta vile vile kama kawaida kama wako nje, wanaovuta bangi wanavuta kama wako nje tunaipeleka wapi nchi Mhe. Mwenyekiti? Tunaipeleka wapi nchi?

Mhe. Mwenyekiti la kusikitisha zaidi palikuwa pana mlinzi ambae analinda sehemu ile kwa kawaida tunapokwenda jela unaingia geti la kwanza anakuja askari anakufungulia geti jengine lakini kule kulikuwa *shareware* milango iko wazi, wanaingia wakitoka, kuna askari kama kule akaitwa hata sisi tulikuwa hatukupitia jeshini lakini angalau tuna ile nidhamu ya JKU unajua namna gani

kamanda wako akikwita unavyotakiwa kutii. Kama kajali kaitwa na Mwenyekiti akajikaza kamtizama kama mchuzi wa magozi halafu kaelekea kule kule, kamanda wake kaita kimya kama alinyanyua hatua inaonekana yeye ndiye kungwi pale na alikuwa anajua kwamba naitiwa kitu gani ndio maana hakwenda.

Sasa Mhe. Mwenyekiti niliondoka siku ile nikiwa katika hali mbaya, presha iliniteremka mpaka miguuni nikiwa sioni kabisa na nilikasirika sikutaka kuzungumza lolote, hii hali si ya kuifumbia macho ni hali ambayo tunataka tuelezwe hatua gani za haraka zitachukuliwa, akiwemo huyu askari hatua gani nae kachukuliwa Mhe. Waziri uje kutueleza hapa, hili nataka nilijue.

Jambo jengine Mhe. Mwenyekiti, la huku huku ndani Chuo cha Mafunzo kuna hii sehemu ambayo wanalazia wagonjwa kuna mambo mawili matatu alhamdullillahi tunashukuru kwa sababu tokea niingie hapa barazani kamati ambayo naifanyia kazi ni hii, kwa hivyo najua ni maendeleo gani ambayo yamefikiwa na lipi ambalo bado. Kuhusu habari ya magodoro na dawa za *panadol* afadhali zinapatikana kwa sasa lakini ile sehemu ambayo wanalaziwa wagonjwa bado ni mbaya kwa sababu ni chumba ambacho hakina hata *sealing* jua la mchana wa kutwa na joto la usiku na wale wanaolazwa mle ni wagonjwa na wagonjwa wa aina mbali mbali wa maradhi mbali mbali ambao wanalazwa mle.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti hili pia naliomba Wizara itizame sehemu hii kwa jicho la huruma wawekewe hii *sealing* angalau wale wagonjwa waliokuwemo waone wanapata afadhali badala ya kutolewa katika vyumba vyao kule, lakini ukienda kule hali iliyoko ni kama hiyo niliyoieleza Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti JKU kuna hichi kilimo cha mboga mboga ni mradi ulioanza tokea mwaka 2000 Mhe. Mwenyekiti lakini mradi huu hauwezi kuendelea bila ya kupatikana maji, wenzetu wa Misri wamejitahidi kile ambacho waliahiri kukitoa wamekitoa wataalam wametupa, zana za kilimo wametuletea sasa yale mambo ambayo tunatakiwa sisi wenyewe tuyatimize basi nadhani tujitahidi wapewe hizi pesa ambazo zimebakia ili hili hodhi lipate kukamilika. Utakapokamilika huu mradi itakuwa ni mkombozi nina hakika eneo ambalo wanalo na watalam waliokuwa nao basi kwa Zanzibar tu wenyewe tunaweza kujiendesha kwa matunda bila ya kutarajia matunda mengine yoyote kutoka nje au kutoka Bara.

Mhe. Mwenyekiti, vikosi Pemba Mhe. Said Ali Mbarouk alizungumza, jamani tunapopelekwa Pemba kama Kamanda sio kama umefanya makosa au kama ni adhabu kwako, mahitaji ambayo wanahitaji hapa na kule wanahitaji vile vile . Kwa nini tunawafanya kama ni watoto mayatima leo inafikia mpaka ofisi ya

kamanda wa Chuo cha Mafunzo inaanguka chini kabisa mchangani, mwaka jana tumekwenda imewekewa mwega kama mkungu wa ndizi vile uliokuwa na ndizi kubwa, mara hii tumekwenda ipo chini. Yuko upenuni utafikiri anajificha mvua Mhe. Mwenyekiti, sasa hii sio hali nzuri ni kudhalilishana huku na hii inatokana na kuwa hichi chao ambacho wanatiliwa hakiendi moja kwa moja wanapewa afisi kuu na kufikiria tu wapeleke nini na nini.
Mhe. Mwenyekiti wapelekee wenyewe kuwa na *sub voucher* moja kwa moja ambayo itatoka Wizarani na kupelekewa wao wenyewe watapanga vipaumbele vyao wenyewe, sasa kwa nini tunakwenda hivi jamani iwe mtu akipelekwa Pemba anaona kama kapelekwa motoni kwake ni adhabu sivyo hivi tunavyokwenda.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana. Ahsante. *(Makofi)*

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: *Bismillahi Rahmani Rahim.* Mhe. Mwenyekiti na mimi nashukuru sana kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu kunipa nafasi hii leo jioni na mimi kutoa mawazo yangu, fikra zangu na busara zangu katika kitabu hiki cha hotuba Mhe. Waziri Nchi Afisi ya Rais Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ.

Mhe. Mwenyekiti, hata mimi niungane na Mhe. Zahra Ali Hamad bahati mbayo tu niliwahi kufuta machozi yangu sikuacha yakadondoka kutokana na hii hamasa ambayo ametupa hapa, lakini kwa kweli hili suala namuomba Mhe. Waziri nasema kwa unyonge sana hii hali ambayo kama anavyoisema Mhe. Zahra Ali Hamad basi hili lichukuliwe harua haraka sana. Kwa sababu ni suala la unyanyasaji na kudhalilisha hata kama huyo askari siku hiyo anaambiwa alikuwa kungwi basi angachukuliwa hatua mara moja, kwa asbabu yeye ndio muanzilishi.

Mhe. Mwenyekiti mimi sikutaka niseme kwamba siungi mkono lakini kwa huyu itabidi mimi nipate taarifa rasmi kachukuliwa hatua gani, kwa sababu kaanzisha au kashadidia maovu yafanyike pale sehemu husika kinyume na utaratibu. Hata mimi nilikuwa katika Kamati hiyo Mhe. Zahra Ali Hamad alikuwa mwenzangu kipindi kilichopita lakini kwa mujibu wa sheria za kanuni zetu kila baada ya kipindi fulani tunakuwa tunabadilika, hiyo hali tunaiona kwenye magereza na tunapokwenda kwenye magereza ya wenzetu tunakuta tofauti na hapa kwetu.

Labda tuseme sijui ni ufinyi wa gereza lenyewe na kama ni ufinyu basi watafutiwe kiwanja wapewe ili angalau hilo gereza letu liende na wakati halafu liwe na nafasi nzuri, yasingetokea hayo masuala kama wangelipewa kiwanja hawa na sasa hivi tungekuwa tumo katika hali ya ujenzi, tokea tulivyopiga kelele mpaka leo hakuna kilichofanyika. Mimi mwanzo nilikuwa napiga kelele

nasema mafungu haya yaongezwe zaidi lakini sasa hivi nasema yapunguzwe na sio lengo langu.

Mhe. Mwenyekiti sasa nakwenda kwenye mchangio kwenye ukurasa wa kumi na moja kunako vitambulisho na usajili, mimi niwashukuru sana hawa lakini nini maana ya kusema niwashukuru sana kila mtu anaona vyake wengine wanavaa miwani, wengine hawavai miwani lakini alimradi aone tu. Mhe. Mwenyekiti mimi nina wanangu wawili lakini ukiwaona utasema wale watoto wameshakuwa wakubwa lakini ukienda kwenye vyeti wanaambiwa wale watoto ni wadogo hawakusajiliwa ninao hawana vitambulisho. Sasa hapa mimi nawapa ongezi wametumia haki ambayo tumeisema watoto lazima watimie umri wa miaka kumi na nane.

Mhe. Mwenyekiti juzi Mhe. Moh'd Kombo Mkanga alikaa hapa lakini jamaa wakatuletea vimemori wakatwambia nyie kwenye baraza lenu mmetia mtoto humo kutokana na ile hali yake kuwa mfupi, sasa mimi naona hawa ndugu zetu sijui vipi kasoro ndogo ndogo binaadamu anakuwa nazo, kwa hivyo tuwarekebishe na tuwafahamishe kuhusu hizo kasoro ndogo ndogo zilizojitokeza katika utendaji wao.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea nije katika habari ya Mikoa yetu hususan Mkoa wa Kaskazini niseme tu nawashukuru sana utendaji wao mzuri, maafisa wetu wa kilimo wanafanya kazi vizuri wanaelimisha vizuri sana katika utekelezaji wa ulimaji wa mboga mboga na kama tulivyosema sasa hivi alhamdullilahi tunafika pahali ambapo sasa hivi itafika wakati hata yale matungule ya bara, mabiringanyi ya bara kwa kaskazini tutakuwa hatuwezi tena kwenda kununua kwa sababu wamefanya kazi vizuri sana. Wamewaelimisha wananchi vizuri na wamepeleka mbolea za samadi za kutumia mavi ya kuku, mavi ya ng'ombe hata hizi za magugu nazo kutengeneza wamewafundisha vizuri, nao nawapa pongezi sana kwa kazi zao nzuri wanazozifanya.

Nijika katika Halmashauri ya Kaskazini (B) Unguja nayo vile vile wamefanya kazi vizuri sana, hii ningemuomba Mhe. Waziri ajaribu kukaa na Waziri wa Fedha na Uchumi kuna mambo mengine kidogo ya ada ada ambazo zinakwenda kwenye kodi ya mapato kidogo wawasaidie ili izidi kuimarisha Halmashauri zetu ili waweze kufanya kazi vizuri, kwa sababu Halmashauri wanafanya kazi vizuri sana na wanatumia zile fedha ambazo kwa makusanyo kwa kuwasogezea wananchi matatizo yao kama maji vijijini tayari wanasadiai, mambo ya hospitali hayo mambo ya skuli. Sasa hili tunamuomba ajaribu kukaa na Mhe. Waziri wa Fedha na Uchumi kuna hivi vikodi vidogo vidogo waruhusiwe na wao ili waweze kufanya kazi vizuri.

Mhe. Mwenyekiti nikija katika masuala ya Baraza la Manispaa nalishukuru sana kwa utendaji wao mzuri sana, tena nawashukuru sana kwa sababu hata zile sheria zao zinafanya kazi vizuri hata wakubwa tunapigwa minyororo na tunalipa shilingi elfu kumi, kwa hili nawashukuru sana kwa utekelezaji wao mzuri na hata umuonyeshe katika ukusanyaji wao hapa wamekusanya vizuri katika vianzio vyao na vianzio vyenyewe ni hivyo ambavyo vya minyororo, *packing*. Kwa hivyo mimi nashukuru sana hii sheria waiendeleze tu sio kwamba waheshimiwa wawili walipigwa faini lakini naomba na wengine na wengine waendelee kuwapiga mnyororo akiweka gari hapastahiki apigwe mnyororo mimi naunga mkono sana, kwa sababu hii kupaki ovyo ovyo ni moja kati ya mambo yanayoleta misongamano ya magari na kusababisha maajali.

Lakini vile vile kuna hili suala la kulaza gari barabarani hili naomba na wao wapite wakati wa usiku na wapige minyororo magari yote yanayolazwa sehemu sa njiani ili nao wasisababishe mambo ya ajali kama hayo tunayokataza hivi sasa, lakini kuna picha ambayo tumeonyeshwa hapa na Mhe. Mheshimi mmoja kuna watu sasa hivi wanakuwa wanayaomba magari ya taka, sasa kwa mfano kama hili ambalo lilikutwa maguguni mwenye shamba kaliomba na wengine wenye gari la kinyesi kuna wengine wanapenda mbolea zile. Ndio maana utakuta biringani kama kichwa hivi sasa utashangaa katumia mbolea gani kumbe mbolea hizi hizi, sasa na hili tufikirie mimi nilifikiria magari haya yamemwaga pembezoni mwa nyumba hapa na mimi ningekemea ten asana tu.

Lakini siku hizi kuna watu spesheli wanayanunua haya jamani kanitupieni mimi sehemu fulani ili kwa kutusaidia, sasa ile inakuwa katusaidia ameshaondoa uchafu hapa mjini sasa unakwenda kupelekwa huko mwituni sasa wakifika wanamwaga kwenye shimo sio wanaeneza tu hivi hivi ili kusababisha maradhi, wanachimbia kwenye shimo halafu lile shimo linafukiwa baadae yanabadilika yanakuwa kama udongo huhisi tena kama kile kinyesi unaweza hata ukikikamata kwa mkono kisikudhuru, kwa sababu kimeshageuka imekuwa sehemu ya mchanga. Hili nalo tulione kama sio tatizo sasa hivi, kwa sababu tumeliomba wenyewe ili tuweze kusaidiwa kule kwa kupata hizi mbolea za kisasa.

Mhe. Mwenyekiti, vikosi vya SMZ jamani tuangalie mshahara kidogo, hili tuliseme wenzetu hawa wanakuwa wana wivu sana wakisikia askari wa Muungano wanapata mshahara mkubwa. Pamoja na matatizo yanayotiwa kunako siasa. Mimi sioni jamani kila nchi kuwa na askari wake sio tatizo na sisi askari wetu ni hawa vikosi vya SMZ ndio maana wakaitwa kwa jina hilo. Kule wenzetu askari hawa jeshi, polisi wa Muungano sio wetu wameshakuwa wa Muungano hao. Sasa hawa tunajivunia kwa usalama wetu, wanatusaidia kazi vizuri jamani.

Mimi nafikiria sisi tukisimama waheshimiwa tuwapongeze tena tuwapongeze sana na tulie hasa kwamba mshahara wanaopewa ni kidogo, leo askari mmoja apewe lakini moja kweli inastahiki kwa kazi inayofanywa. Mimi naomba Mheshimiwa haya mafungu yaliyoongezwa bado hayatoshi yaongezwe kabisa. Na kuna ajira yetu ya askari iyengezwe tayari watu wengine wameshastaafu. Kwa nini tusiwaongeze vijana wetu.

Leo utakuta KMKM bado mimi nawaona ni kidogo sana kwa sababu wanataka kulinda baharini na nchi kavu. Kama sasa hivi hali halisi imeshatujia ya ugaidi huo. Mheshimiwa tuwaongeze tusione tabu, tuwaongeze kabisa askari hawajatutosha mshahara, tuwasaidie. Mhe. Waziri kaa na Mhe. Waziri mwenzako mshahara kidogo askari wako. Askari bubembelezwa na askari ndio mlinzi wetu. Askari tukimkera akikereka hali itakuwa ngumu na wale tayari wana mafunzo ya kila aina. Mimi nakuomba waajiriwe na mshahara waongezwe. Hapo mimi ndio nitakuunga mkono Mheshimiwa wangu Waziri. Ukija hapa unambie mshahara umepanda sasa wa askari, nitaipenda sana hotuba yako.

Nije, kwenye JKU hapa katuonesha mambo mazuri jinsi wanavyookoa zao la uchumi kwa hivyo haya masuala madogo madogo tuwasaidie. Waheshimiwa wanapiga kelele masuala ya maji, maji tayari kule sehemu za Chwaka maji yamo kebo kebo, Mhe. Mkuu wa Mkoa yupo hapo atawasaidia sana ndugu zetu. Namjua miye Mheshimiwa mara nyingi sana huwa mstari wa mbele katika masuala kama haya na hasa alivyokuwa analipenda jeshi lake.

Siku moja nilipita njia ya Bambi kati kati kule basi nimekuta bomba limepasuka, nikafikiri kuna bahari ile ya kule imekuja huku kumbe ni maji tu. Maji yapo mengi sana. Kama tatizo ni hilo basi muda tunao wa kuweza kusimamia Mhe. Mkuu wa Mkoa na watu wetu wakaweza kupata mboga mboga, eneo wanalo zuri watasimamisha kila kitu. Tatizo kama ni maji basi hilo limeisha mamlaka waambieni tu Mheshimiwa.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema kuwa mimi leo sitokuwa na mambo mengi sana. Mimi mwalimu wangu amenifundisha masuala ya mpira kwa hivyo narudi nyuma kidogo namuunga mkono Mhe. Waziri pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Kitope asilimia 75.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kama ilivyokawaida yangu sina mchangio mkubwa lakini namuomba Mhe. Waziri hayo nitakayoyazungumza ayazingatie na kunieleza vizuri wakati wa kutoa majumuisho.

Mhe. Mwenyekiti, nitaanzia kwenye kikosi cha KMKM. Kikosi hiki kinahitaji kiangaliwe sana kwa sababu ni kikosi ambacho ni roho ya Wazanzibari wote na kinahitaji kupatiwa zana zilizo kamilifu sio kukaa pale kukamata magendo ya karafuu tu, lakini kipatiwe zana zitakazowawezesha kuwanusuru hata na wao na maisha yao.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mfano sasa hivi tunaingiliwa na mameli makubwa ambayo yanaingia katika bahari kuu lakini wanashindwa kuyakamata kutokana na zana za kuwaza kurafikia kule walipo. Kwa hivyo Mhe. Waziri nakuomba ukiangalie sana Kikosi hiki.

Mhe. Waziri nikija katika jaduweli kiambatanisho namba 5(b), hapa kuna kilimo cha mpunga cha mvua kuna lengo na utekelezaji. Kaskazini Pemba mpunga ekari elfu saba mia sita na sabini na tisa na tukaendelea mpaka tukapata asilimia 107 lakini tukija katika mpunga wa umwagiliaji tuna 470 lengo ekari 155. Pacenti hii Mhe. Waziri naomba uiangalie sana 222 naona bado haijakaa vizuri. Halafu tukaja katika kilimo cha maweni. Mhe. Waziri vile vile *percentage* yake naona bado aiangalie kwa vizuri.

Tukija Kusini Pemba hakuna chochote, sijui ni kitu gani kilichokwamisha hata ikabidi Kusini Pemba ikawa kuna matatizo kama hayo. Tukija mazao tofauti 3,104. Mhe. Waziri pia naomba uiangalie vizuri tukija mwani kwa Pemba nzima kwa kipindi hichi nadhani labda hakuna anayepanda mwani sijui au Mhe. Waziri sijui ilikuwaje.

Tukija kwenye mikarafuu lengo ni asilimia 39,789 utekelezaji 1,760 utekelezaji 42,016 lakini *percentage* Mhe. Waziri iangalie vile vile kwa vizuri bado haijakuwa na uhakika.

Mhe. Waziri nikija kwenye ukurasa wa 54 Baraza la Mji Mkoani naomba ninukuu kidogo;

Kifungu 89. **“**Baraza la Mji Mkoani kwa mwaka wa fedha 2009/2010 liliomba Ruzuku kwa Serikali Kuu yenye jumla ya Tsh 140,000,000/= na hadi kufikia mwezi wa Juni, Baraza lilikuwa tayari limeshapokea jumla ya Tsh. 112,360,000/= sawa na silimia 80.3. Aidha kwa mwaka huo Baraza la Mji Mkoani lilipanga kukusanya jumla ya Shs 14,240,000 kupitia vianzio vyake vya mapato ilivyonavyo, na lilipanga kutumia Tsh. 7,540,000/=”

Mhe. Mwenyekiti naomba kumuuliza Mhe. Waziri, katika hizi Shs. 140,000,000/.= walipata Shs. 112,360,000/= na humu katika kazi zao

walizozipanga walitumia katika vianzio vyao walivyovipata. Je, Mhe. Waziri hizi milioni 112,360/= ziko wapi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niishie hapo. Ahsante.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nashukuru sana kupanga nafasi hii fupi ya kuzungumza kwa uchache kabisa hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ.

Mhe. Mwenyekiti, pili nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa kujitahidi kutoa sifa kwa watendaji wote tokea waliokuwepo mpaka kwa wastaafu lakini kwa masikitiko makubwa Mhe. Rais wetu Dokta Amani Karume hakummalizia sifa yake alisahau kuwa yeye alikutana na Katibu Mkuu wa CUF na kuweka maridhiano ambayo faida yake hata kwenye Baraza tumeiyona. Basi sijui ni kwa sababu kuna CUF au vipi lakini sikuridhika kuwa sifa hii nzito Mheshimiwa hakupewa.

Mhe. Mwenyekiti, hichi ni kitabu muhimu sana na kutokana na Wizara yake imekushanya mambo kadhaa yanayohusiana na Wizara hii. Lakini mimi nina wasi wasi kwa baadhi ya mambo yaliyotiwa katika kitabu hichi kuwa ndivyo na hali halisi ilivyo. Na Ikiwa sivyo basi nasisitiza kama nilivyosisitiza kipindi kilichopita kuwa tunapotoa taarifa kupeleka mpaka kikatungwa kitabu iwe ni taarifa ya ukweli na uhakika.

Mfano tukitizama ukurasa wa 36 hii ni shuhuda Mkoa wa Kaskazini Pemba kifungu 62 namba 4 na 5 ni kifungu hicho hicho kimoja kinaeleza kuwa Mkoa wa Kaskazini moja katika kazi yake ni kushirikiana na Wizara husika kusimamia upatikanaji wa huduma muhimu ya maji na umeme kwa vijiji kadhaa. Hapa kaviandika. Lakini ukiangalia kama hivi:

Kijiji	**Umeme**	**Maji**
Makongeni	Upo	hakuna.
Kivubuni	Hakuna	Upo
Machengwe	nguzo 10 za wananchi	
Mitambuni	Hakuna	Hakuna
Kinazini	Hakuna	Hakuna
Mkanjuni	Hakuna	Upo

Sasa ikiwa anayetoa taarifa anatoa taarifa kama hizi huwa wanapotosho ukweli na kutupa shida hata sisi tunaopiga makelele kuomba msaada tuonekana kama kwamba hatujui yaliyokuwemo katika majimbo yetu. Kwa hivyo naomba masahihishoi makubwa na natoa wito kwa watendaji wa Mkoa wa Kaskazini

kuwa wanaiyona hali halisi ilivyo katika Wilaya ya Wete kama walivyoonyesha wenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, la pili ni hii taarifa aliyoizungumza sasa hivi Mhe. Mwanajuma kuhusu utekelezaji wa Kilimo Pemba nzima. Kwa sababu limeshazungumzwa mimi naomba nielekeze tu. Ni kweli haya mambo ambayo hayamo iwe ni Mkoa wa Kaskazini au Kusini ni kweli au ni taarifa tu imetolewa. Ikiwa ni kweli kulikuwa na sababu gani mpaka wakawa kinyume katika hali hiyo wakati tunapolima sana ndio tunakuza uchumi wetu na kupunguza umasikini. Au kama ilikosewa tuambiwe hiyo hali halisi ilivyo.

Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba kwa ruhusa yako kuendelea kwa kuzungumza na taasisi hii inayohusiana na vitambulisho vya Uzanzibari Mkaazi. Kila mmoja katoa maelezo kwa maoni yake na mimi natoa kama nilivyoona katika jimbo langu. Kwanza tuelewa kuwa kitambulisho cha Uzanzibari ukaazi kwa wakati tuliokuwa nao hivi sasa kina umuhimu wa aina yake kwa shughuli zote za binaadamu ambazo zinahusiana na vitambulisho. Mfano huwezi kupata leseni ya biashara kama huna kitambulisho hiki. Huwezi kupata paspoti kama huna kitambulisho hiki hata kuisajili simu ni lazima uwe na kitambulisho hiki. Mhe. Waziri wizara yake ndiyo inayohusiana na utoaji wa vitambulisho hivi.

Mhe. Mwenyekiti, tukitizama Katiba yetu ya Zanzibar ukurasa wa 3 kifungu cha 4 kinaeleza kuwa naomba kunukuu.

Kifungu cha 4 “Katiba hii ni Katiba ya Zanzibar na itakuwa na nguvu za Kisheria nchini kote isipokuwa kutokana na kifungu cha 80 ikiwa Sheria yoyote inayotofautiana na Katiba basi Katiba hii ndiyo itakayokuwa na nguvu ya sheria hiyo na itakuwa batili kwa kiwango kile ambacho kinahitilafiana”

Mhe. Mwenyekiti, katiba hii hii imeeleza kuwa

“Mtu yoyote ambaye ni Mzanzibari kwa mujibu wa sheria hii iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi anawajibika kupata haki zote zinazohusika kwa mujibu wa sheria zilizowekwa”

Kifungu cha 7” “Mzanzibari yeyote aliyetimia umri wa miaka 18 na ambaye hakuzuiliwa na sheria yeyote ile kupiga kura atakuwa na haki ya kupiga kura katika uchaguzi wowote ule uliopo Zanzibar”

Mhe. Mwenyekiti mwaka wa 2010 ni mwaka wa uchaguzi na ni mwaka peke yake wa historia uliyokuwa una chaguzi mbili, kuna uchaguzi wa kura ya maoni kupata maoni ya wananchi kuikubali au kuikata serikali ya ummoja wa kitaifa ambayo naamini tutaikubali kwa wingi na kuna uchaguzi mkuu wa 2010 mwezi wa Oktoba, kama tunavyojua.

Mhe.. Mwenyekiti, jambo la kusikitisha huwezi kuingizwa katika daftari la kupigia kuwa kama huna kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi wakati wapo wengi waliingiwa hapo mwanzo matokeo yaliyotokea katika uwandikishaji na nimeshuhudia mwenyewe katika jimbo langu, ilikuwa kwanza kuna wengi, tayari walikwisha kupiga kura, lakini hawakupata kujiandikisha tena kupiga kura eti tu kwa sababu hawakuwa na vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi.

Wanasheria wanasema ikiwa ni kweli ilikuwa *there is no rule with out exception*. Namuomba Mhe. Waziri kwa hili wale wote ambao wamekwisha kupiga kura kadhaa huko nyuma tufuate agizo la Mhe. Raisi wetu kipenzi kuwa kusiwe na sababu za kukoseshwa kupiga kura labda kuwe na sababu za msingi za kupoteza kupiga kura kwake. Lakini kitambulisho cha Mzanzibari Ukaazi isiwe ni sababu. Hawa hawana makosa tuliwapa, wamepiga kura kutekeleza demokrasia yao hakuna sababu yakuwazuia.

Mhe. Mwenyekiti, masheha wetu ndio watumishi wetu wakubwa katika serikali na katika maeneo ya Shehia na ndio wachangiaji wakubwa kuivunja hii haki. Sheha kapewa eneo dogo tu Shehia anamjua kila mtu na wazazi wake pengine kahusiana naye. Lakini sijui ikiwa katiba ndio yenye nguvu za mwisho ile kauli ya kupinga pinga mpaka ikabidi kupinga yenyewe maana hata ikawa haina msingi kaipata wapi.

Mfano mtu kazaliwa, kaleta cheti chake kidogo bahati mbaya wazazi wake pengine kwa mazingira ya Pemba ilivyo hawakuwahi kwenda kuandikisha. cheti *register* anasema kama huna cheti cha *register* cha kuzaliwa huandikishwi na wengi mpaka leo wapo waliokoseshwa haki hiyo.

Nashukuru maana mtu husema kweli natoa shukurani za dhati hasa kwa Mkuu wetu wa Wilaya ya Wete alikuwa mara nyingi tulikuwa tukimshika katika matatizo haya na akatusaidia kwa kiasi fulani alau kupunguza ule ukali wa kukosesha watu haki zao. Kwa hilo namshukuru na nampongeza. Sasa ninaloomba Mheshimiwa tunaingia katika uchaguzi na tunaingia katika uwamuzi ambao ndio wa mwanzo na muhimu kuliko mambo yote ni ya kura ya maoni.

Hawa watu wakati ni Wazanzibari tu nawajua, tusione tu kwa kukosa kitambulisho cha Uzanzibari Ukaazi kuwa watakosa kupiga kura, lakini pia

tunawakosesha na haki zao zote. Mimi sikubaliani mia kwa mia na wale waliosema angalau wapewe baada ya uchaguzi mimi nasisitiza uwezo uwepo hawa watu wapewe vitambulisho vyao vya Uzanzibar Ukaazi au wapewe barua rasmin kama upigaji picha hauwezekani kwa wakati huu *at list* waitumie hii haki yao ya kidemokrasia.

Mhe. Mwenyekiti, kidogo nizungumzie Baraza la Mji Wete. Pale wetu huwa siondoki mara nyingi huwa natembea na nayajua mazingira. Mji wa Wete tunaujua ukitoka Chakechake unaofuata ni mji wa Wete kwa bahati mbaya pamoja na jitihada kubwa iliyopo katika kufanikisha shughuli zao za kiserikali lakini hali ni ngumu sana kwa utekelezaji kwa upande wao. Kwa mfano gari liliopo linalotumika hivi sasa ni spana mkononi leo linafanya kazi kesho halifanyi kazi. Siku moja tulikuwa tunalipeleka mazikoni tulilazimika tubakie na maiti wetu njiani mpaka likatokea gari za ZSTC tukabadilisha. Hilo ndio gari la Baraza la Mji Wete.

Kwa hivyo Mheshimiwa kwa vyovyote vile ilivyo tufanye kila inavyowezekana angalau pale wete papatikane angalau magari mawili yanayoweza kufanya kazi kwa maslahi yetu na taifa letu. Kuna kazi za usafi na kazi nyengine Mheshimiwa unajua zaidi kuliko mimi ninayeeleza.

Mhe. Mwenyekiti, Wete tumebahatika tuna Bandari na tuna makushanyo mengi kwa sababu ni mji. Lakini kwa sababu mimi ni mwenyeji sana pale Wete linalonisikitisha sana ni kuona baadhi ya wale wanaosafisha mjini ndio wanaotoza kodi, hata ile *personality* ya kumwendea mtu hana kutokana na zile kazi zake. Kama hivyo ndivyo ningelikuomba Mheshimiwa ushauriane na watendaji wetu wa Wete ili kupata ajira kwa watu wenye uwezo wa kukushanya mapato ili mapato yapatikane kwa maslahi yetu sote.

Mapato yanayokusanywa yanatusaidia sana katika sekta kadhaa, kwa hivyo kutokukusanya mapato maana yake ni kuturudisha nyuma. Kwa hivyo hili naliomba sana lichukuliwe hatua.

Mwisho nataka kusema sijui hivi majuzi lakini uwongozi wote wa pale Wete hapana Mwanasheria. Taasisi iliyokuwa haina mwanasheria sijui inakwenda vipi. Kwa hivyo kama hajatokea kuajiriwa ikiwa kauli yangu ni kweli ningeliliomba na hili pia lichukuliwe hatua. Mengine Mheshimiwa utayaona zaidi katika ufatiliaji.

Mhe. Mwenyekiti, nimeangalia kwa muhtasari hapa Mhe. Waziri ametuomba tumuidhinishie pesa nyingi sana bilioni ishirini na nane milioni mia tatu na ishirini na tisa laki saba na sabini na tatu alfu kwa wizara nzima. Lakini katika mgao wake vikosi vya SMZ kama hesabu yangu ni sahihi imetengewa bilioni

kumi na tisa milioni mia mbili na thalathini na moja na laki tatu. Hii takriban inakaribia arilimia 68 ya fedha yote ya Wizara.

Wakati kwa hesabu hizo taasisi zote za Wizara zilizobakia ni bilioni tisa, milioni tisini na nane laki sita na sabini na tatu alfu, takriban ni 32%. Sasa sijui asilimia hii 32% itamuwezesha vipi Mhe. Waziri kuweza kumudu uendeshaji wa taasisi zake za serikali tukiacha hivyo vikosi vya SMZ. Kwa vile Mhe. Mwenyekiti, hii wizara ni muhimu sana inafika mpaka kwenye wananchi kwa kutumia masheha na taasisi zake takriban ukiasha hivi vikosi vya SMZ ambavyo vinaombwa kuongezewa fedha ni nyingi na pesa ni kidogo sana.

Ninalomuomba Mheshimiwa ama azidi kuomba fedha zaidi na ikiwa hapana budi afanye *structuring* ili tuone kuwa na hizi taasisi za Wizara yake tukiacha vile vikosi vya SMZ zinapatikana fedha za kuweza kujiendesha na katika shughuli zake.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru.

Mhe. Ali Moh'd Bakari: Mhe, Mwenyekiti, na mimi nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kufika hapa tukiwa katika hali ya uzima. Pia nimpongeze Waziri Kivuli wa Wizara hii Shekh Abdalla bina Juma kwa maelekezo yake ambayo yatamsaidia Waziri katika kusimamia majukumu yake ya Wizara ya Nchi, Afisi ya Raisi na Vikosi vya SMZ.

Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa ufupi sana nataka nigusie kidogo katika Afisi hii ya Usajili wa Vitambulisho. Kama ilivyokawaida kwamba kila Mzanzibar anayo haki atakapofikia umri wa miaka 18 kupewa kitambulisho kile ili aweze kuthitibisha Uzanzibari wake. Lakini leo ukiacha umri wa miaka 18 tunao watu wa zaidi ya miaka 26,22, hawakupata haki hii. Ilhali hapa imeelezwa miaka 18 inatia mashaka sana kwamba amenyimwa fursa hii na wasimamizi wakubwa ni masheha. Masheha imekuwa ni kikwazo kikubwa sana juu ya kuwapatia watu haki zao. Ndio maana unakuta kunakuwa na mashakili ya namna mbali mbali kuwapelekea watu kukosa haki zao.

Leo Mhe. Mwenyekiti, nilikuwepo Benki BME pamoja na Kamanda Omar nilikuwa watu wengi wamerudishwa kwa sababu hawana vitambulisho vya Uzanzibari, wakatakiwa wathibitishe Uzanzibari wao. Wakawa hawana vitambulisho vile wakarudishwa wakaambiwa basi walete hata leseni ya udereva na vitu kama hivyo vitakavyoweza kuwathibitisha kwamba wao ni Wazanzibari.

Sasa ukishakumnyima mtu haki yake hii maana yake sio kwamba atakosa kupiga kura tu lakini kuna vitu vingi atavikosa. Sasa hivi mbali na hii kupiga

kura kwamba labda kuna mpango wa kupunguza idadi au vyovyote vile. Lakini hata ukenda kuchukua tiketi sasa hivi kama unasafiri kwenda Bara au popote pale kwa hapa Unguja unaambiwa uwe na kile kitambulisho. Sasa ikiwa huna kitambulisho hukosi kupiga kura tu utakosa mambo mengi. Jambo ambalo kwa kweli itakuwa tunawadhulumu watu.

Mimi nadhani suala hili lisichukuliwe kisiasa na watu waliangalie kwa mbali zaidi kwamba, kumpatia fursa hii ambayo hapa tumekuja kuipitisha na tuling'ang'ania kuwa kitambulisho kisiwepo katika muundo huu. Lakini ndio tukazidiwa nguvu na madala yake kikapita.

Lakini sasa baada ya kupita inaonekana kwamba watu hawatendewi haki. Kwa hivyo, hapa tunachokuja kukizungumza ni kitu chengine na tunachofanyia watu kitu chengine.

Sasa mimi nadhani Mhe. Mwenyekiti, waziri naamini anayo habari kwamba watu huko chini hawapati haki zao hizi. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri afuatilie ili Wazanzibari wote wanaostahiki kupata haki hii wapate. Kwa sababu kama nilivyokwishasema pasiangaliwe suala la kwenda kupiga kura tu, lakini tuangalie na mambo mengine ya msingi ambayo mtu anapaswa kuyapata kupitia hicho kitambulisho.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika Manispaa. Mnadhimu wangu wa Kambi ya Upinzani, Mhe. Haji Faki Shaali wakati anachangia alimsifu Mkurugenzi wa Manispaa. Na akasema hamjui lakini ana kila sababu ya kumsifu kwa sababu ya mabadiliko ya aina mbali mbali ambayo yeye anayaona hapa Unguja yapo.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, mimi nimuulize Mhe. Waziri kama kawahi kusafiri katika nchi yoyote ile duniani ama bado. Kwa sababu huu mji wetu hivi ulivyo leo basi hakuna mji wowote duniani ulio kama hivi, licha ya usafi unaoambiwa upo, ndio maana nikamuuliza Mhe. Waziri, mimi waziri ni rafiki yangu lakini nimeuliza swali hilo kuwa kawahi kusafiri akaulinganisha usafi wa mji huu na mji mwengine wowote duniani labda inawezekana. Lakini mimi naona kwamba mji wetu ni mchafu mno tena kwa kiasi kikubwa na wala hakuna cha kukiringia hata kimoja.

Kama Mkurugenzi kaja kuondosha uchafu majaa anakwe kutupa maeneo mengine inawezekana ndio labda Mhe. Haji Faki akaona amsifu. Kwa sababu ukifanya jambo moja hata kama ni dogo lililokuwa linaudhi watu ukaliondosha basi unastahili pongezi. Kwa hilo labda ndio Mhe. Haji Faki Shaali akaona ampe hizo pongezi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli mji wetu ulivyo hauna kivutio popote na chochote kile ukilinganisha na baadhi ya maeneo ambayo tumewahi kwenda tukaona wenzetu jinsi gani wanavyosimamia miji yao. Kila mmoja anachukua jukumu na dhamana ya kusimamia eneo ambalo analifanyia kazi na hivyo ukawa ule mji una kivutio kikubwa. Siku moja nilizungumza hapa nikauliza hata bustani sisi wataalamu wa kusimamia hatuna, nikaambiwa eti bustani ya Forodhani.

Mhe. Mwenyekiti, tulikwenda safari nyingi na uliona ni jinsi gani miji ile watu wanasimamia usafi na mazingira ya miji yao, mpaka wewe mwenyewe mgeni kutema mate barabarani unaona shida, unaona kama utaonekana kwa sababu ya ule usafi ambao upo katika mji. Leo hapa uchafu ukipita asubuhi hapa kwenye miti mbele nyuma kuna watu wanakuja wakimwaga uchafu pale, sehemu ambayo ndio kitovu cha mji, watu wanapita hapo, wanafanya shughuli zao hapo, uchafu moja kwa moja unaletwa pale. Sasa imekuwa ni kitovu cha uchafu hapo halafu watu wanakuja kuchukua wanakwenda kupeleka maeneo mengine.

Sasa nadhani katikati ya mji hakumwagwi uchafu, katikati ya mji unatafutwa uchafu na unachukuliwa kupelekwa maeneo mengine huko kwenda kutupwa. Lakini hapa haiwi ni kitovu cha kuweka uchafu kwanza halafu ndio ukaja ukauchukua ukaupeleka maeneo mengine. Kwa kweli mimi sijawahi kuona katika miji ya watu ambayo imeendelea zaidi ya huku kwetu. Hapa watu kila siku wanasafiri tena wanakwenda miji mbali mbali, kwa nini hatujifunzi, kuona hatuoni basi hata kusikia hatusikii? Kwa sababu unaweza kwenda pahala ukawa huoni lakini unaweza kusikia kwamba pahali pale ni safi halafu ukaja ukawaambia watu wako kwamba, eneo fulani nasikia ni safi hebu shughulikieni watendaji wangu.

Kwa hivyo, Mkurugenzi mimi sikujui, lakini bado unalo jukumu zaidi la kuhakikisha kwamba angalau huu mji wetu wa Unguja umekuwa safi na kivutio. Kwa sababu kila siku mimi nasikia kuwa Unguja ni kivutio cha watalii, hawa watalii wanaokuja humu wanakuja kwa sababu kujua mji na mambo yao mengine tu, lakini hakuna kivutio hapa. Kama kuna vivutio vya kumvutia mtu ndio aje basi asingekuja mtu hata mmoja hapa, kwa sababu ya huu mji ulivyo hasa ukizingatia miji ya wenzetu ilivyosafika, bustani za kuvutia na vitu kama hivyo. Mhe. Mwenyekiti, bado zipo changamoto nyingi za Manispaa ya mji wetu ili kusudi kwenda sambamba na ushindani wa miji mingine.

Mhe. Mwenyekiti, nataka kidogo niingie katika Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni. Nimekuta hapa kuna usaidizi wa kituo cha afya Bule na kusaidiwa miradi ya jamii. Sasa mimi nataka nijue ni jamii gani iliyosaidiwa. Kwa sabau sijaona kwamba kuna maeneo fulani kuna kitu kimetolewa na kiasi gani

kimetolewa. Hapa pametajwa pesa za ujumla wake tu, lakini sioni kwamba kuna kijiji kimetengwa au mradi ulifanywa katika eneo fulani.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri katika hili nakuomba san auje unisaidie kwamba ni kijiji gani na eneo gani ambapo pesa hizi zilitumika pamoja na hawa wanafunzi ni wanafunzi gani, kwa tukio lipi na hayo majanga yaliyotajwa ni majanga ya aina gani. Hivi karibuni kule kwetu kulinyesha mvua kubwa sana lakini sikuona msaada na kuna nyumba nyingi zilipata athari kubwa, lakini sikuona msaada uliotoka labda kwa Halmashauri au eneo jengine lolote lile. Sasa nilitaka nibainishiwe msaada huu umekwenda wapi?

Kwa sababu siku hizi kuna mtindo wa watu wakishakula pesa huko basi huchukua namabari zile wakazileta kwenye vitabu wewe ukazisoma hapa ukaona kitu hicho kimefanyika, ilihali kumbe hakuna kilichofanyika. Na wewe si kweli kwamba kila kitu utakijua. Kwa sababu ili kitu ukijue lazima ukisimamie, haiwezekani kwamba vitu vyote hivi wende ukavisimamie. Lakini nategemea kwamba watembeaji wako waweze kusimamia na kuthibitisha haya ambayo wanakuletea.

Mhe. Mwenyekiti: La mwisho hilo malizia.

Mhe. Ali Moh'd Bakari: Basi kama nimalizie nitakwenda huko jela. Mhe. Mwenyekiti, kumezungumzwa masuala mengi hapa na Mhe. Zahra Ali Hamad na Mhe. Makame Mshimba Mbarouk. Wakati mimi mwenyewe binafsi niko katika Kamati ya Katiba, Sheia na Utawala, tulikwenda miaka miwili iliyopita na hii hali ambayo ameizungumzia Mhe. Zahra hapa tuliikuta. Lakini mimi nimepata wasiwasi mmoja, hawa askari wanawafanya nini hawa watoto mpaka ikawa wao wanashindwa kuwatenganisha? Kuna tatizo gani kwani kule? Kwa sababu isije ikawa kuna michezo mibaya wanaifanya hawa halafu wakawa wanashindwa kuwatenganisha. Ni kwa sababu gani Mhe. Mwenyekiti?

Sisi tulipokwenda kule kilio hiki kilikuwepo na wao tukawaambia chini ya Mwenyekiti Mhe. Haji Omar Kheir na wakakubali kwamba watatenganishwa. Lakini leo ni miaka miwili ishapita hawatenganishwi watoto hawa na manjemba yale na mengine yameingia jela kwa kubaka watoto wa watu humo humo mitaani, halafu mtoto huyo unakwenda kumpelekea kule kule. Sasa huko ulikwenda kumtenganisha na jamii kwa vipi halafu mtoto yule yule unakwenda kumpeleka kule kule itakuwa umefanya kazi gani?

Sasa isijekuwa kuna michezo inachezwa kwa kushirikiana na hawa mnaowaita ni askari jela halafu wakitoka tukawa tunalaumu. Lazima watoto watenganishwe hili si suala la hiyari Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, pale pasiangaliwe, kama vile hospitali anaweza kuingia mtu yeyote tu na yeye akaenda kufanya vitendo vile vile, akija akiseka aa, mnanifanya vipi, haya wewe ulifurahi nini. Sasa hili si jambo la kulifurahia. Mimi nadhani serikali lazima ione kwamba ipo haja na lazima ione kuwa hakuna sababu yoyote ya kumchukua mtoto mdogo ambaye hana kosa lolote kaingia pale kibahati mbaya akenda akawekwa na jambazi sugu ambalo limeingia pale kwa makosa hayo halafu tukamwambia hiki chakula kula. Kwa nini asile na huko katokea kwa sababu hizo hizo.
Mimi nadhani suala hili Mhe. Mwenyekiti, waziri aliangalie kama linatendeka na linatendeka hili suala, ujaribu kulifuatilia halafu maeneo hataka mama hatuna sehemu za jela, lakini maeneo ya kuwaweka watoto wale wakahifadhika katika mtindo huo wa ulinzi yapo tele. Wale watoto wahamishwe mule ili wapate manusura kama alivyosema Mhe. Zahra, kwamba itafika wakati hatuna watoto wa kuwatumia. Leo watoto wakitoka kule wakija huku…

Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru ingawa na mimi nilikuwa nianzie hapo hapo alipomalizia Mhe. Ali Moh'd Bakari kwa uzito na unyeti wa suala hili lililojitokeza Mhe. Mwenyekiti, kama wazazi, sisi kama Wawakilishi wa wananchi lazima tupeleke kilio chetu mbele ya kiti chako, kwamba ifike pahala katika hili serikali ichukue maamuzi.

Ni wakati sasa umefika kama wazazi tunataka tuone hatua madhubuti zinazochukuliwa na serikali kwa hawa vijana wetu. Kwa sababu mtoto wa mtu yeyote mle anaweza akenda kuna hili na lile, msi hili ana lile. Leo haipendezi na hata kama ni wewe haiwezi ikakufurahisha kumuona mtoto wako akifanyiwa kitendo kama hicho. Kwa hivyo, kama wawakilishi wa wananchi, kama wazazi tunaiomba serikali katika hili basi itakapokuja hapa itupe jawabu namna gani watatekeleza azma ya kuwatenganisha vijana hawa na watu ambao washakubuhu katika masuala haya.

Mhe. Mwenyekiti: Naamini Mhe. Waziri msikivu ameshalisikia hilo.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Mwenyekiti, nataka nianze kwa kueleza kwamba sura ya nchi yoyote inaonekana kwenye miji yake mikuu. Nchi yoyote ile duniani utakapokwenda sura yake kama hii ni nchi yenye kuendelea, iliyokuwa si ya kuendelea, nchi yenye wastaarabu, nchi yenye watu wasiokuwa wastaarabu, utaiona katika miji yake mikuu. Hali ya miji mikuu ya nchi inachangiwa sana na hali ya usafi, hali ya mpangilio wa majengo, hali ya barabara, hali ya bustani na vitu vingine.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli katika nchi yetu hii ya Zanzibar sifa hiyo inakosekana na inakosekana kwa kuwa Serikali zetu za Mitaa ambazo ndio zenye wajibu mkubwa wa kuhakikisha mambo hayo, bado hazijakaa katika nafasi iliyokuwa ni nzuri. Leo serikali zetu za mitaa zinaonekana kwamba ni sehemu tu ya kuwakaba wafanyabiashara na watu wengine kwa ajili ya kukusanya kodi, yale mantiki ya kuhudumia jamii, mantiki ya kusafisha miji na vitu vingine kwa kweli bado havijakaa katika hali ambayo inahitajika.

Hili hatuwezi tukalaumu moja kwa moja ni kwa sababu serikali zetu hizi kwa kweli mara nyingi zinakosa uwezo wa kimapato, fedha wanazoingiziwa kule ni kwa ajili ya matumizi ya ofisi na mishahara tu, lakini yale mambo hasa ya kufanya maendeleo na yakaonekana, kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, na kwa kuwa serikali hizi vyanzo vyake vya mapato ni kidogo sana, basi ndio zikaonekana hazijafanya vya kutosha katika eneo hilo.

Lakini pamoja na hilo, tuna tatizo la kukosa wafanyakazi ambao wana sifa, wafanyakazi wengi wa Manispaa hizi pamoja na Mabaraza ya Miji hawana sifa. Zamani ilikuwa ikionekana kwamba ni pahala tu watu wote kwenye wapigadebe wanataka kuajiriwa peleka Baraza la Mji, peleka Halmashauri, watu wamemaliza muda wao katika kazi washakuwa wazee, peleka kwenye Mabaraza ya Miji. Sasa hali hiyo imepelekea sehemu hizo kukosa watu wenye sifa katika utumishi.

Mhe. Mwenyekiti, katika kamati yangu ya *PAC* mara nyingi tukienda katika Halmashauri tumekuwa ni mashahidi wazuri, kwamba hata matumizi mazuri ya fedha za umma yanakosekana katika serikali hizi za mitaa.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, katika hilo basi ningependa ile rai ya serikali. Kwa sababu tufanye nini? Kinachokosekana inaonekana ni kwamba mageuzi hasa katika serikali zetu hizi za mitaa bado hayakuwepo na serikali ilituahidi mara nyingi. Nafikiri tangu mimi niingie katika Baraza hili serikali lugha hiyo inakuwa ni ya kawaida kwamba kuna *reform*, kuna *reform*, lakini huu ni mwaka wa tano zaidi kwamba *reform* hiyo haijaletwa mbele ya Baraza hili kupata baraka. Sasa sijui lini serikali italeta mageuzi hayo ya Serikali za Mitaa ili angalau basi isilingane na serikali za nchi za nje angalau tuige tu wenzetu wa Bara.

Wenzetu wa Bara sasa hivi wanafanya vizuri sana katika Serikali za Mitaa. Takriban mambo mengi ya maendeleo katika jamii yanatekelezwa na Serikali za Mitaa. Sasa kwetu sisi ni donda ndugu hatujui serikali lini watalileta hilo.

Tatizo jengine mimi nafikiria kwa fikra zangu, Mhe. Mwenyekiti, kutembea ni kusoma, ukiwa hujasoma tembea. Sisi tulipokwenda angalau kijisafari kidogo

leo kila mmoja anazungumzia kwa sababu tuliona. Sasa utawezaje mtu anatoka Chake Chake, Unguja mbali Tanga halafu useme afanye vitu kama vya watu na hajaonapo kitu utasemaje afanye kazi? Sasa mimi niiombe serikali wale watu wengine hawana elimu basi angalau wapiti wende wakajifunze hata kama wana elimu. Wakajifunze namna watu wanavyosimamia miji yao na kuipamba angalau makatibu.

Leo ukisikia Katibu wa Halmashauri ya Baraza la Mji kenda mbali basi kenda Tanga, Tanga kenda kujifunza kitu gani? Labda barabara mbovu. Kwa hivyo, naiomba serikali angalau kila mwaka au miaka miwili iwatoe wale Makatibu wetu wa Halmashauri na watendaji wengine wende wakajifunze.

Mhe. Mwenyekiti, la pili ni Vikosi vyetu vya Ulinzi, Vikosi vya SMZ. Mimi naunga mkono sana vikosi hivi, naunga mkono kwa sababu sisi ni waumini na tunaamini na ndivyo ilivyo kwamba Zanzibar ni nchi, hatuwezi kuwa na nchi iliyokuwa haina vyombo vya ulinzi. Kwa hivyo, kuwepo kwa vyombo hivi ni kuthibitisha kwamba Zanzibar ni nchi. Mara nyingi tumekuwa tukilalamika sana na tutaendelea kulalamika. Tatizo linalojitokeza ni namna tu ya utumiaji wa vyombo hivi vinatumika vibaya vikosi hivi hususan katika nyakati za uchaguzi.

Lakini naamini kwamba tukijaaliwa kwa hali hii iliyoonekana *Inshaaallh* mara hii vikosi vitakwenda katika hali nzuri. Na watu wa vikosi watusikie kwamba sasa hivi tunabadilika na wao wabadilike, waache kutumiwa na wanasiasa hata *CUF* waweza kuwatumia hatusemi CCM tu kwamba watawatumia, hata *CUF* tunaweza kuwatumia lakini wakatumika vibaya. Kwa hivyo, wasitusikilize sisi wanasiasa. Kwa sababu kuna siku wanasiasa tutakaa katika meza moja wao tutawanyooshea vidole.

Kenya hilo limetokea na linaendelea kutokea, watu wanakaa katika meza moja sasa hivi wale wote waliokuwa wanahusika na vurugu. Sasa naomba Mhe. Mwenyekiti, katika hili serikali ifanye mageuzi katika vyombo vyetu. Vyombo vyote vya dunia ya sasa vya ulinzi vinatakiwa tuwe na majeshi kidogo lakini lililofunzwa vyema, ndio sera za kiulinzi zinavyokwenda katiak dunia. Unakuwa na namba ndogo ya askari lakini uliowafunza vyema, tunakuwa na namba ndogo ya askari lakini wenye vifaa na zana za kisasa huwezi kila siku wewe ukaongeza namba tu.

Leo Mhe. Najma Khalfan anazungumzia kwamba tupewe kiona mbali akishaona mbali keshakiona cha mbali atakwambia vipi na hawezi kwenda. Askari ana mtumbwi atakwenda vipi? Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, serikali ifanye mageuzi ya msingi katika vyombo hivi na moja kati ya mageuzi ya msingi vijana wetu wale. Tuna kikosi cha KMKM hiki ni kikosi sisi ni visiwa,

lazima tuwe na Jeshi la Majini hii ni muhimu. Lakini vile vile tuna jeshi la kuzalisha uchumi tunataka tuone namna JKU wanavyosaidia serikali katika kujenga uchumi.

Tuna Valantia wenzangu walizungumza hawajui kazi zao na mimi sijui kazi zao, tunahitaji Valantia tuone nao wakipangiwa majumu wasiranderande tu, hawa wanawezekana wakawa ni kikosi kama walivyozungumza hawa wakawa ni askari wetu, wabadilisheni wawe ni askari wa kawaida. Lakini vile vile mafunzo tumesikia na tunaomba Jeshi la Mafunzo nalo lichukue hatua ili Vyuo vya Mafunzo viwe ni mafunzo kweli kweli ni yaachane kuwa ni Magereza.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho kabisa nataka niipongeze Idara ya Vitambulisho. Kama walivyosema Idara ya Vitambulisho wanatoa vitambulisho ambavyo ni vya kimataifa na vimepata sifa ya kimataifa. Na sisi tukubaliane navyo hivyo, hiyo ni sifa yetu, ingawa Idara ya Vitambulisho inakosa saifa ya kuwapa watu haki zao za kuwapa vitambulisho.

Vitambulisho ni vizuri lakini wanaopaswa kupewa vitambulisho hawapewi. Hilo ni kasoro. Tumeshapiga kelele sana, tumeshazungumza sana, hatuna lugha nyengine ya kuzungumza wanaotaka watasikia na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu awajaalie wasikie, kwamba tufike pahala wote wanaohusika kama alivyosema Mnadhimi kwamba, basi japo baada ya uchaguzi, lakini kila mtu apewe haki yake.

Mwisho katika hilo, idara iache ile tabia ya baada ya miaka miwili, mitatu kubadilisha vitambulisho. Gharama za kuchapisha hivi vitambulisho ni kubwa sana, sasa angalau kitambulisho kikitengenezwa kikao muda mkubwa kabla ya kubadilisha ili kuipunguzia serikali gharama ambayo haistahiki. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru ahsante.

Mhe. Zakiya Omar Juma: Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa nafasi ya kuzungumza machache. Nitajitahidi kwa sababu mambo ni mengi. Lakini nataka nianze na wenzetu hawa wa vikosi na nianze kwa bango ambalo mama taifa anapenda kuitumia. Mama Salma Kikwete siku zote anasema kwamba, ‘Mtoto wa mwenzio na wewe ni wako’.

Mhe. Mwenyekiti, sikufichi katika waliolengalenga machozi mmoja alikuwa mimi na kwa kweli inauma sana kwa sababu sisi ni wazazi na wale ni watoto wetu. Watoto siku zote na ndio maana wakaitwa watoto ni watu wenye kukosea na wakataka kunyooshwa. Kwa maana hiyo, Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana Mhe. Waziri na ninaiomba serikali kupitia wizara hii kwamba sasa jela ya watoto isiwe ni sehemu kama ambavyo ilivyo sasa hivi, hata kama watatenganishwa, bado nasema ombi langu watoto wanahitaji malezi,

wanahitaji mafunzo. Wao jela yao iwe ni sehemu ya mafunzo kwa maana ya mafunzo, katika wakati huo anapokuwa kwenye eneo hilo waelimishwe kwa maana ya kupewa masomo kama wako skuli, wafunzwe na kuwekwa katika msatari wa maadili, lakini pia wapewe na muda wa kucheza kupumzika kwa sababu bado ni watoto.

Vyenginevyo Mhe. Mwenyekiti, serikali inapozalisha majangili kwa mkono wake. Hali iliyoelezwa hapa si nzuri hata kama ni watoto wa kike au wa kiume, ni kuwaharibia maisha yao. Lakini pia ni kuwaathiri kisaikolojia na wanapotoka pale tusitarajie kwamba tunapata tena watoto tutapata wezi, majambazi, majangili, magaidi kwenda mbele. Kwa hivyo, kupitia chombo hiki Mhe. Mwenyekiti, kwa niaba ya wenzangu wote nasema Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tunalaani vikali matendo ambayo wanafanyiwa watoto wetu walioko katika mikono ya serikali katika eneo hilo la vikosi.

Pia napenda nirudie kwa kusisitiza Mhe. Mwenyekiti, naomba radhi sana, lakini kwa hili lazima tuseme, hatua kali zichukuliwe na Mhe. Waziri aanze kutueleza hapa hapa hatua ambazo zitachukuliwa. Kwa sababu muda umepita, matendo haya ni mengi kila siku tunasema lakini hali inazidi kuwa mbaya. Kwa hivyo, mimi binafsi peke yangu kama wote wataunga mkono mimi suingi mkono mpaka nipate maelezo ambayo nitaona hapa kweli serikali imedhamiria kulichukulia hatua suala hili.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na hivyo hivyo vikosi, kwa mujibu wa takwimu zote zilizokuwemo katika kitabu hiki inaonesha kwamba, jumla ya fedha ambazo zinaombwa ni shilingi 25.9 bilioni. Shilingi 19 bilioni peke yake zinakwenda kwenye vikosi, mimi nashukuru kwamba kaomba fedha nyingi. Sasa katika hili naomba kwamba lazima kupitia fedha hizi tuone kituo cha watoto ambacho mimi nakiita ni *special* cha mafunzo kinajengwa na tupate kauli hiyo katika bajeti hii angalau tuone ule mwelekeo kwamba upo. Hapo nitakuwa sina mashaka sana na hii bajeti.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo jambo jengine ninalotaka kuzungumza ni suala zima la vitambulisho. Nakubaliana na hoja au ile sifa tuliyopewa kwamba vitambulisho vyetu vina ubora wa hali ya juu. Hilo halina ubishi linaonekana, lakini pia napenda niseme kwamba na kasoro ipo. Kasoro ile ndio inayopelekea sasa kuiingiza tena serikali katika gharama na hasara mpya. Vitambulisho vyetu Mhe. Mwenyekiti, vina *expire date*, jambo ambalo nafikiri dunia nzima hakuna. Kwa hivyo, naomba sana hivyo vitambulisho vipya vitakavyotengenezwa hicho kitu cha *expire date* kwanza kisiwepo, hilo la mwanzo.

Lakini la pili matatizo na kelele nyingi tunazopiga nafikiri pia ni kule kukataa mapendekezo tuliokuwa tukiyatoa wakati sheria ya vitambulisho inapitishwa. Mhe. Mwenyekiti, vitambulisho si Zanzibar tu, lakini dunia nzima na hususan nchi ambazo zimeendelea na nitasema zile ambazo nimekwenda mwenyewe *physical* nimeona jinsi gani wenzetu wanafanya. Kitambulisho cha Uzanzibari au kwa nchi nyengine yoyote maana yake ni haki ya kila Mzanzibari au mwananchi wa nchi hiyo, ni tofauti na sisi. Tumekiwekwa kwamba kina watu maalum. Kigezo cha kusema kwamba vitambulisho vianze kwa mtu mwenye miaka 18 ni kasoro.

Wenzetu kitambulisho kinatoka kutoka siku moja amezaliwa mtoto, inawezekana akakipata baada ya wiki au wiki mbili, lakini kinatolewa wakati mtoto amezaliwa na ile ndio inakuwa usajili wake katika nchi ile wanajua mpaka idadi ya watu wao, anapokufa mtu inakuwa rahisi, shughuli nyengine zote zinaanzia kutoka hapo. Kwa hivyo, inakuwa si tatizo mtu kwenda pahala akadaiwa kitambulisho, kila mtu anacho hawakubaguliwa.

Sasa sisi kwetu tumefanya kitambulisho mpaka utimie miaka 18 tena apende yule mtoaji. Kwa sababu kumdai mtu cheti cha kuzaliwa wenzetu ndio hiki kinachoitwa kitambulisho. Kwa hiyo naomba sana kwa sababu vinataka kutengenezwa vitambulisho vipya basi waone kuwa hivyo vitambulisho vipya apewe kila Mzanzibari na utaratibu uwekwe ikiwa kubadilisha kidogo sheria lakini iwe wakati mtu anazaliwa ile *registration* yake ndio ifuatane na kupata hicho kitambulisho ili kuondosha usumbufu mwengine ambao Mhe. Mwenyekiti, huwa unatokea.

Mhe. Mwenyekiti, katika suala la vitambulisho jambo zuri au ba ya sana ambalo lipo katika sheria hii ya vitambulisho ni kwamba, kukosa kitambulisho ni kosa la jinai. Sasa afisi ya vitambulisho pengine na hii sheria, lakini sheria inawezekana ikawa haina matatizo, lakini watendaji au. *implementation* ya hii sheria ndio inaleta matatizo. Tunawafanya Wazanzibari wetu ambao hawana makosa kwamba wana makosa ya kesi za jinai kwa kuwakosesha kuwapa haki yao.

Kwa hivyo, mimi naomba kama walivyoomba wengine itafutwe namna ya kuwa kila mmoja aweze kupata haki hii hasa tukiangalia kwamba tunaelekea katika chaguzi mbili muhimu sana kwa mwaka huu na kwa historia ya visiwa vyetu.

Mhe. Mwenyekiti, sitaki niwe na maneno mengi sana katika vitambulisho, lakini nataka pia nizungumzie suala zima la Baraza la Manispaa kwenye kifungu cha 79 ukurasa wa 48.

Mhe. Mwenyekiti, katika ukurasa huu kumezungumzwa maeneo ya wazi kama bustani, Jamhuri, Forodhani na vitu kama hivyo. Lakini mimi nina mawazo tofauti Mhe. Mwenyekiti, kuhusiana na hili eneo ambalo liko jirani yetu hapa. Mimi nilidhani kwamba *Jamhuri Garden* ingelipaswa kuwa na hadhi au sura kama ile ya Forodhani, tuone yale mandhari yake ya kijani bila ya kuwa na matatizo. Lakini leo katika kipindi cha muda mfupi sana tunaiona *Jamhuri Garden* jinsi ya mazingira yalivyochafuka na sijui kwa vigezo vipi ikatolewa nafasi ile kufanywa michezo ya watoto katika bustani ya aina ile.

Mimi naona pale palitakiwa kubaki bustani yenye miti na mauwa na haiba ya aina hiyo, kama kuna mambo ya michezo ya watoto yapo maeneo mengine ya wazi ambayo yangeweza kabisa kufanya shughuli ile. Ingekuwa si vibaya kusogezwa nje kidogo ya huu mji. Kwa sababu unapofanya shughuli kama hizo ule mrundikano wa watu pia unakuwa mkubwa. Hali za hewa na mazingira kama tunavyoambiwa mkusanyiko mkubwa wa watu pia unachangia uharibifu wa mazingira na ndio hali halisi ambayo ipo hapo.

Wenzangu wameuliza kutaka kujua ikiwa ni ubia, ikiwa imeuzwa au kiwa imekodishwa basi na mimi nasisitiza hilo tuelezwe. Lakini hivi ile sehemu ya jumba nambari 2 pale ambalo linaelekezeana na kituo cha daladala Michenzani, nahisi lilikuwa ni eneo muafaka kwa kufanya suala hili. Kulikuwa kuna kasoro gani mpaka ikaja ikachafuliwa? Mimi naona nikuchafuliwa mazingira ya *Jamhuri Garden* na kwa kweli ningependa sana katika masuala haya tusingekuwa tunaharibu haribu haya mazingira yetu. Kwa hivyo, tunahitaji maelezo zaidi kutoka kwako Mhe. Waziri utakapokuja kufanya majumuisho.

Vile vile niseme kuhusu ujenzi umpya uliopo katika soko kuu la Darajani, hapa tulikuta malalamiko wakati kamati yetu ilipotembelea. Sisi tulikwenda pale kama kukagua tu ujenzi, lakini kwa sababu wale wahusika wao hawakuwahi kutokana na majukumu mengi ambayo kamati inakuwa nazo, sasa wahusika wa pale wakatufuata sisi. Tatizo lililokuwepo pale Mhe. Mwenyekiti, ni juu ya ule ujenzi mpya. Kutokana na wale watu ambao miaka zaidi ya 40 wako pale na hali halisi inavyoendelea ya ujenzi upande ule wa soko la mboga mboga na upande huu sehemu ambayo ni maarufu kwa kuuza biashara ya ndizi.

Mhe. Mwenyekiti, katika sehemu hiyo kuna ujenzi mpya unaendelea, pia kuna tetesi za kwamba wahusika waliokuwa wanastahiki baada ya ujenzi huo waweze kupata nafasi pale, basi kuna malalamiko kwamba kuna maneno ya chini chini kuwa eneo lile ameshapewa mtu ndio anaendelea na huo ujenzi. Lakini kwa wale ambao watahitaji kupata maeneo ya kuendelea na biashara wametakiwa kutoa kiasi kikubwa cha fedha ili waweze kupata. Mhe. Mwenyekiti, nilitaka kujua ukweli wa suala hili Mhe. Waziri atakuwa anajua zaidi kwa kupitia Afisi hii ya Baraza la Manispaa.

Mhe. Mwenyekiti, halafu tulikuwa tunaona kwamba na suala hili tulilifanya hata kwa upande wa Forodhani wakati inatengenezwa, kwa sababu kamati yetu ilikuwa inahusika. Basi tulipendekeza kwamba wale wahusika yaani wafanyabiashara ambao walikuwepo tangu mwanzo basi wawe wa mwanzo kufikiriwa badala ya kumfikiria mtu mwenye pesa zake. Mhe. Mwenyekiti, mtu mwenye pesa zake anaweza akatafuta eneo akajenga kitega uchumi chake akaweka watu ikiwa anawauzia au kiwa anawakodisha.

Lakini watu ambao hawana uwezo wa kwenda kokote wako pale kwa biashara ya kuchuma kijio, kwa kweli kuwahamisha kwa namna hizi za kiutaalamu inakuwa sio vizuri. Kwa hivyo, tungependa kujua utaratibu mzima wa ujenzi wa pale na jinsi ya ugavi utakavyokuwa, ili tuone kwamba na hawa wafanyabiashara wadogo wadogo ambao wako pale kwa ajili ya kutafuta rizki pamoja na familia zao, hali yao itakuwaje baada ya ujenzi ule kukamilika.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nina ushauri kwa Baraza hili la Manispaa, kwamba wawe wabunifu. Sasa hivi mwenzangu Mhe. Makame Mshimba alipozungumza alisema kwamba watu wa manispaa wasubiri usiku wakapige minyororo gari zote zinazolala barabarani.

Mhe. Mwenyekiti, nataka niseme kwamba je, hatuoni kuwa litakapofanyika hili tutakuwa hatutendi haki, kwa sababu wenyewe Baraza la Manispaa wameshindwa hata ku-*create* kitu chochote kile ambacho sasa hivi si jambo la kuficha ni jambo la wazi kwamba kila mtu ana gari, labda watu wawili watatu ndi hawana. Je, waliyonayo hayo magari watayaweka wapi, juu varanda Michenzani kule hayawezi kukaa?

Sasa nilikuwa naiomba wizara ifanye utaratibu wa kutafuta eneo na maeneo yapo. Kuna lile eneo pale mbele ya hoteli ya bwawani, kama linaweza kutengenezwa vizuri, basi wanaweza kufanya *parking* ya magari wakaweza kuweka na vitu vyengine migahawa na kadhalika na Baraza la Manispaa likaweza kukusanya mapato, badala ya kuwa wao wanasubiri mtu.

Kwa mfano, Benki ya FBME pale wamejenga *parking* yao vizuri kwa ajili ya wateja wao, kwa sababu kule walikokuwa watu walikuwa wanapata usumbufu mkubwa. Lakini badala yake watu wengine wameshajenga *parking* halafu wao wanakuja kukusanya mapato. Sasa mimi nauliza hivi kweli hii ni haki. Sawa pengine sheria zimewekwa hivyo, lakini bado nadhani manispaa hapo haikutenda haki. Vyenginevyo labda wangetakiwa watowe Benki ya FBME kutoa *commission* na kitu kama hicho.

Kwa hivyo, ningewashauri kwamba na wao waone kuwa kutokana na hali halisi ambayo sasa hivi mji wetu inao basi watafute eneo na maeneo yapo ndani ya mji, ili wajenge *car parking* za kisasa ili waweze kupata mapato ya kutosha na ndani yake wanaweza kufanya na kitu changine. Kuna migahawa ambayo asubuhi wafanyakazi wanaweza kupata chochote au muda wowote mtu anaotaka na wanaweza kukusanya mapato ya kutosha.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia nataka nizungumzie suala la alama za barabarani. Kwa kweli mimi ninayekaa pale *roundabout* huwa napata mashaka makubwa sana. Madereva sasa hivi ni wengi na sijui kama utaratibu kama huwa unakamilika wa kupewa hizi leseni, lakini inaonekana hawaelewi hata maeneo ambayo wanatakiwa gari zisimame.

Kwa mfano, *round-about* pale katika makutano kuna barabara nane, lakini katika nane nne unatakiwa ukifika kama kuna gari imeshaingia kwenye *round-about* basi wewe unatakiwa usimame, hawasimami wanakwenda moja kwa moja na wakati mwengine ajali zinatokea, watu wanapata matatizo. Sasa hapa katika suala hili nilikuwa naomba manispaa ijaribu kuweka alama. Moja ya alama ambayo nilikuwa naomba iwekwe ni kuwa pachorwe mstari na iandikwe ile simama, kama ambayo imeandikwa pale nje. Maana yake labda wengine hawajui au wanahitaji kukumbushwa.

Pia eneo hili baina ya jumba nambari 8 na jumba nambari 7, Kisiwandui hapa, kuna skuli pale Mhe. Mwenyekiti. Bahati mbaya ni kwamba hii barabara inapotokea juu kule Michenzani kuteremka kuja Kisiwandui kuna kama mteremko kidogo, kwa hivyo ni hatari kwa watoto hasa wakati wanapotoka skuli na pia kuna skuli ya watoto wadogo pale. Kwa hivyo, nilikuwa naomba pawekwe ile mistari ya pundamilia yaani *zebra cross* ili kuwe na ule utaratibu wa watoto kuweza kuvuka badala ya kuwa wanasubiri paka wanaoendesha gari wapende kuwapisha. Sasa hili nilikuwa naomba sana Mhe. Mwenyekiti, alione na waweze kulifanya kwa haraka ili watoto wetu waweze kupata salama wakati wanatoka maskulini mwao. Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, ingawa muda ni mdogo.

Mhe. Abass Juma Muhunzi: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti. Naomba nianze moja kwa moja na kumpongeza waziri kwa hotuba yake hii.

Mhe. Mwenyekiti, serikali zetu za karne ya sasa hivi zinajaribu kama inavyowezekana kujipunguzia mzigo wa kufanyabiashara, mzigo wa matumizi ambayo yangeweza kufanywa pahala pengine. Ndio maana kukawa kuna uhuria wa soko huru, kukawa kuna sekta binafsi ambayo inapewa nguvu sana. Lakini vile vile kukawa kuna uwekezaji ambao unafanywa na sekta binafsi, yote ni serikali kujipunguzia mizigo.

Mhe. Mwenyekiti, eneo jengine ni hili la *decentralization* ambapo serikali inafanya kila inavyowezekana ili ule ushirikishwaji wa watu uwe sio kushirikishwa katika kufanyakazi tu, lakini katika kupanga mipango yao na kufanya maamuzi mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, niseme kwamba kwa serikali ya SMZ katika suala hili la ubinafsishaji na suala la sekta binafsi angalau imefanya kazi kidogo. Lakini katika suala hili la *decentralization* bado kuna mapungufu makubwa na ndio maana tuliomba sana, na Baraza limekuwa likiomba sana kwamba lazima kuwe na marekebisho makubwa ya serikali za mitaa, lakini hadi leo Mhe. Mwenyekiti, mambo haya hayajafanyika.

Mhe. Mwenyekiti, kuna umuhimu huu kwa sababu katika vijiji ambavyo wananchi wanaishi, kuna matatizo ambayo naweza kusema mara nyengine hata Serikali Kuu haina habari nayo. Kwa mfano, ukiangalia miradi hii ya barabara ambayo imezungumzwa humu, ni barabara kuu pamoja na *fader roads*, lakini zile barabara ambazo zinaunganisha vijiji ambazo zinafanya jimbo halafu kwenda ndani ya wilaya, inawezekana kabisa serikali ikawa hata habari nazo hizo, pengine hata kwenye mipango yao haimo. Ilikuwa ni kazi ya serikali za mitaa kuweza kupewa nguvu zikafanya maamuzi ili kuweza kufanya kazi hizo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mfano leo Mtangani iko katika Jimbo la Kiwani, lakini Mtangani huna *connection* ya aina yoyote iliyo nzuri ya kuweza kupita mule katika jimbo lake ukawa unatoka Mtangani unakwenda Kichaka, unakwenda Chwaka, unakwenda Mkiwani halafu unakwenda Mwambe, hiyo *connection* hasa huioni. Lakini ni barabara na watu wengi wanaishi.

Mhe. Mwenyekiti, mfano ukija Chambani. Chambani kilomita 3.2 ndizo zinazotajwa kwenye vitabu vyote vya bajeti, ingawa hakuna jambo lolote limeanza. Lakini kilomita 3.2 ni kutoka Kenya mpaka Miamboni. Lakini kuna *ring road* inayounganisha ile Chambani, inayopita Ukutini na kwenda Matele, inakwenda Chwale inakuja zake Tumbini na inakuja tena Miamboni. Hapo kuna wakaazi zaidi ya 10,000, lakini hawana pahala pa kupita.

Mhe. Mwenyekiti, ukija katika masuala ya elimu. Miradi mingi sana inakwenda kule kwenye elimu, lakini uendelevu ndio tatizo. Kuna mabanda ambayo yanajengwa unakwenda unaliona, baada ya miaka mitano pesa zimekwishaingia hizi, lakini banda hili miaka mitano haliwezi kuwa hai tena. Kwa hivyo, uendelevu wa miradi ya aina hii ambayo pesa zinatupwa tu bila ya kuwa na usimamizi ulio madhubuti hili ni tatizo. Mradi wowote ambao unaleta maendeleo ni lazima uwe ni mradi ambao utakuwa endelevu.

Mhe. Mwenyekiti, halikadhalika kwenye afya na sekta nyengine. Yote hayo nasema ili kutilia nguvu hoja ya kuwa na serikali za mitaa zilizo madhubuti sana. Mhe. Mwenyekiti, mambo mengine sasa hivi katika nchi nyingi hayasimamiwi tena na serikali kuu. Hizi skuli za *primary* leo tunaziongezea na chekechea za kulea watoto.

Mhe. Mwenyekiti, bado kelele ambazo tunapiga hapa kuhusu *reform* za serikali za mitaa, ni jambo muhimu na la msingi sana. Serikali kwa sababu ni muda mkubwa sana imekuwa ikitoa ahadi kwamba serikali ita- *reform*, italeta *document*

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe nawashukuru sana kwa mashirikiano yenu. Katika orodha yetu bado nina wajumbe 9 wamebakia na hoja hii tunatakiwa asubuhi tuikamilishe. Sasa na kesho asubuhi pia tutaomba mashirikiano yenu. Kwa hivyo, sasa hivi naomba kuahirisha kikao hiki mpaka kesho asubuhi tarehe 23/06/2010 saa 3:00.

(*Saa 1:45 usiku Baraza liliahirishwa mpaka tarehe 23/06/2010 saa 3:00 za asubuhi)*